# Kiswahili

## kwa

## Shule za Rwanda

### Kidato cha 3

### Kitabu cha Mwanafunzi

© 2020 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Haki zote zimehifadhiwa.
Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi
wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# DIBAJI

Mwanafunzi mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa Kitabu cha Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari.

Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri maisha yake na kumpa fursa ya kujipatia ajira au kuandaa miradi mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii anamoishi.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza kuhusu umuhimu wa kufungamanisha shughuli za ujifunzaji na ufundishaji pamoja na zana na mitaala ili kufanikisha mchakato mzima wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale yanayofundishwa na uwezo waupatao wanafunzi. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Hivyo basi, kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza unaokuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti ya kibinafsi na yale utakayofanya katika makundi kwa msaada wa walimu ambao huwajibika kufanikisha ufundishaji. Aidha, utapata stadi muhimu zitakazokuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha mbalimbali ya maisha halisi ili uweze kuonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Mwelekeo uliozingatiwa katika kitabu hiki unatofautiana na ule uliotiliwa maanani katika mfumo wa zamani ambapo mchakato wa kujifunza ulifanywa kwa kutilia mkazo upataji wa maarifa kutoka kwa mwalimu ambaye pia alifikiriwa kumzidi mwanafunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi. Kwa hiyo, dhana huanzishwa aghalabu kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na kupata maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya ujifunzaji hujihusisha na shughuli mbalimbali zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri kuhusu yale anayoyafanya, kuonyesha uzoefu wake halisi na maarifa aliyonayo katika mchakato huo wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, utakuwa na majukumu yafuatayo ili uweze kutumia kitabu hiki kwa ufanisi:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi au mazoezi yanayolenga kwenye mada;
- Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kupitia mawasilisho, mijadala, kazi za makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama vile michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, mitandao na hata nje ya shule;
- • Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa /mtandaoni, wataalamu na kuwasilisha matokeo ya utafiti;
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi ulizopewa kupitia maelezo na majadiliano kila unapoongea hadharani;
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi yako ya ujifunzaji.

Mwishowe, ningependa kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki na kutoa mchango wao kwa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioongoza mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu kutoka shule tofauti kwa kuendeleza na kufanikisha kazi hii. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB**


RWANDA BASIC EDUCATION BOARD (REB)

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki, jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziwaendee viongozi wa shule mbalimbali walioruhusu walimu wao kufanya kazi na Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi katika mradi wa ukamilishaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu ambao juhudi zao na uandikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, shukrani ziwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.



**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

# Yaliyomo


DIBAJI....................................................................III
SHUKRANI..............................................................V
UTANGULIZI.............................................................1
SURA YA KWANZA .................................................... 3
MADA KUU 1: LUGHA NA MAZINGIRA .................... 3
MADA NDOGO: Utalii nchini Rwanda ............................ 3
Somo la 1: Ofisi ya utalii .............................................................. 3
1.1 Mazungumzo kati ya Mpokeaji na Mtalii ............................................ 3
1.2 Msamiati kuhusu utalii.............................................................................. 5
1.3 **Matumizi ya lugha:** Aina mbalimbali za pesa ................................ 6
1.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo........................................... 8
1.5 **Sarufi:** Viulizi '*nani*' na '*nini*' ............................................................ 8

Somo la 2: Mbuga za wanyama.................................................... 10
2.1 Kifungu kuhusu mbuga za wanyama nchini Rwanda ........................ 10
2.2 Msamiati kuhusu mbuga za wanyama ................................................ 12
2.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ........................................................ 15
2.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ........................................ 16
2.5 **Sarufi:** Kiulizi '*lini*' ...................................................... 16

Somo la 3: Mwelekezaji na Mtalii ................................................ 18
3.1 Mazungumzo kati ya Mwelekezaji na Mtalii ...................................... 18
3.2 Msamiati kuhusu ziara ya kitalii .......................................................... 20
3.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ...................................................... 22
3.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ............................................... 23
3.5 **Sarufi:** Viulizi '*wapi*' na '*vipi*' ........................................................... 23

**Somo la 4: Utamaduni na utalii .................................... 27**
4.1 Kifungu kuhusu utamaduni na utalii ................................................ 27
4.2 Msamiati kuhusu utamaduni ......................................................... 29
4.3 **Matumizi ya lugha:** Zoezi la msamiati ............................................. 31
4.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano .................................... 31
4.5 **Sarufi:** Wakati wa mazoea, tungo yakinishi ...................................... 32

**Somo la 5: Milima yetu ................................................ 34**
5.1 Kifungu kuhusu 'milima yetu' ........................................................ 34
5.2 Msamiati kuhusu 'milima yetu' ................................................... 36
5.3 **Matumizi ya lugha:** Zoezi la jedwali ............................................. 37
5.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ..................................... 39
5.5 **Sarufi:** Wakati wa mazoea, tungo kanushi ........................................ 39

**Somo la 6: Maji yetu ................................................... 42**
6.1 Kifungu kuhusu 'maji yetu' .......................................................... 42
6.2 Msamiati kuhusu 'maji yetu' ......................................................... 44
6.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano.................................................... 45
6.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ...................................... 46
**6.5 Sarufi:** Kiulizi '*-pi*'............................................................................ 47
**Tathmini ya mada ya 1** ............................................................. 48
**Faharasa** ................................................................................. 50

SURA YA PILI .................................................................... 51
MADA KUU 2: LUGHA NA MATUKIO YA KIJAMII NA KITAIFA .................................... 51
MADA NDOGO: Sikukuu na sherehe nchini Rwanda ......... 51
Somo la 7: Sikukuu na sherehe katika kalenda ................ 51
7.1 Kifungu kuhusu sikukuu na sherehe nchini Rwanda ......................... 51
7.2 Msamiati kuhusu sikukuu nchini Rwanda ............................................ 53
7.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano .................................................. 54
7.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ............................................. 54
7.5 **Sarufi:** Matumizi ya wakati uliopita ................................................ 55
7.6 **Sarufi:** Matumizi ya wakati ujao ........................................................ 58
Somo la 8: Maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda......... 61
8.1 Shairi kuhusu maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda .................... 61
8.2 Msamiati kuhusu maadhimisho mbalimbali ........................................ 62
8.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ........................................................ 63
8.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Zoezi la mazungumzo ....................... 63
8.5 **Sarufi:** Vitenzi vya silabi moja .......................................................... 65
Somo la 9: Matumizi ya kalenda ya mwaka ...................... 69
9.1 Mazungumzo kuhusu kalenda ya mwaka ............................................ 69
9.2 Msamiati kuhusu kalenda ya mwaka ................................................... 71
9.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ....................................................... 71
9.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ............................................... 73
9.5 **Sarufi:** Matumizi ya herufi kubwa na alama za uandishi .................... 73
Tathmini ya mada ya 2 ........................................................................ 75
Faharasa ............................................................................................. 78

SURA YA TATU ........................................................ 79

MADA KUU 3: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO ................................ 79

MADA NDOGO: Midahalo na mijadala kuhusu shughuli za maendeleo na uzalishajimali dhidi ya umaskini nchini .................................. 79

Somo la 10: Mdahalo .................................................. 79

10.1 Mdahalo kuhusu '*Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi kuliko biashara*' .................................................. 79

10.2 Msamiati kuhusu mdahalo .................................................. 82

10.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano .................................................. 83

10.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kuandaa mdahalo ........................... 85

10.5 **Sarufi:** Wakati uliotimilika, tungo yakinishi .................................... 86

Somo la 11: Mjadala .................................................. 90

11.1 Mjadala kuhusu '*Nafasi ya ukulima katika uzalishajimali dhidi ya umaskini*' .................................................. 90

11.2 Msamiati kuhusu ukulima .................................................. 92

11.3 **Matumizi ya lugha:** Zoezi la jedwali.......................................... 93

11.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kuandaa mjadala ........................... 94

11.5 **Sarufi:** Kauli asili na kauli taarifa .................................................. 94

Somo la 12: Mjadala .................................................. 97

12.1 Mjadala kuhusu '*Ufugaji kama njia ya kupigana na umaskini nchini*'.................................................. 97

12.2 Msamiati wa mjadala kuhusu ufugaji .............................................. 99

12.3 **Matumizi ya lugha:** Kuunda maneno kamili ............................... 100

12.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Kuandaa mjadala ........................... 101

12.5 **Sarufi:** Mabadiliko ya kauli asili na kauli taarifa ............................ 101

Tathmini ya mada ya 3 .................................................. 103

Faharasa .................................................. 107

**SURA YA NNE** ........................................................ **108**
**MADA KUU 4: UIMARISHAJI WA STADI YA UANDISHI NA MASIMULIZI KUPITIA LUGHA YA KISWAHILI** .................................... **108**
**MADA NDOGO: Utungaji wa insha** ................................. **108**
**Somo la 13: Sehemu kuu za insha** ................................. **108**
13.1 Kifungu kuhusu somo la Kiswahili ............................................. 108
13.2 Msamiati kuhusu sehemu za insha ................................................ 110
13.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ................................................ 111
13.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Somo la imla ................................ 112
13.5 **Sarufi:** Ngeli ya U-ZI ................................................................ 112
**Somo la 14: Mambo ya kuzingatia katika kuandika nsha:** ...................................... **117**
14.1 Kifungu kuhusu malezi bora ........................................................ 117
14.2 Msamiati kuhusu uandishi wa insha .......................................... 119
14.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ................................................ 120
14.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ................................ 120
14.5 **Sarufi:** Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria ...................... 120
**Somo la 15: Aina mbalimbali za insha** ............................. **124**
15.1 Kifungu kuhusu umuhimu wa adabu .......................................... 124
15.2 Msamiati kuhusiana na umuhimu wa adabu .................................. 125
15.3 **Matumizi ya lugha:** Mifano ya insha ........................................ 126
15.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Somo la imla ................................ 129
15.5 **Sarufi:** Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi ................. 130
**Somo la 16: Aina za insha**............................................. **133**

16.1 Kifungu kuhusu madhara ya uvivu ........ 133
16.2 Msamiati kuhusu madhara ya uvivu ........ 134
16.3 **Matumizi ya lugha:** Aina za insha ........ 135
16.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Somo la imla ........ 138
16.5 **Sarufi:** Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi ........ 138
**Tathmini ya mada ya 4 ........ 141**
**Faharasa ........ 143**

**SURA YA TANO ........ 144**
**MADA KUU 5: LUGHA NA TEKNOLOJIA ........ 144**
**MADA NDOGO: Kiswahili katika teknolojia ya habari na mawasiliano ........ 144**
**Somo la 17: Simu ya mkononi ........ 144**
17.1 Mazungumzo kuhusu matumizi ya simu ya mkononi ........ 144
17.2 Msamiati kuhusu simu ya mkononi ........ 146
17.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ........ 147
17.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ........ 148
17.5 **Sarufi:** Hali ya kuomba, tungo yakinishi ........ 148

**Somo la 18: Matumizi ya tarakilishi ........ 149**
18.1 Kifungu kuhusu matumizi ya tarakilishi ........ 149
18.2 Msamiati kuhusu matumizi ya tarakilishi ........ 151
18.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ........ 152
18.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ........ 153
18.5 **Sarufi:** Hali ya kuomba, tungo kanushi ........ 153

**Somo la 19: Redio na runinga ........ 155**

19.1 Kifungu kuhusu matumizi ya redio na runinga ................................ 155
19.2 Msamiati kuhusu matumizi ya redio na runinga ................................ 157
19.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ................................ 157
19.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Maigizo ................................ 158
19.5 **Sarufi:** Hali ya kuamrisha, tungo yakinishi ................................ 158
**Somo la 20: Barua kwa mhariri ................................ 160**
20.1 Kifungu kuhusu barua kwa mhariri ................................ 160
20.2 Msamiati kuhusu barua kwa mhariri ................................ 162
20.3 **Matumizi ya lugha:** Majadiliano ................................ 162
20.4 **Kusikiliza na kuzungumza:** Majadiliano ................................ 163
20.5 **Sarufi:** Hali ya kuamrisha, tungo kanushi ................................ 163

**Tathmini ya mada ya 5 ................................ 165**
**Faharasa ................................ 167**
**Marejeleo ................................ 168**

# UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hayo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi nchini Rwanda na hata katika jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari nchini Rwanda.

Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki imegawanywa katika masomo. Masomo haya yamegusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu
- Matumizi ya msamiati wa msingi
- Sarufi
- Kusikiliza na kuzungumza
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwa sababu Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo, utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu mauaji

ya kimbari, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu ujinsia na elimu jumuishi.

Ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya kazi zilizotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki. Kazi nyingi zilizopendekezwa zitamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa Kudumu. Vilevile, kazi za mijadala ya kibinafsi na ya makundi zote zitasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha.

Kazi za makundi zilizopendekezwa zitamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi akumbuke kwamba kitabu hiki kinafuata vitabu vingine vya Kiswahili ambavyo viliandaliwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na kidato cha pili nchini Rwanda. Kwa hiyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa awali wa kutosha ambao utamwezesha kuelewa mada zilizotolewa katika kitabu hiki kwa kuhakikisha kwamba amepata uwezo wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za maisha.

# SURA YA KWANZA

## MADA KUU 1: LUGHA NA MAZINGIRA

### MADA NDOGO: Utalii nchini Rwanda

### SOMO LA 1: Ofisi ya Utalii

### 1.1 Mazungumzo kati ya Mpokeaji na Mtalii

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kueleza kinachoendelea au mnachokiona katika mchoro huu.*




*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni kifungu cha mazungumzo yafuatayo kati ya Mtalii na Mpokeaji wa watalii kisha mjibu maswali yanayofuata.*

**Mpokeaji:** Karibu, karibu sana katika ofisi yetu ya utalii.
**Mtalii:** Asante sana.
**Mpokeaji:** Mimi ninaitwa Nezi. Nikusaidie vipi?
**Mtalii:** Mimi ninaitwa Jane kutoka Ujerumani. Nina lengo la kuzuru mazingira yenu.
**Mpokeaji:** Karibu sana. Rwanda ni nchi nzuri ambayo ina mazingira

yanayovutia. Ungependa kuanza ziara yako lini?

**Mtalii:** Naomba kwanza unieleze kuhusu vivutio vya kitalii vilivyopo nchini humu ili niweze kufanya uamuzi wangu.

**Mpokeaji:** Sawa. Nchi yetu ina vivutio vingi: mbuga za wanyama, mito, milima mizuri pamoja na nyumba za kuhifadhia utamaduni wetu. Je, ungependa kuzuru mazingira ya aina gani?

**Mtalii:** Kwa sasa ningependa kuzuru mojawapo ya mbuga za wanyama. Mna mbuga gani za wanyama ili niweze kuchagua?

**Mpokeaji:** *(Anachukua ramani)* Unaweza kutalii *(anamwonyesha ramani)* eneo hili la mbuga ya wanyama ya Akagera, hii ni mbuga ya wanyama ya milima mirefu (Virunga) na sehemu hii ni ya mbuga ya wanyama ya msitu wa Nyungwe.

**Mtalii:** Naona kweli kuna mahali pengi pa kutalii. Nimependa sana mazingira ya Akagera na yale ya milima mirefu ya Virunga. Nafikiria kurudi Rwanda mwaka ujao ili nitalii mahali kwingi.

**Mpokeaji:** Je, utakaa nchini humu kwa muda gani?

**Mtalii:** Nina wiki mbili tu na ninataka kuzitumia vizuri. Naomba kujua bei ya kuruhusiwa kuingia katika mbuga.

**Mpokeaji:** Aaah! Bei ni nafuu. Ili uingie katika kila mbuga utalipa kiingilio kisha utapewa mwelekezaji wa watalii katika kila mbuga.

**Mtalii:** Watu huingia na kutoka mbugani saa ngapi?

**Mpokeaji:** Kwa kawaida, watu huingia mbugani asubuhi na hutoka jioni.

**Mtalii:** Natarajia kuanza ziara yangu kesho asubuhi. Unaweza kunipa maelekezo kuhusu hoteli ya kutumia kwa wiki mbili?

**Mpokeaji:** Hoteli ni nyingi sana na nzuri. Hizi hapa nambari za simu. Ufikapo mahali panapoitwa Musanze, piga mojawapo ya nambari hizi ili utengewe chumba cha kulala pamoja na maakuli. Nambari hii nyingine utaitumia ukiwa mjini Kigali na hii hapa utaitumia ukiwa katika sehemu za Akagera.

**Mtalii:** Asante sana. Naomba unipe akaunti yenu ili niweze kulipa kiingilio cha mbuga hizo za wanyama. Je, kuna kampuni ya kutoa huduma za magari ya kutumiwa na watalii?

**Mpokeaji:** Ndiyo! Hii hapa orodha ya kampuni hizo, aina za magari ya kutumia na bei zake kwa siku pamoja na nambari zao za simu.

**Mtalii:** Vizuri sana. Asante sana na kwaheri.

**Mpokeaji:** Karibu sana. Kwaheri ya kuonana na karibu tena.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu cha mazungumzo kilicho hapo juu kati ya Mtalii na Mpokeaji, kisha mjibu maswali haya.*

1. Mtalii anatoka katika nchi gani? Yeye anataka nini?
2. Taja vivutio vya utalii vilivyopo nchini Rwanda.
3. Mtalii atatembelea vivutio gani?
4. Mtalii atachukua muda gani nchini Rwanda?
5. Umuhimu wa mwelekezaji wa watalii ni upi?
6. Watu huruhusiwa kuingia katika mbuga za wanyama kuanzia saa ngapi na hutoka saa ngapi?
7. Mtalii atatumia nambari za simu alizopewa kufanya nini?
8. Mtalii ataanza shughuli yake ya kuzuru maeneo mbalimbali lini?
9. Mtalii atatumia nini kusafiri hadi kwenye mbuga za wanyama?
10. Huduma za hoteli kwa Mtalii ni zipi?

## 1.2 Msamiati kuhusu utalii

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya katika kifungu cha mazungumzo mlichosoma hapo juu kisha muutolee maelezo. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale panapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***mbuga*** – sehemu maalum ya kuwahifadhia wanyamapori

**Zoezi la 1.1**

A. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi hizi kisha mtunge sentensi zenu sahihi kwa kutumia msamiati huo.*

1. ***Mtalii*** huyu kutoka nchi ya Ujerumani anataka kujua maeneo mazuri ya kuzuru nchini.
2. Maeneo mengi ya nchi yetu ***yanavutia*** watalii wengi.
3. Mtalii huyu anataka ***kuzuru*** wilaya ya Korongi ili aweze kutazama ziwa Kivu.
4. Simba wengi walileta katika ***mbuga ya wanyama*** ya Akagera.
5. Mbuga ya Wanyama ya Akagera ni ***kivutio*** muhimu cha utalii nchini Rwanda.

6. Mtalii huyu aliamua kufanya ***ziara*** ya kitalii ya siku tano nchini mwetu.
7. Nchi yetu ***inatarajia*** kupokea watalii elfu themanini na watano mwaka huu.
8. Mimi ninaona heri niondoke katika sehemu hii; sitaki ***wanyama wakali*** wanipate hapa.
9. Unaweza kufanya ziara yako ya ***kitalii*** mjini Kigali kwa bei nafuu.
10. Watalii hufurahia ***mazingira*** ya Akagera.

B. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika Zoezi la 1A*

## 1.3 Matumizi ya lugha: Aina mbalimbali za pesa

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni pesa zifuatazo kisha mziambatanishe kwa usahihi na nchi zinakotumika.*

| Pesa | Nchi |
|---|---|
| <br>*1. Faranga elfu tano* | *Tanzania* |
| <br>*2. Shilingi mia moja* | *Rwanda* |
| <br>*3. Shilingi elfu moja* | *Kenya* |

| | |
|---|---|
| <br>*4. Shilingi mia tano* | *Marekani* |
| <br>*5. Dola tano* | *Uganda* |

## Zoezi la 1.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, ambatanisheni aina za pesa zilizo katika sehemu A na nchi zinakotumika katika sehemu B kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** Faranga - Rwanda

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Faranga | A. Japani |
| 2. Yeni | B. Naijeria |
| 3. Dola | CH. Rwanda |
| 4. Naira | D. Uganda |
| 5. Shilingi | E. Marekani |

## Zoezi la 1.3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, onyesheni aina za pesa ambazo hutumiwa katika nchi zifuatazo kwa kutunga sentensi sahihi.*

**Kwa mfano:** Tanzania

**Jibu:** Nchi ya Tanzania hutumia **shilingi ya Tanzania.**

1. Ubelgiji
2. Uingereza
3. Kanada
4. Malawi
5. Afrika Kusini

### Zoezi la utafiti

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, badilisheni pesa za kigeni zifuatazo ziwe katika faranga za Rwanda kama ilivyo sasa hivi.*

**Kwa mfano:**

Shilingi elfu moja za Kenya = Faranga elfu saba na mia tano za Rwanda

1. Dola hamsini za Marekani
2. Shilingi mia mbili za Uganda
3. Shilingi hamsini za Tanzania
4. Yuro tano za Ulaya
5. Naira mia moja za Naijeria

## 1.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, igizeni mazungumzo mliyosoma hapo awali kati ya Mtalii na Mpokeaji.*

## 1.5 Sarufi: Viulizi '*nani*' na '*nini*'

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi zifuatazo kisha mfanye mazoezi yanayofuata.*

1. ***Nani*** atamaliza wiki mbili nchini Rwanda?

   **Jibu:** Mtalii.
2. ***Nini*** kinavutia katika mbuga ya Akagera?

   **Jibu:** Wanyamapori kwa mfano: simba.
3. ***Nani*** alimpa mtalii maelezo kuhusu hoteli ya kuishi?

   **Jibu:** Mpokeaji wa watalii.
4. ***Nani*** atarudi mwaka ujao kwa shughuli za utalii?

   **Jibu:** Mtalii.
5. Ni ***nini*** mtalii atalipa ili kuzuru mbuga ya wanyama?

   **Jibu:** Pesa za kiingilio

### Zoezi la 1.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, ulizeni maswali mliyosoma hapo juu kwa kuanza na kiulizi '**je**'.*

**Kwa mfano:**

*Je*, ni nani atamaliza wiki mbili nchini Rwanda?

## Zoezi la 1.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi hizi kwa jibu sahihi kutoka kwenye mabano.*

1. ____________ anaishi kwenye jumba hili? (*Nini, Nani*)
2. _____________ anaitwa Uwase? (*Nini, Nani*)
3. ______________ kitapikwa leo jioni? (*Nani, Nini*)
4. _____________ kitatumiwa kuandikia barua hii? (*Nani, Nini*)
5. _____________ hajawahi kuwaona wanyama wakali? (*Nini, Nani*)

### Maelezo muhimu!

- Maneno yaliyopigiwa mistari huitwa ***viulizi***. Haya ni maneno ambayo hutumiwa kuulizia maswali.

**Kwa mfano:**

***i)*** ***Nani*** *alikulipia karo ya muhula uliopita?*

- Neno '***nani'*** linauliza kuhusu mtu aliyetenda kitendo cha kulipa karo.

***ii)*** ***Nini*** *kimekuhuzunisha?*

- Neno '***nini'*** linauliza kuhusu kitu au jambo ambalo limemhuzunisha anayehusika.
- Maneno '***nani'*** na '***nini'*** hayaongezewi viambishi ngeli vyovyote.

## Zoezi la 1.6

*Tunga sentensi tano sahihi kwa kutumia kiulizi '**nani'** na sentensi nyingine tano sahihi kwa kutumia kiulizi '**nini'**.*

## SOMO LA 2: Mbuga za wanyama

### 2.1 Kifungu kuhusu mbuga za wanyama nchini Rwanda

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini kuhusu mnachokiona katika picha hizi kisha, mjitokeze mbele ya wanafunzi wenzenu ili muwaeleze. Baadaye, msome kifungu kinachofuata cha habari kuhusu mbuga za wanyama zinazopatikana nchini Rwanda.*



*Wanyamapori katika mbuga ya Akagera*



*Ndege katika msitu wa Nyungwe*



*Milima ya Virunga na sokwewatu*

Rwanda ni nchi nzuri iliyo katikati ya bara la Afrika. Rwanda ina vivutio vingi vya kitalii. Miongoni mwa vivutio vya kupendeza ni pamoja na mito mbalimbali, mbuga za wanyama, misitu ya kiasili, hoteli nzuri, maziwa, milima mirefu na hata nyumba za kuhifadhia vifaa vya utamaduni.

Mbuga za wanyama zinapendwa na watalii wengi. Mbuga ya wanyama ya Akagera inapendwa na watu wengi. Mbuga hii ina wanyama wengi: pundamilia, swara, paa, twiga, tembo, vifaru, simba, na wengine wengi. Mbuga hii ina mandhari ya kipekee: savana ya kupendeza watu wengi, sehemu kubwa ya majimaji yenye mto mkubwa wa Akagera, maziwa mengi na visiwa mbalimbali.

Sehemu hii inapakana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Milima yake mingi ina mimea ya aina tofauti. Nyasi ndogo ndogo kwenye vilele vya milima pamoja na savana yenye miti midogo midogo hadi misitu mikubwa hupatikana katika eneo hili. Kwa sababu hiyo, wanyama hupenda kuishi katika mazingira hayo ya kuvutia na watalii wengi hupenda kuyatazama mazingira yake.

Mbuga ya wanyama ya milima mirefu ya Virunga nayo inavutia sana watalii kutoka mataifa mbalimbali. Mbuga hii inapatikana sehemu za Kaskazini Magharibi mwa Rwanda kuanzia kwenye mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hadi mpaka wa Rwanda na Jamhuri ya Uganda. Sehemu hii ina milima mingi mirefu inayovutia macho. Miongoni mwa milima hiyo ni pamoja na milima ya *Kalisimbi, Muhabura, Bisoke, Sabyinyo*, *Nyamuragira* na *Nyiragongo*. Mbuga hii inajulikana kwa wanyama wanaoitwa "*sokwewatu*". Wanyama hawa wanapenda kuishi mahali penye milima mirefu kama hiyo. Watu wengi hupenda kuwatazama kutokana na maumbile yao na tabia zao zinazofanana na tabia za binadamu. Kila mwaka, Rwanda huandaa sikukuu ya kuwapa watoto wao majina na watu wengi hushirikishwa katika shughuli hii.

Mbuga ya wanyama ya msitu wa Nyungwe nayo hutembelewa na watalii wengi. Ni mbuga inayopatikana katika sehemu za Magharibi mwa Rwanda kuanzia msitu wa Kibira nchini Burundi. Msitu huu unajulikana kwa miti yake ya aina mbalimbali pamoja na aina nyingi za ndege wasiopatikana mahali pengi ulimwenguni. Mazingira haya yanavutia sana na wageni hulipa pesa nyingi kuja kutembelea nchi yetu na kuzuru maeneo haya.

Licha ya manufaa mengi ya kiuchumi tunayopata kutokana na shughuli za kitalii, kuna idadi ndogo ya Wanyarwanda ambao mpaka sasa hawajaelewa umuhimu wake. Baadhi yao hujiingiza katika vitendo vya kuwinda, kuwaua wanyamapori kiharamu na kufanya biashara za magendo za kuuza pembe za tembo baada ya kuwaua. Kwa sababu hiyo, wito umetolewa ili shughuli kama hizo zikomeshwe. Kila mwananchi anapaswa kuchangia katika kulinda wanyama hao ili waweze kuongezeka na kuendelea kutuletea fedha nyingi za kigeni na kuendeleza uchumi wetu.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena kifungu cha habari kuhusu mbuga za wanyama kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Nchi ya Rwanda inapatikana wapi?
2. Je, ni vivutio gani vya utalii vinavyopatikana nchini Rwanda?
3. Mbuga ya wanyama ya Akagera inahifadhi wanyama gani?
4. Eleza sifa za mbuga ya Akagera.
5. Mbuga ya wanyama ya milima mirefu inapatikana katika sehemu gani? Taja milima mirefu minne inayopatikana hapo.
6. Mbuga hii inasifiwa kwa sababu ya kuwa na wanyama gani? Kwa nini wanyama hao wanapendwa sana na watalii?
7. Je, ni sherehe gani inayofanywa kila mwaka kuhusiana na wanyama hao?
8. Mbuga ya wanyama ya msitu wa Nyungwe inajulikana kwa sifa gani?
9. Je, ni faida gani tunazopata kutokana na shughuli ya utalii?
10. Ni mambo gani yanayostahili kukomeshwa ili utalii uweze kuendelea na kustawi?

## 2.2 Msamiati kuhusu mbuga za wanyama

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya katika kifungu cha habari mlichosoma kisha mueleze maana ya msamiati huo. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale panapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***msitu*** – eneo kubwa lisilokuwa na watu lenye mimea mingi

## Zoezi la 2.1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni kwa usahihi maneno yaliyoandikwa katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B. Zingatieni mfano uliotolewa.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. kuwinda | A. umbo la asili la kiumbe au ardhi |
| 2. savana | B. kuonekana kuwa na umbo au sura sawa, kushabihiana |
| 3. uchumi | CH. kuwa na wajibu wa kufanya au kutekeleza jambo fulani |
| 4. pekee | D. eneo la ardhi lenye nyasi ndefu katika sehemu zenye joto |
| 5. mandhari | E. ufanyaji biashara kwa njia isiyo halali |
| 6. kukomesha | F. mapato na matumizi ya watu katika nchi pamoja na mali na fedha ambazo zinapatikana kupitia shughuli za watu |
| 7. kupaswa | G. kuzuia au kukataza jambo lisiendelee kufanyika |
| 8. magendo | H. sura ya nchi kama ardhi, milima, miti au mimea |
| 9. kufanana | I. kuandama au kuvizia mnyama msituni kwa kumsaka ili kumkamata au kumwua kwa silaha |
| 10. maumbile | J. peke yake, bila -ingine |

## Zoezi la 2.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni kwa usahihi sentensi zilizo hapo chini na picha zifuatazo.*
















1. Mlima huu ni mrefu kuliko milima mingine nchini Rwanda.
2. Mnyama huyu ana pembe ndefu.
3. Ziwa hili lina kisiwa kimoja kilicho na vibanda vingi.
4. Pundamilia na nyati huishi katika msitu huu.
5. Ziwa hili lina samaki wengi.

## 2.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jaribuni kujadiliana kuhusu sifa za vivutio vya utalii mlivyojadili katika kifungu cha habari mlichosoma hapo awali. Tajeni vivutio ambavyo mngependa kutembelea huku mkitoa sababu za chaguo lenu.*

### 2.3.1 Kuandika ufupisho/ Muhtasari

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni mambo muhimu yaliyozungumziwa katika kifungu cha habari mlichosoma. Msinakili sentensi zilizotumiwa katika kifungu hicho, jaribuni kutumia maneno yenu na kuunda sentensi zenu zilizofupishwa. Tumieni maneno yasiyozidi mia moja (100).*

Maelezo muhimu!

**Kabla ya kuandika ufupisho wenu ni vyema:**

1. Kusoma kwa makini kifungu kilichopo na kuandika mawazo muhimu. Soma mara tatu ili kuelewa vizuri.
2. Kujibu maswali haya:
   - Kifungu cha habari kinahusu nini? (Andika sentensi moja)
   - Kifungu hiki kina aya ngapi? (Tambua aya zinazojenga kifungu hiki).
   - Andikeni wazo moja kutoka kwa kila aya.
3. Kuunganisha mawazo mliyoorodhesha na kuandika habari kamili. Ili mwandike vizuri ni vyema:
   - Kutumia maneno yenu wenyewe (msitumie maneno pamoja na sentensi zilizotumiwa katika kifungu cha habari mlichokisoma)
   - Kutoa maelezo bila kupotosha ujumbe asilia.
   - Kuhakikisha kuwa mmerejelea mawazo yote muhimu yanayopatikana katika kifungu cha habari mlichokisoma.
   - Kuhakikisha kuwa hakuna makosa ya kisarufi.
   - Kuhakikisha kwamba mmezingatia urefu unaofaa.
   - Kuzingatia matumizi ya alama za uandishi.

   Habari hiyo mliyoandika kwa kuzingatia maelekezo hayo hapo juu ni ***muhtasari*** au ***ufupisho*** wa habari asilia mliyosoma. Neno 'ufupisho' linatokana na kitenzi 'fupisha' lenye maana ya '*kufanya maelezo kuwa mafupi au kupunguza urefu wake*'.

### Mfano wa ufupisho wa kifungu kuhusu mbuga za wanyama

Rwanda ni nchi iliyo na vivutio vingi vya kitalii kama vile: mito mbalimbali, mbuga za wanyama, misitu ya kiasili, hoteli nzuri, maziwa, milima mirefu pamoja na nyumba za kuhifadhia vifaa vya utamaduni wetu. Mbuga ya wanyama ya Akagera inapendwa na watu wengi. Mbuga hii ina wanyama kama vile: pundamilia, swara, paa, twiga, vifaru, tembo, simba pamoja na wanyama wengine. Pia, mbuga hii ina savana ya kupendeza. Mbuga ya wanyama ya milima mirefu ya Virunga huvutia kwa milima yake mirefu kama vile: Kalisimbi, Muhabura, Bisoke, Sabyinyo, Nyamuragira na Nyiragongo. Mbuga hii pia inajulikana kwa wanyama wanaoitwa 'sokwe watu'.

Mbuga ya msitu wa Nyungwe inafahamika kwa miti yake mirefu sana pamoja na ndege wa aina nyingi wasiopatikana kwingi ulimwenguni. Vivutio hivi vina manufaa mengi ya kiuchumi kwa Wanyarwanda. Ni lengo la kila Mnyarwanda kuhakikisha kuwa anatunza vivutio hivi ili utalii uendelee kutufaidi. ***(Maneno 140 )***

## 2.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini kuhusu mbuga za wanyama zinazopatikana nchini Rwanda na kuyaandika maelezo yenu kwa ufupi halafu mjitokeze mbele ya wanafunzi wenzenu na kuwasomea kuhusu mbuga hizo pamoja na sifa zao.*

## 2.5 Sarufi: Kiulizi '*lini*'

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili mchunguze sentensi zifuatazo katika umoja na wingi kisha mfanye zoezi linalofuata.*

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| ***Lini*** utakuja kwangu? | ***Lini*** mtakuja kwetu? |
| ***Lini*** atafanya mtihani wake? | ***Lini*** watafanya mitihani yao? |
| ***Lini*** utanilipa deni langu? | ***Lini*** mtatulipa madeni yetu? |

**Zoezi la 2.3**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili:*

1. *Jadilini aina ya neno lililopigiwa mstari katika sentensi mlizopewa.*
2. *Jadilini mabadiliko ya sentensi hizo yanayojitokeza katika umoja na wingi.*
3. *Tungeni sentensi tano sahihi kwa kutumia neno lililopigiwa mstari.*

## Zoezi la 2.4

*Katika makundi yenu ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizo wazi katika sentensi hizi kwa jibu sahihi kutoka kwenye mabano.*

1. Mtafika Gikondo ______________? (*nani, lini, nini*)
2. Nitapata zawadi uliyoniahidi ______________? (*nini, nani, lini*)
3. Atapelekwa hospitali ______________? (*nini, lini, nani*)
4. Watasafisha madarasa yetu ______________? (*lini, nini, nani*)
5. Tutaenda kuzuru nchi ya Kenya ______________? (*nani, nini, lini*)

### Maelezo muhimu!

- Neno '***lini***' ni kiulizi cha wakati. Hutumika katika sentensi kuulizia wakati wa kutendeka kwa kitendo fulani.

    ***Kwa mfano:*** Utasafisha chumba cha mgonjwa ***lini***?

    ***Jibu:*** ***Kesho jioni.***

*Jibu linalotolewa kwa sentensi iliyo na neno* **'lini'** *linaonyesha majira mbalimbali ya wakati kama vile:* ***majira ya siku*** *(asubuhi, usiku, alasiri, mchana, jioni),* ***saa, siku, wiki, mwezi***, ***mwaka*** *miongoni mwa nyakati nyingine.*

## Zoezi la 2.5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi hizi upya katika hali ya kuuliza kwa kufuata maagizo yaliyo kwenye mabano.*

**Kwa mfano:** Mgeni ataondoka kesho jioni. (Tumia: ***lini***)

**Jibu:** Mgeni ataondoka ***lini?***

1. Mtalii alizuru mbuga ya wanyama. (Tumia: ***Nani***)
2. Chakula hiki kitaliwa kesho. (Tumia: ***Nini***)
3. Watalii kutoka Marekani watafika kesho asubuhi. (Tumia: ***lini***)
4. Mwelekezaji atawapeleka watalii mjini Kigali. (Tumia: ***Nani***)
5. Kisu kitanunuliwa sokoni. (Tumia: ***Nini***)

## Zoezi la 2.6

A. Tunga sentensi tano sahihi kwa kutumia kiulizi '***lini***'.

B. Andika sentensi ulizotunga katika sehemu A katika umoja au wingi.

## SOMO LA 3: Mwelekezaji na Mtalii

### 3.1 Mazungumzo kati ya Mwelekezaji na Mtalii

*Tazameni mchoro huu katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mwelezane mnachokiona.*



*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni kifungu cha mazungumzo haya kati ya Mtalii wa kigeni na Mwelekezaji wa wageni katika mbuga ya wanyama ya Akagera kisha mjibu maswali yanayofuata.*

**Mwelekezaji:** Karibu sana katika mbuga yetu ya wanyama ya Akagera.

**Mtalii:** Asante sana.

**Mwelekezaji:** Mbuga hii iko katika mazingira mazuri ya nchi yetu. Utajionea kuwa wanyama walioko huku hufurahia kuishi huku.

**Mtalii:** *(Anatikisa kichwa)* Ndiyo! Naona kuna miti mingi na savana ya kuvutia! Bila shaka mnapokea watalii wengi sana.

**Mwelekezaji:** Ndiyo kabisa! Kila siku tunapokea watalii wengi sana. Naomba tuelekee sehemu ile ndiko kwenye wanyama wengi.

**Mtalii:** Sawa kabisa. Asante.

**Mwelekezaji:** Je, hii ndiyo mara yako ya kwanza kufika nchini mwetu?

**Mtalii:** Naam! Hii ndiyo mara yangu ya kwanza kufika nchini Rwanda. Nimefurahi sana!

| | |
|---|---|
| **Mwelekezaji:** | Karibu sana! Nini kimekufurahisha zaidi? |
| **Mtalii:** | Ooo! Kwanza, huduma nzuri niliyopata, usafi uliopo, hewa nzuri na tena zaidi mazingira haya ya mbuga zenu za wanyama. |
| **Mwelekezaji:** | Ahaa! Asante kwa hayo. Ulifika Rwanda lini? Leo? Ama! |
| **Mtalii:** | Nilifika jana. |
| **Mwelekezaji:** | Na unatarajia kurudi kwenu lini? |
| **Mtalii:** | Natarajia kurudi baada ya wiki mbili hivi. |
| **Mwelekezaji:** | Hapo ni sawa. Angalau utakuwa na muda wa kuzuru maeneo mbalimbali. Kuwa macho sasa. Tunafika katika eneo zuri ambapo wanyama wengi hupatikana. |
| **Mtalii:** | Sawasawa. Ni wanyama wa aina gani wanaopatikana hapa? |
| **Mwelekezaji:** | Hapa kuna ndovu, pundamilia, paa, simba na wengine. Angalia pale, kuna ndovu mmoja akila majani. |
| **Mtalii:** | Oooh! Ajabu! Namwaona kweli anafurahia majani hayo. |
| **Mwelekezaji:** | Angalia ndovu yuleee, aliye kando, unamwona? |
| **Mtalii:** | Ndiyo. Namwona vizuri. |
| **Mwelekezaji:** | Yule ana umri wa miaka mingi kuliko ndovu wote hapa. |
| **Mtalii:** | Oooh! Ndiyo namwona. Anaonekana mpole sana. Naweza kumpiga picha? |
| **Mwelekezaji:** | Ngoja nimwite ajitokeze vizuri. *(anapaza sauti kumwita).* |
| **Mtalii:** | *(Anapiga picha).* Naona pale, kuna sungura wawili, eeeh! Acha niwapige picha *(anataka kupiga picha lakini wanatoroka).* |
| **Mwelekezaji:** | Sungura hupenda kujificha sana. Kuna mashimo yao pale. Lazima wabembelezwe ili wasitoroke upesi. |
| **Mtalii:** | *(Anapiga picha)* Vizuri. Wanyama hawa wanakujua hivi? |
| **Mwelekezaji:** | Wao wana tabia nzuri, hawamwogopi mtu waliyemzoea. Lakini, wakiona umebeba silaha wao hurudi mara moja katika maficho yao. |
| **Mtalii:** | Kwa nini wanaogopa? |
| **Mwelekezaji:** | Kwa sababu kuna waharibifu wa mazingira wanaokuja kuwawinda na kuwaua! |
| **Mtalii:** | Ooooh! Eeeh Bwana! Angalia pale, kuna simba mkali anayeonekana! Njoo tukimbie haraka, anaweza kutuua! |
| **Mwelekezaji:** | Hapana! Usiwe na hofu! Hawezi kutufanyia lolote. |
| **Mtalii:** | Ndiyo? |
| **Mwelekezaji:** | Eeee! *(anatazama kwa saa yake)* Ni vizuri tutoke hapa tuelekee sehemu nyingine. Bado kuna mengi ya kutazama. |

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu cha mazungumzo kati ya Mwelekezaji na Mtalii, kisha mjibu maswali haya.*

1. Kwa nini wanyama hufurahia kuishi katika mazingira ya mbuga ya Akagera?
2. Taja vitu vilivyomfurahisha mgeni wa kitalii.
3. Mgeni huyu alifika lini nchini Rwanda?
4. Mgeni huyu wa kitalii atarudi nchini kwao lini?
5. Ni wanyama gani wanaopatikana katika mbuga ya wanyama ya Akagera?
6. Ndovu mwenye umri mrefu kuliko wengine ana sifa gani?
7. Sungura hupenda nini?
8. Ili sungura wasitoroke mwelekezaji alifanya nini?
9. Ni wakati gani wanyama hujificha?
10. Waharibifu wa mazingira hufanya nini?

## 3.2 Msamiati kuhusu ziara ya kitalii

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha mazungumzo mlichosoma hapo juu na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 3.1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni kwa usahihi msamiati katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B. Zingatieni mfano uliopo.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. hewa | A. kuweza kutenda jambo |
| 2. bila shaka | B. mahali palipo na miti mingi midogo midogo iliyoshikamana pamoja na nyasi au miba |
| 3. kuwa macho | CH. kutazama bila kufumba macho |
| 4. kuwahi | D. upepo laini ambao watu huuvuta ili waweze kuishi |
| 5. mharibifu | E. bila wasiwasi, kwa hakika |
| 6. vichaka | F. kutopata usingizi |
| 7. kukazia macho | G. kuambia mtu maneno mazuri ili akupatie unachotaka au afanye unavyotaka |
| 8. kubembeleza | H. mtu anayeharibu vitu |

## Zoezi la 3.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni kwa usahihi michoro na picha hizi na sentensi zinazofuata.*















1. Watalii wanawatazama wanyama katika mbuga ya Akagera.
2. Mtoto wa simba anaitwa shibli.
3. Msitu wa Virunga una miti mingi na sokwe wengi.
4. Walinzi wa mbuga za wanyama wamewashika wasasi waliokuwa wakiwinda ndovu kwa ajili ya pembe zao.
5. Wanafunzi walienda kuzuru mbuga ya *Wanyama*.


## 3.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini kuhusu wanyamapori ambao mmewahi kuwaona kwa kuelezana:*

1. Majina ya wanyamapori hao.
2. Sifa za wanyamapori hao.
3. Chakula cha wanyamapori hao.
4. Maumbile ya wanyamapori hao.
5. Uliwaona wanyama hao wapi?
6. Wanyamapori hao wanapenda kuishi katika mazingira ya aina gani?

### Zoezi la 3.3

A. *Chunguza picha za wanyama hawa na kuzihusisha na majina yao sahihi.*

| **1. Ndovu** | **2. Kiboko** | **3. Mamba** |
|---|---|---|
|  |  |  |
| **4. Sungura** | **5. Pundamilia** | **6. Kondoo** |
|  |  |  |

| 7. Simba | 8. Mbuzi | 9. Ng'ombe |
|---|---|---|
|  |  |  |

B. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, onyesheni wanyama ambao hufugwa na wanyamapori (wanyama wasiofugwa) kati ya wanyama walio hapo juu.*

## 3.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, igizeni mazungumzo mliyosoma kati ya Mwelekezaji na Mtalii wa kigeni.*

## 3.5 Sarufi

### Viulizi '*wapi*' na '*vipi*'

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mjibu maswali haya.*

**Sentensi 1:** Kila siku tunapokea watalii wengi kutoka ***Marekani.***

**Swali:** Kila siku tunapokea watalii wengi kutoka ***wapi?***

**Sentensi 2:** Mgeni alihudumiwa ***vizuri***.

**Swali:** Mgeni alihudumiwa ***vipi?***

**Sentensi 3:** Mgeni alifurahishwa na huduma ya ***hoteli***.

**Swali:** Mgeni alifurahishwa na huduma ya ***wapi?***

**Sentensi 4:** Ndovu alionekana ***mpole***.

**Swali:** Ndovu alionekana ***vipi?***

*Je, mmegundua nini?*

**Zoezi la 3.4**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi tano kama hizo zilizoandikwa hapo juu. Kutokana na sentensi utakazotunga, tunga maswali yake kwa kutumia neno '**wapi**'.*

### Maelezo muhimu!

- Maneno ***wapi*** na ***vipi*** ni viulizi.
- Kiulizi ***wapi*** kinatumiwa kuulizia swali kuhusu ***mahali***.
- Kiulizi ***vipi*** kinatumiwa kuulizia swali kuhusu ***namna***.

**Kwa mfano:**

**Sentensi:** Watalii wawili walizuru ***eneo la utalii la Akagera***.
**Swali:** Watalii wawili walizuru ***wapi?***
**Sentensi:** Viongozi wetu walifika ***salama***.
**Swali:** Viongozi wetu walifika ***vipi?***

## Zoezi la 3.5

*Tunga maswali kuhusu maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hizi kwa kutumia viulizi sahihi.*

**Kwa mfano:**

1. Mwanafunzi huyu anasomea ***Uchina***.

**Jibu:** Mwanafunzi huyu anasomea ***wapi?***

2. Mwanafunzi huyu anaandika ***vizuri***.

**Jibu:** Mwanafunzi huyu anaandika ***vipi?***

1. Dereva huyu anatoka Afrika Kusini.
2. Sembare anaingia chumbani mwake haraka.
3. Gari la mtalii limesimama nje ya nyumba yetu.
4. Simba anajificha vichakani.
5. Ndugu yangu anatembea polepole.

## Zoezi la 3.6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi tano katika umoja na wingi kwa kutumia viulizi '**wapi**' na '**vipi**'.*

**Zoezi la 3.7**

*Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia jibu sahihi kutoka kwa yaliyo kwenye mabano.*

1. Kijana mmoja alienda __________ ? *(nani, nini, wapi)*
2. Waziri ataondoka __________ ? *(nani, vipi, nini)*
3. Mtumishi amepoteza ufagio wake __________? *(lini, nani, wapi)*
4. Fundi hodari amejenga nyumba __________? (*nani, vipi, nini*)
5. Mwalimu wetu ameenda __________? (*nani, nini, wapi*)

### 3.5.1 Kiulizi '*kwa nini*'

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo.*

**Sentensi 1:** Mtalii atatembelea mbuga ya wanyama ili kuwaona wanyamapori.

**Swali:** ***Kwa nini*** mtalii atatembelea mbuga ya wanyama?

**Sentensi 2:** Mgeni alifurahi kwa sababu alipewa huduma nzuri.

**Swali:** ***Kwa nini*** mgeni alifurahi?

**Zoezi la 3.8**

1. *Katika makundi ya wanafunzi wawili, tungeni sentensi mbili mbili kama hizo zilizoandikwa hapo juu. (Sentensi 1 na 2)*
2. *Tunga maswali kwa sentensi mlizotunga katika swali la 1 hapo juu. (Hakikisha kuwa mmetumia* ***kwa nini*** *katika maswali yenu).*

**Maelezo muhimu!**

- Maneno ***'kwa nini'*** yanatumiwa kuulizia ***sababu ya kufanyika kwa jambo fulani.***

  **Kwa mfano:**

- **Sentensi 1:** Mwanafunzi huyu alipewa zawadi kwa sababu anathamini mazingira yake.
- **Swali:** ***Kwa nini*** mwanafunzi huyu alipewa zawadi?

  *(Maneno* ***'kwa nini'*** *yametumiwa kuulizia sababu ya kupewa zawadi kwa mwanafunzi huyu).*

- **Sentensi 2:** Waelekezaji walipewa mafundisho ili wajue namna ya kuwapokea wageni.
- **Swali:** ***Kwa nini*** waelekezaji walipewa mafundisho?

*(Maneno **'kwa nini'** yametumiwa kuulizia sababu ya waelekezaji kupewa mafundisho). Maneno ya kuulizia maswali huitwa **viulizi**.*

## Zoezi la 3.9

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, ulizeni maswali kuhusu maneno na vifungu vya maneno vilivyopigiwa mstari katika sentensi hizi.*

**Kwa mfano:** Mtalii huyu hupenda kuja Rwanda ***kwa sababu Rwanda ni nchi nzuri.***

**Jibu:** ***Kwa nini*** mtalii huyu hupenda kuja Rwanda?

1. Mtoto huyu analia kwa sababu anataka chakula.
2. Mkulima huyu alichinja mbuzi mmoja kwa sababu ana wageni.
3. Mukandori anakaa katika nyumba hii kwa sababu alihamishwa kikazi.
4. Mtu huyu amepelekwa jela kwa sababu alihukumiwa kifungo cha miaka miwili.
5. Mama na baba wamekaa sebuleni kwa sababu wanazungumza na wageni wetu.

## SOMO LA 4: Utamaduni na utalii

### 4.1 Kifungu kuhusu utamaduni na utalii

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni picha hizi kisha mjadili kuhusu mnachokiona na kuwaelezea wenzenu.*






*Soma kifungu cha habari kinachofuata kuhusu utamaduni na utalii kisha mjibu maswali yanayofuata. Kifungu hiki kinaeleza jinsi utamaduni unavyoweza kutumiwa katika utalii na kuleta manufaa kwa nchi.*

Baadhi ya watu wanafikiri kwamba kuhifadhi utamaduni ni ishara ya kurudi nyuma na kutochangamkia maendeleo. Watu hawa wanalinganisha utamaduni na mambo yasiyo ya kisasa; mambo ya zamani; yaani mambo ya watu wasio na elimu. Utamaduni ni mazoea yetu, mila zetu na maisha yetu kwa jumla. Utamaduni unaingiliana na shughuli zetu za kila siku na unatusaidia kujitambulisha kama Wanyarwanda wenye thamani.

Ili kudumisha mambo yetu ya kitamaduni na kuyathamini, nyumba mbalimbali za kuhifadhi vifaa na shughuli zote za kitamaduni zilijengwa. Nyumba nyingine zinaendelea kujengwa nchini kote na zina umuhimu mkubwa wa kuhifadhi vifaa vilivyotumiwa kudumisha utamaduni wetu.

Watu wengi, watalii wa ndani ya nchi na wa kigeni huzitembelea na kujionea mambo hayo ya utamaduni wetu.

Uendapo wilayani Huye, utafika katika nyumba kubwa yenye vifaa na mambo mengine mengi kuhusu utamaduni wa Wanyarwanda. Utaweza kuona kwa mfano aina mbalimbali za mavazi yaliyotumiwa na mababu zetu, ngoma zetu za kitamaduni, viti vya Kinyarwanda, majamvi mazuri, picha za wanawake waliovaa taji za kitamaduni, mitindo ya kitamaduni ya kukata nywele, nyumba ya zamani iliyotumiwa na mababu zetu na sehemu zake mbalimbali, vifaa vilivyotumiwa katika nyimbo na sherehe za kitamaduni, vifaa vya zamani vilivyotumiwa nyumbani na kadhalika.

Nyumba ya utambulisho wa utamaduni wa Rwanda iliyopo wilayani Nyanza '*Rukari*' hutembelewa na watu wengi. Nyumba hii ilikuwa makazi ya mfalme Mutara III Rudahigwa na imegawanywa katika vyumba tofauti vilivyotumiwa kwa shughuli mahususi. Kwa mfano, unaweza kupata chumba kilichotumiwa kutunza na kutengeneza maziwa ya mfalme, chumba kilichotumiwa kufanya vitu viwe baridi, sebule tatu zilizotumiwa kupokelea wageni na kadhalika. Pembeni mwa uga wa nyumba hii, mtu huweza kutazama ng'ombe wa kitamaduni '*Inyambo*' ambao hupendwa na watu wengi. Ng'ombe hawa husifiwa sana kwa umbo lao la kuvutia na pembe zao nzuri na ndefu ajabu. Mbali na vifaa vya zamani vinavyopatikana katika nyumba za kuvihifadhi na majengo mbalimbali ya kitamaduni, wageni wengi hufurahia pia nyimbo zetu za kitamaduni pamoja na mitindo mbalimbali ya kuzicheza.

Kwa kweli, utamaduni wetu ni sehemu muhimu ya utalii na unaipatia nchi yetu pesa nyingi za kigeni. Watalii wengi huja kutembelea nchi yetu kwa ajili ya kufurahia mambo mengi ya utamaduni wetu. Pesa zinazotokana na utalii katika sekta ya utamaduni huchangia sana katika miradi mbalimbali ya maendeleo ya taifa letu.

## Maswali ya ufahamu

I. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena kifungu cha ufahamu kilichotangulia kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Kwa nini watu wengi hawaelewi umuhimu wa utamaduni?
2. Utamaduni unahusu nini?
3. Ni mambo gani yanayofanywa ili kuhifadhi utamaduni wetu?
4. Taja maeneo ambapo tunaweza kupata nyumba za kuhifadhia utamaduni wetu?

5. Taja vitu tunavyoweza kupata katika nyumba ya kuhifadhi utamaduni wetu iliyoko wilayani Huye.
6. Nyumba iliyoko wilayani Nyanza ilikuwa makazi ya nani?
7. Ni vitu gani vya kuvutia ambavyo tunaweza kukuta katika nyumba hiyo?
8. Kwa nini tunafaa kujivunia utamaduni wetu?

II. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni kwa ufupi kifungu cha habari mlichosoma hapo juu. Tumieni maneno sabini (70).*

## 4.2 Msamiati kuhusu utamaduni

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha habari mlichosoma kilichotangulia na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale panapohitajika.*

### Zoezi la 4.1


*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni maneno yaliyoandikwa katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B. Zingatieni mfano uliopo.*

| Sehemu A | Sehemu B |
| --- | --- |
| 1. hawatambui | A. mafunzo |
| 2. mambo ya kisasa | B. kuleta mafanikio au faida |
| 3. kuthamini | CH. mambo yanayohusiana na utamaduni wa watu |
| 4. elimu | D. hawaelewi |
| 5. mila | E. mambo yasiyo ya zamani |
| 6. kuzaa matunda | F. kuheshimu |
| 7. kujivunia | G. wazazi wetu walioishi zamani |
| 8. kudumisha | H. kumwambia mtu jina lako, kujielezea |
| 9. mababu zetu | I. kufurahia |
| 10. kujitambulisha | J. kufanya kitu kiendelee kutumika kwa muda mrefu, kukifanya kiishi maisha marefu |

## Zoezi la 4.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni mchoro na picha hizi na sentensi zifuatazo kwa usahihi.*

A



B



CH



D



E



1. Wageni hupokelewa katika sebule hii nzuri kwa mazungumzo.
2. Mama yangu huvaa taji la kitamaduni katika sherehe za harusi.
3. Babu anawasimulia wajukuu wake hadithi ya kusisimua.
4. Huu ni mtindo tofauti wa kukata nywele unaoitwa '*Amasunzu*'.
5. Haya ni makazi yetu. Tuna nyumba nzuri ya kisasa.

## 4.3 Matumizi ya lugha: Zoezi la msamiati

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni herufi zilizoachwa wazi katika visanduku vifuatavyo ili kuunda neno kamili.*

**Kwa mfano:**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | A | | A | D | | N | |

**Jibu:**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | T | A | M | A | D | U | N | I |

1.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| V | | F | | A |

2.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | E | L | | K | E | | A | J | |

3.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | H | | M | | N | I |

4.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| M | | Y | | M | |

5.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| M | | V | | Z | |

## 4.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu utamaduni na utalii halafu mjitokezee mbele ya wanafunzi wenzenu kuwaeleza kuhusu yale mliyoafikiana. Jaribuni kuhakikisha kwamba mmejibu maswali haya katika majadiliano yenu:*

1. Utamaduni unahusu nini?
2. Utamaduni wa Wanyarwanda unatambulishwa na nini?
3. Utamaduni unaweza kuvutia watalii?

4. Ni faida gani tunaweza kupata kutokana na utamaduni?
5. Tunaweza kufanya nini ili kuhifadhi utamaduni wetu?
6. Ni hasara gani tunaweza kupata iwapo hatutathamini utamaduni wetu?

## 4.5 Sarufi: Wakati wa mazoea, tungo yakinishi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi zinazofuata katika umoja na wingi kisha mfanye zoezi lililo hapo chini.*

| Umoja/ Tungo yakinishi | Wingi/ Tungo yakinishi |
|---|---|
| ***Mimi hu***enda kutazama wanyama ***kila mwaka***. | ***Sisi hu***enda kutazama wanyama ***kila mwaka***. |
| ***Wewe hu***chota maji ***kila asubuhi***. | ***Nyinyi hu***chota maji ***kila asubuhi***. |
| **Yeye hu**cheza mpira ***kila jioni***. | ***Wao hu***cheza mpira ***kila jioni***. |

### Zoezi la 4.3

1. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi moja moja kwa kutumia neno* ***kila siku*** *na kitenzi* ***pika*** *katika nafsi zifuatazo:* ***mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi*** *na* ***wao***.
2. *Linganisheni sentensi zenu na zile ulizotolewa hapo juu kuhusu kitenzi* ***enda, chota*** *na* ***cheza***.

### Maelezo muhimu!

- Sehemu za kitenzi ***enda, chota*** na ***cheza*** zinaandikwa baada ya kutumia ***hu***.
- ***'hu'*** inarudiwarudiwa katika vitenzi vyote baada ya nafsi ***mimi, wewe, yeye sisi, nyinyi*** na ***wao.***
- '***hu***' inatumiwa kuonyesha kitendo kinachofanywa mara kwa mara, kila wakati.

  **Kwa mfano:** *Mimi huchota maji kila asubuhi.* (Kitendo cha kuchota maji kinafanywa kila asubuhi)

  - Kitenzi ***chota*** kimetumiwa katika ***wakati wa mazoea*** ili kuonyesha kuwa kitendo hicho kinafanywa kila asubuhi.

## Zoezi la 4.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi zifuatazo kwa kutumia wakati wa mazoea.*

**Kwa mfano:** Wachezaji hawa wanapenda kucheza kila jioni.

**Jibu:** Wachezaji hawa **hupenda** kucheza kila jioni.

1. Wagonjwa hawa wanapelekwa hospitalini kwa magari haya.
2. Waimbaji hawa wanapata fedha nyingi kila wiki.
3. Wageni wetu watafika kwenye uwanja wa ndege kabla ya saa kumi.
4. Mimi nitatembea kwa miguu hadi kanisani.
5. Mwalimu wetu ataondoka saa kumi na moja.

## Zoezi la 4.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni majibu ya sentensi za Zoezi la 4.4 (lililo hapo juu) katika umoja au wingi.*

**Kwa mfano**: Wachezaji hawa hupenda kucheza kila jioni.

**Jibu:** Mchezaji huyu hupenda kucheza kila jioni.

## SOMO LA 5: Milima yetu

### 5.1 Kifungu kuhusu 'Milima yetu'

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni picha zifuatazo kisha mjadili kuhusu kile kinachoendelea au mnachokiona katika picha hizi kwa kujitokeza mbele ya wanafunzi wenzenu na kuwaelezea.*





*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni kifungu cha habari kinachofuata kuhusu '**Milima yetu**' kisha mjibu maswali yanayofuata. Kifungu hiki kinaelezea milima mbalimbali inayopatikana nchini Rwanda na mazingira yake mazuri yanayovutia sana.*

Rwanda inasifiwa kwa milima yake mikubwa na midogo. Watu wengi huiita *nchi ya milima elfu moja*. Milima hii ina misitu mingi mikubwa na midogo. Misitu hii hutuletea hewa safi. Miongoni mwa misitu hii mikubwa ni kama vile: msitu wa Nyungwe, msitu wa Gishwati na msitu wa Mukura. Misitu hii huvutia na huhifadhi wanyama wadogo kama vile: sungura mwitu, kima, mbwa mwitu na wengine. Wanyama kama kima huwa hawaogopi watu kutokana na tabia zao zinazofanana na tabia za binadamu.
Msitu wa Nyungwe huhifadhi ndege wa aina nyingi. Kila mwaka mbuga ya wanyama iliyotengwa katika msitu huu hupokea watalii wengi kutoka nchi mbalimbali. Misitu ya Rwanda husababisha mvua inayostawisha mimea kiasi kwamba bila misitu hiyo, nchi nzima inaweza kukumbwa na ukame.

Milima ya Rwanda ni mingi mno na ni ya aina nyingi. Kuna milima mirefu inayojulikana kwa volkano kama vile: Muhabura, Kalisimbi, Sabyinyo, Nyiragongo, Gahinga na kadhalika. Aina ya milima hii inapatikana katika sehemu za Kaskazini mwa Rwanda kuanzia mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na huendelea hadi kwenye mpaka wa Rwanda na Uganda. Milima mingine inapatikana kote nchini na kila wilaya ina milima yake inayovutia sana. Wilayani Muhanga, kwa mfano, kuna milima Ndiza, Kanyarira na mingine. Wilayani Huye kuna Ibisi bya Huye. Wilayani Nyanza kuna Gacu, Rwabicuma na Mpanga inayopendwa na watu wengi kwa mandhari yake ya kuvutia. Wilayani Ngororero kuna mlima Kageyo ambapo kuna mahali panapojulikana kama '*Mu Miko y'Abakobwa'*. Kutoka Muhanga kwenda Karongi mtu hupita kwenye mwamba mrefu wenye mteremko wa maji. Mwamba huu unajulikana kwa jina la '*Mwamba wa Ndaba'* na huvutia watalii wengi wakiwemo Wanyarwanda wenyewe. Mjini Kigali watu hupenda kufurahia mazingira ya mji huu kwa kusimama juu ya Mlima Kigali. Mlima huu unasifiwa kuwa ndio kilele cha Kigali na kuwa palikuwa makazi ya Mfalme Cyirima Rujugiro. Hapa, mtu huweza kutazama mji mzima, asili ya Rwanda 'Gasabo' na sehemu mbalimbali za mjini, mto Nyabarongo na hata sehemu za Bugesera.

Licha ya kuvutia, faida za mazingira safi ya Rwanda ni nyingi. Serikali yetu huomba Wanyarwanda wote kutunza vizuri mazingira yetu na kupambana na waharibifu wa mazingira hayo. Viongozi wetu hupenda kusema. "Msikate miti ovyoovyo na msiharibu mazingira kwa kuchoma milima na misitu. Tupande miti mingi na tujiepushe na kuchafua mazingira yetu".

## Maswali ya ufahamu

I. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena kifungu cha habari kilichotangulia, kisha mjibu maswali haya.*

1. Kwa nini watu wengi huita Rwanda ‘nchi yenye milima elfu moja’?
2. Ni faida gani tunazopata kutokana na misitu yetu?
3. Taja misitu mikubwa iliyozungumziwa katika kifungu hiki cha habari.
4. Taja milima minne mirefu iliyozungumziwa katika habari hii.
5. Milima hiyo hupatikana katika sehemu gani ya nchi yetu?
6. Taja wilaya mbili na mlima mmoja mmoja unaopatikana katika kila wilaya.
7. Ni kwa nini Mlima Kageyo unajulikana?
8. Mwamba wa Ndaba una sifa gani?
9. Serikali ya Rwanda huomba Wanyarwanda kufanya nini?
10. Ni funzo gani tunalopata kutoka kwa viongozi wetu?

II. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni habari hii kwa ufupi. Tumieni idadi ya maneno mia moja.*

## 5.2 Msamiati kuhusu ‘Milima yetu’

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha habari kilicho hapo juu na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale panapohitajika.*


### Zoezi la 5.1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi zenu kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.*

1. *Miongoni mwa* ***viumbe*** wote, binadamu ndiye mwenye akili.
2. Mjini ***Kigali*** kuna magari mengi mno.
3. Hapa kuna ***mteremko*** mrefu, jihadhari usianguke.
4. Watu wengi wananunua rangi hii kwa sababu ***inavutia*** sana.
5. Mvua haijanyesha kwa muda mrefu; kuna ***ukame*** na wanyama wetu wamekosa maji na chakula.
6. Mtu huyu alishikwa na polisi kwa sababu anaharibu mazingira kwa ***kuchoma*** misitu.
7. Huwezi kulima hapa kwa sababu kuna ***mwamba*** mkubwa.
8. Ni lazima kila mwananchi afanye kazi ili ***kupambana*** na umaskini.

## Zoezi la 5.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni mchoro na picha pamoja na sentensi ulizopewa hapo chini kwa usahihi.*














1. Mlima huu ni mrefu sana kuliko milima mingine.
2. Watu hawa wanapanda miti.
3. Msitu huu una ndovu wengi.
4. Mteremko wa maji katika eneo hili unavutia sana.

## 5.3 Matumizi ya lugha: Zoezi la jedwali

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizoachwa wazi kwa kuzingatia maelezo yaliyo chini ya jedwali.*



## Kwenda kulia

1. Mtu anayetembelea mahali pa kuvutia kwa kujifurahisha
4. Aina ya silaha inayotumiwa kukata mti
5. Muda wa saa ishirini na nne
8. Kujinyosha kitandani ili kupata usingizi
10. Ndege jike anayefugwa
12. Kupata kiumbe kichanga baada ya kukomaa kwa mimba
14. Mimea mikubwa iliyopandwa shambani au kuota mwituni
15. Sarafu ya Marekani

## Kwenda chini

1. Mtu anayefanya kazi ya kulinda
2. Azuru mbuga za wanyama
3. Sehemu yenye pori, vichaka na nyasi au mwitu
6. Kuangalia upande kilipo kitu fulani au kuenda mahali fulani
7. Sehemu ya ardhi inayoinuka juu sana
9. Safari ya kuzuru mahali kwa sababu maalumu

11. Ukosefu wa maji
13. Mnyama wa porini anayefanana na mbuzi

## 5.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu faida za utalii kwa wananchi halafu mjitokeze mbele ya darasa ili muwaeleze wanafunzi wenzenu kuhusu hoja mlizozipata. Katika majadiliano yenu, hakikisheni mmejibu maswali haya:*

1. Utalii ni nini?
2. Ni sehemu zipi za utalii zilizo nchini mwetu?
3. Ni watu gani wanaokuja kutalii nchini mwetu?
4. Nchi yetu ina faida gani kwa kupokea watalii wengi?
5. Wananchi wanapata faida gani kutokana na utalii?

## 5.5 Sarufi: Wakati wa mazoea, tungo kanushi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi zinazofuata katika umoja na wingi kisha mfanye zoezi lililo hapo chini.*

| | **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|---|
| Umoja | ***Mimi hu***panda miti mingi kila mwaka. | ***Mimi si***pandi miti mingi kila mwaka. |
| | ***Wewe hu***panda miti mingi kila mwaka. | ***Wewe hu***pandi miti mingi kila mwaka. |
| | ***Yeye hu***panda miti mingi kila mwaka. | ***Yeye ha***pandi miti mingi kila mwaka. |
| Wingi | ***Sisi hu***panda miti mingi kila mwaka. | ***Sisi hatu***pandi miti mingi kila mwaka. |
| | ***Nyinyi hu***panda miti mingi kila mwaka. | ***Nyinyi ham***pandi miti mingi kila mwaka. |
| | ***Wao hu***panda miti mingi kila mwaka. | ***Wao hawa***pandi miti mingi kila mwaka. |

**Zoezi la 5.3**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi moja moja kwa kutumia wakati wa mazoea (tungo yakinishi na tungo kanushi). Tumia nafsi zifuatazo:* ***mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi*** *na* ***wao.***

## Maelezo muhimu!

***Kiambishi 'hu'*** kinarudiwarudiwa katika nafsi zote za tungo yakinishi. Kikanushi ***'ha'*** hutumiwa katika vitenzi vinavyoisha kwa irabu ***'i'*** badala ya irabu ***'a'*** katika tungo kanushi.

**Kwa mfano:** Sisi **hu**pand**a** miti. (tungo yakinishi)

Sisi **ha***tu*pand**i** miti. (tungo kanushi)

Viambishi vya nafsi hutumiwa baada ya kikanushi ***'ha'*** na hubadilika kulingana na nafsi au ngeli inayohusika.

**Kwa mfano:**

| | **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|---|
| Umoja | Wewe hupanda mti. | Wewe hupandi mti. |
| | Yeye hupanda mti. | Yeye hapandi mti. |
| | Chombo hiki hubeba watu wengi. | Chombo hiki hakibebi watu wengi. |
| | Nyumba hii hutembelewa na watalii wengi. | Nyumba hii haitembelewi na watalii wengi. |
| Wingi | Nyinyi hupanda miti. | Nyinyi ha***m***pandi miti. |
| | Wao hupanda miti. | Wao ha***wa***pandi miti. |
| | Vyombo hivi hubeba watu wengi. | Vyombo hivi ha***vi***bebi watu wengi. |
| | Nyumba hizi hutembelewa na watalii wengi. | Nyumba hizi ha***zi***tembelewi na watalii wengi. |

## Zoezi la 5.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni vitenzi vilivyo kwenye mabano kwa kutumia wakati wa mazoea, tungo yakinishi.*

**Kwa mfano:** Mtoto huyu ______ (kuchelewa) kufika shuleni kila asubuhi.

**Jibu:** Mtoto huyu **huchelewa** kufika shuleni kila asubuhi.

1. Wewe ________________ (kuandika) barua ndefu.
2. Sisi ________________ (kusaidia) walemavu katika kijiji hiki.
3. Watalii hawa ______________ (kufurahia) mazingira ya milima mirefu.
4. Mkulima huyu ______________ (kupanda) miti katika mashamba yake.
5. Mti huu ________________ (kuzaa) matunda mengi kila mwaka.

## Zoezi la 5.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi za zoezi la 5.4 lililotangulia katika tungo kanushi.*

**Kwa mfano:**

**Sentensi:** Mtoto huyu ***huchelewa*** kufika shuleni kila asubuhi.

**Jibu:** Mtoto huyu ***hachelewi*** kufika shuleni kila asubuhi.

## Zoezi la 5.6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kanusheni tungo hizi kwa kuziandika katika umoja na wingi.*

**Kwa mfano:** Kitabu changu ***hupendwa*** na watu wengi.

**Jibu:** **Umoja:** Kitabu changu ***hakipendwi*** na watu wengi.

**Wingi:** Vitabu vyetu ***havipendwi*** na watu wengi.

1. Mwanafunzi yule hujibu vizuri maswali ya mwalimu.
2. Mtalii hutembelea mbuga zetu za wanyama kila siku.
3. Ukucha huu hupakwa rangi nyeupe baada ya mwezi mmoja.
4. Ndege yule hulala kwenye mti huu.
5. Kitanda chako hutumiwa na wageni wetu.

## SOMO LA 6: Maji yetu

### 6.1 Kifungu kuhusu 'Maji yetu'

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni picha na michoro hii kisha mjadili kuhusu kile kinachoendelea kwa kujitokeza mbele ya wanafunzi wenzenu ili kuwaelezea.*










*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni kifungu cha habari kinachofuata ambacho kinahusu '**Maji yetu**' kisha mjibu maswali yanayofuata.*

Maji ni muhimu katika maisha ya binadamu. Maji hutumiwa kupikia chakula, kunawa na kuosha miili yetu na hata kusafisha vyombo tunavyotumia nyumbani. Kazi nyingi haziwezi kutimizwa bila ya maji. Ujenzi wa barabara, nyumba zetu za kuishi na hoteli hauwezi kufanywa iwapo maji yatakosekana.

Ukulima, ufugaji na utunzaji wa mbuga zetu za wanyama hauwezi kutekelezwa na kuleta faida yoyote bila ya maji. Wanyama wote huhitaji maji ya kunywa na mimea huhitaji maji ili iweze kuota na kustawi vizuri.

Bila maji, nguo zetu haziwezi kufuliwa na nyumba zetu haziwezi kusafishwa. Ukosefu wa maji ni chanzo cha uchafu ambao huleta magonjwa ya aina mbalimbali. Kutokana na umuhimu huo mkubwa wa maji, watu wengi husema 'Maji ni uhai'.

Nchini Rwanda, kuna mito mbalimbali na maziwa mengi. Vilevile, mvua hunyesha kwa kipimo kizuri na nchi yetu inahesabiwa miongoni mwa nchi zenye hewa nzuri na safi. Baadhi ya mito inayopatikana nchini Rwanda ni kama vile: *Nyabarongo, Akanyaru, Akagera, Mukungwa, Rusizi, Rukarara* na kadhalika. Mito hii ina faida kubwa kwa nchi nzima. Mbinu za kiteknolojia zinatumiwa kutengeneza vituo vinavyotuletea nguvu za umeme kwa kutumia mito yetu. Watu mbalimbali wakiwemo watalii wa kigeni hupenda kuzuru vituo hivyo na kufurahia mazingira yake. Miongoni mwa vituo hivyo kuna kituo cha Nyabarongo, kituo cha Ntaruka na kituo cha Rusizi. Vituo hivyo vinachangia katika kuleta nguvu za umeme na majengo yake yanavutia sana.

Nchi ya Rwanda inahesabiwa miongoni mwa nchi za ukanda wa maziwa makuu. Nchi nyingine zinazopatikana katika ukanda huu ni kama vile: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Uganda. Maziwa yanayopatikana nchini Rwanda ni kama vile: *Ziwa Kivu* kwenye sehemu za Magharibi mwa nchi katika wilaya za Rubavu, Rutsiro, Karongi, Nyamasheke na Rusizi, *Ziwa la Cyohoha I* na *Ziwa la Cyohoha II*, *Ziwa Rweru* wilayani Bugesera, *Ziwa Burera* na *Ziwa Ruhondo* katika sehemu za Kaskazini wilayani Burera, *Ziwa Muhazi* kuanzia sehemu za Gasabo, Rwamagana, Kayonza, Gatsibo na Gicumbi, *Ziwa Mugesera* katika sehemu za wilayani Rwamagana, Bugesera na Ngoma. Visiwa vingi hupatikana katika maziwa haya na watu wengi hupenda kuvitazama. Maziwa haya yana sehemu zinazopendeza kwenye ufuko wake na watu hupenda kukaa kwenye mchanga wake na kutazama maji yake safi.

Watalii wengi huzuru mazingira ya maziwa yetu. Wao hufurahia kutazama na kusafiri katika vyombo vinavyopatikana hapo. Vyombo hivi hutumiwa kuwazungusha watalii katika mandhari ya maziwa hayo na huwafikisha kwenye visiwa vingi vinavyopatikana hapo. Vyombo vingine hutumiwa kubeba mizigo ya watu kutoka eneo moja hadi eneo jingine.Watalii wengi hupenda sana samaki watamu wanaopatikana katika maji hayo. Ni nadra mtu kutembelea sehemu hizo bila kutarajia kula samaki. Ziwani Kivu, teknolojia hutumiwa kutengeneza gesi inayohitajika kuongeza kiwango cha umeme nchini Rwanda. Watalii wengi hufika pale ili kutazama hali hii na hivyo hoteli nyingi zinazozunguka eneo hilo hufaidika kifedha.

Kwa kweli, maji yana umuhimu mkubwa; si kwa afya yetu tu; bali huvutia macho ya watalii wengi, huwafurahisha na huwaletea burudani isiyo na kipimo kiasi cha kuzalisha mali nyingi katika sekta ya utalii.

## Maswali ya ufahamu

I. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni tena kifungu cha habari kilichotangulia kisha mjibu maswali haya.*

1. Maji yana umuhimu gani kwa afya yetu?
2. Maji huweza kutumiwa katika shughuli gani?
3. Ni mambo gani yanayoweza kutokea iwapo tutakosa maji?
4. Kwa nini nchi ya Rwanda ina maji ya kutosha?
5. Taja maziwa matatu yapatikanayo nchini Rwanda na ueleze sehemu yanakopatikana.
6. Taja mito iliyozungumziwa katika kifungu hiki.
7. Ni vituo gani vilivyojengwa ili kutuletea nguvu za umeme?
8. Rwanda inahesabiwa katika ukanda upi?
9. Ukanda huo unazihusisha nchi gani?
10. Taja mambo mawili ambayo watalii huyafurahia.

II. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, fupisheni kifungu cha habari mlichosoma hapo awali. Tumieni idadi ya maneno mia moja pekee.*

## 6.2 Msamiati kuhusu 'Maji yetu'

### Zoezi la 6.1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.*

1. Mwalimu wetu ***anatimiza*** kazi yake kwa kutufundisha vizuri.
2. Mimi ***hufua*** nguo zangu kila Jumamosi kwa kutumia maji safi na sabuni.
3. ***Ukosefu*** wa mboga katika chakula unaweza kusababisha magonjwa mengi katika mwili wa binadamu.
4. Rwanda inataka kuongeza vituo vya kutengeneza ***nguvu za umeme*** kwa kutumia mito yake.
5. Rwanda hupata ***gesi*** nyingi kutoka Ziwa Kivu.

### Zoezi la 6.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chagueni neno linalofaa kati ya maneno yafuatayo kisha mjaze nafasi zilizo wazi katika sentensi hizi.*

***Mtalii, Mto, Mbuga ya wanyama, ziwa, mbinu, Kisiwa***

**Kwa mfano:** Mwalimu anatumia ________ nzuri kufundisha somo la Kiswahili.

**Jibu:** Mwalimu anatumia ***mbinu*** nzuri kufundisha somo la Kiswahili.

1. ________ cha Ijwi kinapatikana ziwani Kivu.
2. ________ huyu alilipa pesa nyingi ili aweze kuingia katika nyumba hii ya kitalii.
3. ____________ ya Akagera inatembelewa na wageni wengi kutoka nchi mbalimbali.
4. Walimu wetu wanatarajia kwenda Karongi ili kufurahia mazingira ya _______ la Muhazi.
5. Watalii wawili walienda kwa gari zuri kutazama ________ Mukungwa.

## 6.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

### Zoezi la 6.3

*Je, umewahi kutembelea ziwa lolote nchini Rwanda? Umewahi kufika kwenye kisiwa chochote nchini Rwanda? Jadilini kuhusu ziara zenu katika makundi ya wanafunzi wanne wanne huku mkielezeana:*

(a) Mliwaona wanyama gani wa majini?
(b) Mliona mito gani?
(ch) Mlipanda vyombo vipi vya majini?
(d) Mlivua samaki?

### Zoezi la 6.4

*Mkiwa wawili wawili, husisheni kwa usahihi maneno yaliyoandikwa katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. kisiwa | A. namna ya kufanya jambo |
| 2. kuogelea | B. kutoa fedha au mali kwa kusaidia jambo fulani ili lifanywe |
| 3. mbinu | CH. sehemu yenye hali fulani ya hewa, zoni |
| 4. kuchangia | D. kwenda ndani ya maji |
| 5. kuzunguka | E. kupata faida kwa kufanya biashara |
| 6. ukanda | F. kipande cha ardhi kilichozungukwa na maji pande zote |
| 7. kuzalisha | G. kwenda huku na huku |

## Zoezi la 6.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni picha hizi na sentensi zinazofuata kwa usahihi.*













1. Hiki ni kituo cha kutengeneza nguvu za umeme katika Mto Nyabarongo.
2. Ziwani kuna chombo cha kusafiria.
3. Watalii wanatembea kwenye mchanga karibu na bahari hii.
4. Mamba amelala kwenye ufuo wa mto huu.

## 6.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

## Zoezi la 6.6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini kuhusu faida za kiutalii tunazopata kutokana na maji halafu mjitokeze mbele ya darasa ili kuwaelezea wenzenu. Hakikisheni kuwa mnajibu maswali haya katika majadiliano yenu:*

1. Ni vivutio vipi vya utalii vyenye mazingira ya maji?
2. Ni mambo gani ya kuvutia tunayopata katika vivutio hivyo?
3. Vivutio hivyo vinatumiwa vipi kuleta faida kwa nchi yetu?

### 6.4.1 Zoezi la imla

*Funga kitabu chako kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi kifungu ambacho mwalimu wako atakusomea.*

## 6.5 Sarufi: Kiulizi '*-pi*'

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni maswali yafuatayo katika umoja na wingi kisha mwelezeane ugunduzi wenu.*

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mtalii ***yu***pi atafika kesho? | Watalii ***wa***pi/***we***pi watafika kesho? |
| Mnyama ***yu***pi alitoroka? | Wanyama ***wa***pi/***we***pi walitoroka? |
| Mlima ***u***pi unapendeza? | Milima ***i***pi inapendeza? |
| Kituo ***ki***pi kinavutia? | Vituo ***vi***pi vinavutia? |
| Nyumba ***i***pi inahifadhi vifaa vyetu? | Nyumba ***zi***pi zinahifadhi vifaa vyetu? |
| Ukuta ***u***pi ulipakwa rangi? | Kuta ***zi***pi zilipakwa rangi? |

### Zoezi la 6.7

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi tano katika umoja na wingi kwa kutumia kiulizi "-pi" katika ngeli mbalimbali za Kiswahili.*

### Zoezi la 6.8

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kamilisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia kiulizi '**-pi**' kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** Kiti ________ kitakaliwa na mtalii?

**Jibu:** Kiti ***kipi*** kitakaliwa na mtalii?

1. Mtoto ________ anaweza kupika uji?
2. Viatu ________ vilinunuliwa na wageni hawa?
3. Ng'ombe ________ walichinjwa sokoni jana?
4. Kikombe ________ kilijazwa chai?
5. Ubao ________ ulitengenezwa wiki iliyopita?

### Zoezi la 6.9

*Andika sentensi za zoezi la 8 (la hapo awali) katika umoja au wingi.*

**Kwa mfano:**

**Sentensi:** **(Umoja)** Kiti ***kipi*** kitakaliwa na mtalii?

**Jibu:** **(Wingi)** Viti ***vipi*** vitakaliwa na watalii?

**Maelezo muhimu!**

Kiulizi '***-pi***' hutumika kuulizia swali kwa kumtaka mtu achague kitu kimoja au vitu fulani miongoni mwa vitu vingine vilivyopo.

**Kwa mfano:**

**Swali:** Mwanafunzi ***yu***pi ni mwerevu?
**Jibu:** Mwanafunzi mwerevu ni ***Kamaliza.***
*Wanafunzi ni wengi lakini mzungumzaji anauliza swali ili ajue mwanafunzi mwerevu miongoni mwa wanafunzi wengi.*
**Swali:** Wanafunzi ***wa***pi/ ***we***pi ni werevu?
**Jibu:** Wanafunzi werevu ni ***Kamaliza*** na ***Iradukunda.***
*Wanafunzi ni wengi lakini mzungumzaji anauliza swali ili ajue wanafunzi werevu tu miongoni mwa wanafunzi wote waliopo.*
Kiulizi '-pi' kinatumika kulingana na ngeli inayohusika.
**Kwa mfano:**

| Umoja | Wingi | Ngeli |
|---|---|---|
| Mtoto ***yu***pi analia? | Watoto ***wa***pi/***we***pi wanalia? | A-WA |
| Kitabu ***ki***pi kinasomwa? | Vitabu ***vi***pi vinasomwa? | KI-VI |
| Mlima ***u***pi umepandwa? | Milima ***i***pi imepandwa? | U-I |
| Nyumba ***i***pi itajengwa? | Nyumba ***zi***pi zitajengwa? | I-ZI |
| Ukuta ***u***pi umebomoka? | Kuta ***zi***pi zimebomoka? | U-ZI |

## Tathmini ya mada ya 1

### Zoezi la 1

*Jibu maswali yafuatayo kwa usahihi.*

1. Taja vivutio vya utalii vilivyopo nchini Rwanda.
2. Taja baadhi ya wanyama ambao hupatikana katika mbuga ya wanyama ya Akagera.
3. Mbuga ya wanyama ya milima ya Virunga inajulikana kwa wanyama gani?
4. Kwa nini sisi kama Wanyarwanda tunafaa kujivunia utamaduni wetu?

### Zoezi la 2

*Andika sentensi hizi kwa kutumia wakati wa mazoea.*

1. Wewe utaandika ubaoni wakati wa somo letu.
2. Mimi na ndugu yangu tutapika chakula baada ya somo letu.
3. Wewe na mtalii huyu mtafurahia kutazama mnyama yule.
4. Mkulima huyu na Semana watalima shamba lao katika mwezi wa Februari.
5. Wanafunzi hawa wanaimba nyimbo za kufurahisha.

## Zoezi la 3

*Taja aina za pesa ambazo hutumiwa katika nchi zifuatazo.*

1. Naijeria
2. Japani
3. Malawi
4. Rwanda
5. Kanada

## Zoezi la 4

*Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiulizi '**-pi**' kwa usahihi.*

1. Kioo _______ kilivunjika?
2. Mlima _______ una wanyamapori wengi?
3. Ufagio _______ uliharibika?
4. Ndizi _______ ni ya mtoto huyu?
5. Mzigo _______ ni wa mgeni huyu?

## Zoezi la 5

*Jaza nafasi zilizo wazi kwa jibu sahihi kutoka kwenye mabano.*

1. ____________ alizuru mbuga ya Akagera? (*Nini, Nani*)
2. ____________ kitaliwa na wageni? (*Nani, Nini*)
3. ____________ hajawahi kumwona simba? (*Nini, Nani*)
4. ____________ kitaletwa na mhudumu wa hoteli? (*Nani, Nini*)
5. ____________ kilitumika kuwapiga picha wanyamapori? (*Nani, Nini*)

## Zoezi la 6

*Tunga sentensi tano sahihi kwa kutumia kiulizi* ***'kwa nini'.***

**Mfano:** ***Kwa nini*** unamwogopa simba?

## Faharasa

| | |
|---|---|
| utalii: | utembeleaji wa maeneo maalumu au maeneo ya kihistoria kwa ajili ya kujifunza au kujifurahisha |
| mazingira: | vitu vinavyomzunguka mtu katika makazi yake |
| kuzuru: | kutembelea |
| utamaduni: | mwenendo wa maisha unaohusisha asili, mila, desturi au itikadi unaotawala katika jamii fulani |
| maakuli: | chakula |
| bara: | pande kubwa la nchi kavu la Dunia lenye jumla ya nchi kadhaa na limezungukwa na bahari |
| vilele: | sehemu za mwisho kuelekea juu ya mlima |
| kuwawinda: | kuwafukuza wanyama kwa lengo la kuwaua ili kujinufaisha kifedha au kwa ajili ya chakula |
| ametukazia macho: | ametuangalia kwa macho makali |
| hawatambui: | hawafahamu; hawajui |
| majamvi: | mikeka mikubwa iliyosukwa kwa miyaa na hutumiwa kukalia, kulalia au kuanikia vitu |
| inayostawisha: | inayosababisha kuwa na hali nzuri |
| chanzo: | sababu ya kuanza kwa kitu |
| mandhari: | mwonekano wa mahali |

# SURA YA PILI

## MADA KUU 2: LUGHA NA MATUKIO YA KIJAMII NA KITAIFA

## MADA NDOGO: Sikukuu na sherehe nchini Rwanda

## SOMO LA 7: Sikukuu na sherehe katika kalenda

### 7.1 Kifungu kuhusu sikukuu na sherehe nchini Rwanda

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni kalenda hii ya mwaka wa 2016 kisha mjadiliane kuhusu tarehe maalum za sikukuu rasmi:*

**Kalenda ya 2016**

**Januari**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**Februari**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | | | | | |

**Machi**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

**Aprili**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

**Mei**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**Juni**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | | |

**Julai**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**Agosti**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | 31 | | | |

**Septemba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | |

**Oktoba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | 31 | | | | | |

**Novemba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | | | |

**Disemba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 |

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni picha hizi kisha msome kifungu cha habari kinachofuata kuhusu sikukuu na sherehe nchini Rwanda. Baada ya kusoma kifungu, mjibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*





Rwanda ni nchi ambayo ina sikukuu na sherehe rasmi nyingi katika kalenda ya taifa. Wanyarwanda huburudika na kusherehekea matukio yote muhimu. Wanyarwanda huadhimisha sikukuu mbalimbali hasa za kitamaduni, kidini na kisiasa. Shamrashamra za kuadhimisha sikukuu hizo zote zinakubaliwa kisheria na zimewekwa katika kalenda ya taifa na serikali inaunga mkono sikukuu na sherehe hizo.

Sikukuu ya kwanza inayoadhimishwa mwanzoni mwa mwaka ni sherehe za mwaka mpya. Sikukuu hii huadhimishwa tarehe moja mwezi wa Januari. Siku nyingine yenye thamani katika historia ya Rwanda ni siku ya mashujaa inayoadhimishwa tarehe moja mwezi wa Februari. Katika mwezi wa Aprili kuna sikukuu ya Pasaka inayoadhimishwa na Wakristo. Tarehe nyingine muhimu katika historia ya nchi yetu ni tarehe saba mwezi wa Aprili. Ni sikukuu ya kumbukumbu za mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi nchini Rwanda yaliyotokea mwaka 1994. Sikukuu ya wafanyakazi huadhimishwa tarehe moja mwezi wa Mei. Huu huwa ni wakati maalum wa kuwatambua wafanyakazi wote nchini.

Sikukuu ya uhuru wa nchi ya Rwanda huadhimishwa kila tarehe moja mwezi wa Julai. Wanyarwanda hukumbuka namna walivyopambana na kujitolea katika kujikomboa kutoka kwa utawala wa mkoloni. Tarehe nyingine yenye historia kwetu ni tarehe nne mwezi wa Julai. Hii huwa ni sikukuu ya Ukombozi wa taifa. Siku ya kukumbuka njia ndefu ya kuikomboa nchi ya Rwanda. Sikukuu nyingine ambayo husherehekewa ni Umuganura. Umuganura huadhimishwa kila wiki ya kwanza ya mwezi wa Agosti kwenye siku inayochaguliwa na serikali ya Rwanda. Tarehe kumi na tano mwezi wa Agosti, Wakatoliki huadhimisha kupazwa mbinguni kwa Bikira Mariamu. Hii huwa ni sikukuu nchini. Kuna sherehe nyingine za jamii ya Wanyarwanda kama vile: harusi za aina mbalimbali, sherehe za kumaliza kitu fulani kama vile: kumaliza masomo chuoni, kupeana ng'ombe, n.k.

Waislamu wana sherehe mbili kuu. Sherehe ya Idi-ul-Fitr ya kila mwaka. Sherehe hii ya kidini husherehekewa tarehe inayotangazwa na Jumuiya ya Waislamu Rwanda. Waislamu pia husherehekea sikukuu ya Idi ul-Adha kila mwaka. Sherehe hii pia hufanyika tarehe inayotangazwa na Jumuiya ya Waislamu Rwanda.

Wakristo nao wana sherehe mbalimbali kama vile: Pasaka inayoadhimishwa kila mwaka na Krismasi inayoadhimishwa tarehe ishirini na tano mwezi wa Disemba kila mwaka.

## Maswali ya ufahamu

1. Taja sherehe ambayo husherehekewa mwanzoni mwa mwaka.
2. Taja sherehe ambayo husherehekewa mwishoni mwa mwaka.
3. Ni sherehe gani ambayo huadhimishwa tarehe saba mwezi wa Aprili nchini Rwanda?
4. Ni sherehe gani ambayo huadhimishwa tarehe moja mwezi wa Februari nchini Rwanda?
5. Ni sherehe gani ambayo huadhimishwa tarehe moja mwezi wa Julai nchini Rwanda?
6. Taja sherehe mbili ambazo huadhimishwa na Wakristo.
7. Taja sherehe mbili ambazo huadhimishwa na Waislamu.
8. Sherehe ya Umuganura huadhimishwa mwezi gani?
9. Sherehe ya Krismasi ni sikukuu ya dini gani?

## 7.2 Msamiati kuhusu sikukuu nchini Rwanda

*Kutokana na kifungu cha habari mlichosoma hapo awali, katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maana ya msamiati mpya uliojitokeza unaohusiana na sherehe na sikukuu nchini Rwanda. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***serikali:*** mfumo au chombo chenye mamlaka ya kutawala nchi au eneo fulani.

### Zoezi la 7.1

A. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi hizi. Tumieni kamusi panapohitajika.*

1. Wanyarwanda walipigana dhidi ya ***wakoloni***.
2. ***Wananchi*** hawafai kutumia mabavu wanapotafuta mali.
3. Nchi yetu ilipata ***ukombozi*** miaka mingi iliyopita.
4. ***Serikali*** yetu ina viongozi wazuri.
5. ***Utawala*** wa rais wetu ni wa kuigwa na viongozi wengi duniani.

B. *Katika makundi yenu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi za zoezi la 1A.*

**Zoezi la 7.2**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jazeni nafasi zilizo wazi katika sentensi hizi kwa jibu sahihi kutoka katika mabano.*

1. Sherehe za mwaka mpya ________________ mwanzoni mwa kila mwaka. (*huathimishwa, huadhimishwa*)
2. Rwanda ni ____________________ inayopendwa na watu wengi ulimwenguni. (*inchi, nchi*)
3. ____________ ya Krismasi hufanyika tarehe 25 mwezi wa Disemba. (*Shehere, Sherehe*)
4. Siku ya ______________ husherehekewa tarehe 1 mwezi wa Februari. (*washujaa, mashujaa*)
5. ______________ husherehekewa wiki ya kwanza mwezi wa Agosti. (*Umagunura, Umuganura*)

## 7.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha mjadili kuhusu sherehe na sikukuu nchini Rwanda. Waeleze wenzako:*

1. Shughuli zote zinazofanyika katika sherehe za mwaka mpya.
2. Nguo unazopenda kuvaa unapoenda katika sherehe za harusi.
3. Sikukuu unayopenda kuadhimisha katika kalenda. Toa sababu.
4. Umuhimu wa sikukuu na sherehe mbalimbali kwa Wanyarwanda.
5. Umuhimu wa kuwa na Kalenda rasmi nyumbani.

## 7.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni na muigize mchezo mfupi kuhusu sikukuu nchini Rwanda. Mwanafunzi mmoja amuulize mwenzake maswali mbele ya darasa, naye ajibu vizuri.*

**Mfano wa mazungumzo:**

**Kamana:** Habari dada Mukamana.

**Mukamana:** Salama kaka.

**Kamana:** Sikukuu ya Uhuru huadhimishwa lini?

**Mukamana:** Sikukuu ya Uhuru huadhimishwa tarehe mosi mwezi wa Julai kila mwaka.

**Kamana:** Ooh! Nimekumbuka. Asante sana dada.

**Zoezi la imla**

*Funga kitabu chako kisha ufungue daftari lako na uandike kwa usahihi maneno au vifungu vya maneno ambayo mwalimu wako atakusomea.*

## 7.5 Sarufi: Matumizi ya wakati uliopita

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii ya masimulizi mafupi yafuatayo kisha kila mmoja awasimulie wenzake alivyosherehekea mwaka mpya uliopita.*



Katika sherehe za mwaka mpya uliopita, niliamka mapema, nikaoga, nikapiga mswaki, nikavaa nguo mpya na kunywa kiamshakinywa. Baadaye niliondoka na kuelekea kijijini kumtembelea kaka yangu. Nilipofika huko kijijini, niliwaona watoto wengi wakicheza kandanda katika uwanja mdogo. Nilijiunga nao. Baada ya dakika chache, mwamuzi wa mchezo huo alipuliza kipenga cha kuashiria mwisho wa mchezo huo. Timu ya Mashujaa ilipata ushindi wa mabao matatu kwa moja dhidi ya timu ya Simba.

**Swali**: *Eleza wakati uliotumika katika masimulizi mliyosoma hapo juu pamoja na masimulizi yenu kwa kutoa mifano ya vitenzi vilivyotumika.*

**Zoezi la 7.3**

A. Orodhesha vitenzi vyote vilivyotumika katika masimulizi mliyoyasoma hapo awali.

B. Tambua nyakati zilizotumika katika vitenzi mlivyoorodhesha.

### Maelezo muhimu!

Wakati uliopita huonyesha matukio ambayo huwa tayari yameshatendeka. Wakati uliopita hutumia kiambishi cha wakati ***-li-***. Kiambishi hiki hutumika katika nafsi zote za Kiswahili.

Kiambishi ***-ka-*** hutumika katika sentensi iliyo na matukio yanayofuatana katika wakati uliopita.

**Mifano:**

1. Ni***li***tembea pamoja na kakangu.
2. A***li***amka akavaa nguo za michezo.
3. Mimi ni***li***pika chakula, nikala na kulala.
4. Dereva a***li***washa gari, akaliendesha haraka na kushikwa na polisi.
5. Sisi tu***li***vuna mahindi wiki iliyopita.

Katika masimulizi ya wakati uliopita, maneno kama vile: *halafu, kisha* na *baadaye* hutumika.

## Zoezi la 7.4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jazeni nafasi zilizo wazi katika sentensi zinazofuata kwa kutumia wakati uliopita.*

**Kwa mfano:** Mama ____________ (*fua*) nguo, ____________ (*pika*) na __________ (*fagia*) nyumba.

**Jibu:** Mama ***alifua*** nguo, ***akapika*** na ***kufagia*** nyumba.

1. Kaka ____________ (*oga*), ____________ (*piga*) nguo pasi na ____________ (*enda*) shuleni.
2. Mtoto ____________ (*kunywa*) maziwa, ____________ (*bembelezwa*) na ____________ (*lala*).
3. Mwanafunzi ______________ (*enda*) shuleni, ______________ (*soma*) na ____________ (*fanya*) mtihani.
4. Ng'ombe ______________ (*kula*) nyasi, ______________ (*kunywa*) maji na ____________ (*rudi*) zizini.
5. Mmea ________________ (*pandwa*), ______________ (*wekewa*) mbolea na ____________ (*nyunyiziwa*) maji.

## Zoezi la 7.5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, badilisheni sentensi hizi ziwe katika wakati uliopita.*

1. Mama anapika wali.
2. Mimi nitaenda shule.
3. Kwa nini unalia?
4. Siku ya sherehe ya Krismasi imefika.
5. Wanyarwanda wanaadhimisha siku ya Mashujaa.

**Zoezi la 7.6**

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mtunge sentensi tano sahihi kwa kutumia wakati uliopita ukitanguliza msamiati ufuatao.*

**Kwa mfano:** Tarehe

***Tarehe*** moja mwezi wa Februari tuliadhimisha sikukuu ya Mashujaa.

1. Uhuru
2. Ukombozi
3. Ukoloni
4. Utawala
5. Siasa

## 7.6 Sarufi: Matumizi ya wakati ujao

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni mchoro wa kifungu kifuatacho kisha kila mmoja asimulie anavyopanga kusherehekea mwaka mpya ujao baada ya kusoma kifungu mlichopewa kwenye ukurasa unaofuata.*



Katika sherehe za mwaka mpya ujao, nitaamka mapema, nivae sare yangu safi na kupiga mswaki. Baada ya kiamshakinywa, nitajiunga na wanafunzi wenzangu kwenda kutembelea mbuga ya wanyama ya Akagera. Huko tutawaona twiga na swara wengi ambao hatujawahi kuwaona. Tutafurahi iwapo tutapewa mlinzi wa mbuga wa kutuonyesha sehemu zote za mbuga hiyo. Tutawaona simba, ndovu, mamba na hata fisi. Mwishowe, tutapiga picha nyingi.

**Swali**: *Eleza wakati uliotumika katika masimulizi mliyosoma hapo juu pamoja na masimulizi yenu kwa kutoa mifano ya vitenzi vilivyotumika.*

## Zoezi la 7.7

A. Orodhesha vitenzi vyote vilivyotumika katika masimulizi mliyoyasoma hapo awali.

B. Tambua nyakati zilizotumika katika vitenzi mlivyoorodhesha.

## Zoezi la 7.8

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizo wazi kwa vitenzi vilivyo kwenye mabano katika wakati ujao.*

Katika sherehe za Pasaka za mwaka ujao, Kamana ______________ (*enda*) kanisani kwa ajili ya ibada. Baadaye, ____________ (*tembelea*) marafiki zake na kusherehekea pamoja nao. Kisha jioni ________________ (*rudi*) nyumbani. Ndugu yake Yusufu ________________ (*pokea*) kwenye kituo cha basi. Halafu ______________ (*enda*) nyumbani pamoja.

## Zoezi la 7.9

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni aya moja sahihi yenye kuhusisha matukio ya wakati ujao.*

## Zoezi la 7.10

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, badilisheni sentensi zinazofuata ziwe katika wakati ujao.*

**Kwa mfano:** Mwalimu anaandika ubaoni.

**Jibu:** Mwalimu ataandika ubaoni.

1. Mwanafunzi huyu anasoma kitabu cha hadithi.
2. Mbuga hii ilifunguliwa na rais wetu.
3. Darasa letu limesafishwa na wanafunzi hawa.
4. Kwa nini mnanunua vitabu vingine?
5. Wanyamapori hawa wanakula nyasi.

### Maelezo muhimu!

Wakati ujao hutumiwa kuonyesha matukio ambayo huwa yanatarajiwa kutendeka. Wakati huu hutumia kiambishi ***-ta-***. Kiambishi hiki hutumika katika nafsi zote za Kiswahili.

**Mifano:**

1. Ni***ta***omba walinzi wa mbuga waniongoze na baadaye ni***ta***piga picha.
2. Ni***ta***vaa kanzu nzuri halafu ni***ta***enda msikitini kusali.
3. Mwalimu a***ta***tufundisha kesho kisha a***ta***tupa mtihani.
4. Sherehe ya Idi ul Fitri i***ta***adhimishwa mwezi ujao.
5. Wanafunzi wa***ta***fanya mtihani wiki ijayo.

Katika masimulizi ya matukio ya wakati ujao, maneno kama vile: ***kisha, halafu, mwishowe*** na ***baadaye*** hutumika.

## SOMO LA 8: Maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda

### 8.1 Shairi kuhusu maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mtazame picha hizi na hapo baadaye msome na kukariri shairi lifuatalo na kulijadili:*





Furaha tele tunayo, mioyo yetu imetulia,
Wanyarwanda tulijikomboa, kutoka kwa wakoloni,
Maisha yakabadilika, amani tukapata,
Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.

Sikukuu tunazo tele, kila mwaka furaha,
Kuanzia Januari, hadi mwezi Disemba,
Wanyarwanda hufurahia, kuadhimisha sikukuu,
Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.

Mwaka mpya karibu, Januari kusherehekea,
Asante Mola kwa uhai, kutufikisha mwaka mpya,
Tarehe moja Januari, hufurahiwa na kila mtu,
Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.

Februari haitulii, mashujaa kuwaenzi,
Nayo Aprili ikifika, Wakristo na Pasaka,
Kumbukumbu za mauaji ya Kimbari, huhuzunisha,
Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.

Julai ni furaha teletele, uhuru tunao sisi,
Ukombozi wetu hukumbukwa, Wanyarwanda tuko huru,
Agosti huadhimishwa, sherehe ya Umuganura,
Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.

Waislamu twawapenda, kuadhimisha sherehe zao,
Idi-ul-Fitr na Idi ul-Adha, msaada kwa wasiojiweza,
Krismasi huja Disemba, furaha kwa Wakristo,
Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.

## Maswali ya tathmini

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini na mjibu maswali haya ya tathmini kuhusiana na shairi mlilosoma hapo awali.*

1. Taja sherehe ambayo huadhimishwa mwanzoni mwa kila mwaka.
2. Sikukuuu ya Mashujaa husherehekewa lini?
3. Pasaka huadhimishwa na watu gani? Wao hukumbuka nini katika siku hii?
4. Taja sikukuu za Waislamu kutokana na shairi ulilosoma?
5. Sikukuu ya Uhuru nchini Rwanda husherehekewa lini?
6. Kumbukumbu za mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi hufanyika lini?
7. Shairi hili lina mishororo mingapi?
8. Taja kibwagizo cha shairi hili.
9. Sherehe za Krismasi huadhimishwa lini?
10. Sikukuu ya Umuganura hufanyika lini?

## 8.2 Msamiati kuhusu maadhimisho mbalimbali

*Kutokana na shairi mlilosoma hapo awali, katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini maana ya msamiati mpya uliojitokeza unaohusiana na maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***Ukombozi:*** matendo au vita vya kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge.

**Zoezi la 8.1**

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata.*

1. Leo tunaadhimisha ***sikukuu*** ya Mashujaa.
2. Hii ni kalenda ya ***mwaka*** wa 2017.
3. Mwezi wa kwanza katika kalenda ya mwaka ni ***Januari***.
4. ***Wakristo*** husherehekea sikukuu ya Pasaka kila mwaka.
5. ***Waislamu*** husali mara tano kwa siku.
6. Waislamu huadhimisha sherehe ya ***Idi-ul-Fitr*** kila mwaka.
7. Msimu wa sherehe za ***Krismasi*** umefika.
8. ***Wanyarwanda*** huadhimisha sikukuu ya Uhuru wa Taifa kila mwaka.
9. Leo ni tarehe kumi mwezi ***Disemba*** mwaka 2016.
10. Sherehe ya ***Umuganura*** itaadhimishwa kesho.

## 8.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha mjadiliane na kuelezana kuhusu:*

1. Shughuli zinazofanyika nyumbani kwenu wakati wa sherehe za mwaka mpya.
2. Namna mnavyoadhimisha sikukuu iliyo katika mwezi Julai.
3. Shughuli zinazotekelezwa kwenu wakati wa sherehe za *Umuganura*.
4. Shughuli zinazotekelezwa wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Ukombozi wa Taifa.
5. Shughuli zinazofanyika wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Uhuru wa Taifa.

## 8.4 Kusikiliza na kuzungumza: Zoezi la mazungumzo

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni mazungumzo mafupi yafuatayo na majibu yatolewe palipo na maswali mbele ya wanafunzi wenzenu.*

**Mazungumzo kati ya Kamana na Teta:**

**Kamana:** Sikukuu ya Uhuru huadhimishwa tarehe gani?

**Teta:** Sikukuu ya Uhuru huadhimishwa tarehe moja mwezi wa Julai kila mwaka.

**Kamana:** Sikukuu ya sherehe za mwaka mpya huadhimishwa tarehe gani?

**Teta:** Sherehe za mwaka mpya huadhimishwa tarehe moja mwezi wa Januari kila mwaka.

*Endelezeni mazungumzo haya kwa maneno yenu wenyewe.*

## 8.5 Sarufi: Vitenzi vya silabi moja

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha mbainishe vitenzi vilivyo katika sentensi hizi zenye michoro.*



1. Ng'ombe wa jirani ali***kufa***.




2. Wanafunzi wali***kunywa*** maji safi.



3. Kaka ali***pika*** chakula kitamu.



4. Watoto wali***kula*** chakula chao cha mchana.



5. Daktari alim***<u>pima</u>*** kaka aliye***<u>kuwa</u>*** mgonjwa.



6. Wanafunzi wali***<u>cheza</u>*** uwanjani.



7. Shehe aliwa***<u>fundisha</u>*** watoto kuhusu Kurani.

*Katika makundi yenu, chunguzeni miundo ya vitenzi vilivyopigiwa mistari.*

## Zoezi la 8.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi tano sahihi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo.*

**Kwa mfano:** kuja

**Jibu:** Mwalimu *alikuja* kututembelea nyumbani kwetu.

1. kufa
2. kunywa
3. kula
4. kuwa
5. kuja

### Maelezo muhimu!

Katika lugha ya Kiswahili kuna vitenzi vyenye silabi moja. Vitenzi hivi huambatanishwa na ***'ku-'*** katika matumizi.

**Kwa mfano:**

kufa: ***–f-***

kuwa: ***-w-***

kunywa: ***-nyw-***

kula: ***-l-***

kuja: ***-j-***

**Matumizi katika sentensi**

1. Mtoto ali***kunywa*** dawa.
2. Ng'ombe ali***kula*** nyasi.
3. Nyanya ali***kuja*** dukani.

**Zoezi la 8.3**

*A. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, rekebisheni sentensi hizi:*

1. Mwalimu alija darasani.
2. Mbuzi wetu alifa jana.
3. Kalisa alinywa maji.
4. Dada alila wali.
5. Mama aliwa mgonjwa.

*B. Kanusha sentensi mlizosahihisha katika A hapo juu.*

## 8.5.1 Vitenzi vya silabi moja, tungo yakinishi na kanushi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi hizi kisha mjadili ugunduzi wenu.*

1. Mtoto alikunywa dawa. - Mtoto hakunywa dawa.
2. Paka wao alikufa jana. - Paka wao hakufa jana.
3. Mgeni alikuja haraka. - Mgeni hakuja haraka.

### Maelezo muhimu!

***Vitenzi vya silabi moja*** huambatanishwa na ***'ku-'*** katika hali yakinishi. Katika hali kanushi, vitenzi hivi huambatanishwa na kikanushi ***'ha-'*** na nafsi husika.

**Kwa mfano:**

1. Wagonjwa wali***kula*** chakula. - Wagonjwa ***hawakula*** chakula.
2. Walimu wali***kunywa*** chai. - Walimu ***hawakunywa*** chai.
3. Paka wa jirani wali***kufa*** jana. - Paka wa jirani ***hawakufa*** jana.

## Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni mifano ya sentensi katika jedwali hili.*

| **Wakati Uliopita** | | |
|---|---|---|
| **Kitenzi** | **Hali Yakinishi** | **Hali Kanushi** |
| kufa | *Mbwa alikufa jana.* | *Mbwa hakufa jana.* |
| kuwa | *Zamani tulikuwa watoto.* | *Zamani hatukuwa watoto.* |
| kunywa | *Tulikunywa maji.* | *Hatukunywa maji.* |
| kula | *Tulikula chakula.* | *Hatukula chakula.* |
| kuja | *Tulikuja jana.* | *Hatukuja jana.* |

*Je, mmegundua nini?*

## Zoezi la 8.4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tumieni vitenzi vyenye silabi moja vifuatavyo katika wakati uliopita hali yakinishi katika umoja na wingi. Tumieni nafsi zote za Kiswahili.*

**Mfano:** **kunywa:** ***-nyw-***

**Jibu:** Mtoto ali***kunywa*** maziwa. - Watoto wali***kunywa*** maziwa.

1. kuwa
2. kuja
3. kufa
4. kula

## Zoezi la 8.5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tumieni vitenzi vyenye silabi moja vifuatavyo katika wakati uliopita hali kanushi. Tumieni nafsi zote za Kiswahili.*

**Mfano:** **kunywa:** ***-nyw-***

**Jibu:** Mtoto **hakunywa** maziwa yote.

1. kuwa
2. kuja
3. kufa
4. kula

## Zoezi la 8.6

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi zifuatazo katika umoja au wingi.*

**Kwa mfano:**

**Umoja:** Mwalimu alikuwa darasani.

**Wingi:** Walimu walikuwa madarasani.


1. Mtu huyu alikuja jana jioni.
2. Wanafunzi hawa wanakunywa maziwa.
3. Mtoto anakula mkate.
4. Panya alikufa mtegoni.
5. Viongozi walikuwa mjini Kigali.

## SOMO LA 9: Matumizi ya kalenda ya mwaka

### 9.1 Mazungumzo kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni kalenda hii ya mwaka wa 2017 kisha msome mazungumzo yaliyo hapo chini na hatimaye mjibu maswali yanayofuata.*

**Kalenda ya mwaka, 2017**




**Kalisa:** Hujambo rafiki yangu?

**Birasa:** Sijambo Kalisa. Habari ya siku nyingi?

**Kalisa:** Njema. Nashukuru Mungu kwa uhai na afya.

**Birasa:** Nafurahi kusikia u mzima. Mimi pia ni mzima namshukuru Mungu kwa yote.

**Kalisa:** Unaendelea vipi na masomo yako?

**Birasa:** Naendelea vyema kabisa. Nafanya bidii ili nifaulu katika mitihani yangu.

**Kalisa:** Hivi nikuulize, wewe unafurahishwa na somo lipi shuleni?

**Birasa:** Mimi kwa kusema ukweli ninapenda masomo yote ila somo la Kiswahili hunifurahisha kabisa.

**Kalisa:** Mimi pia ni kama wewe, napenda masomo yote ila somo la Kiswahili hunichangamsha zaidi.

**Birasa:** Hehehe! Kwa nini lakini?

**Kalisa:** Hii ni kwa sababu katika somo la Kiswahili huwa tunafundishwa kuhusu mambo ya kawaida ambayo tunayafahamu katika jamii zetu na maisha yetu ya kila siku.

**Birasa:** Kweli. Kwanza somo letu la juzi kuhusu matumizi ya kalenda lilikuwa rahisi sana.

**Kalisa:** Ooh! Kumbe mmeshafundishwa kuhusu matumizi ya kalenda? Sisi bado hatujafundishwa hayo ila sidhani kama ni mambo magumu. Ni kuhusu nini hasa?

**Birasa:** Mada hiyo ni rahisi sana. Ni kuhusu namna ya kuweza kutambua miezi, tarehe na siku mbalimbali katika kalenda ya mwaka husika.

**Kalisa:** Aha! Hiyo ni rahisi sana. Mimi ninajua kuhesabu mwezi wa kwanza hadi wa mwisho. Nikuhesabie?

**Birasa:** Ehe! Ebu hesabu nisikie…

**Kalisa:** Kuna Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba na Disemba, ama?

**Birasa:** (*Anampigia makofi*) Kweli kabisa. Nikuulize swali jingine?

**Kalisa:** Naam, uliza. Nitajaribu kulijibu.

**Birasa:** Sawa. Mtu huweza kuielewa na kuitumia vipi kalenda?

**Kalisa:** Hata kama bado hatujafundishwa hili naweza kujibu kutokana na maarifa yangu ya hapo awali kuhusu kalenda. Mtu husoma kalenda kwa kurejelea mwezi husika, tarehe na siku iliyoandikwa kwenye kalenda hiyo.

**Birasa:** Kweli kabisa Kalisa. Naona wewe ni mwanafunzi mwerevu.

**Kalisa:** Hehehe, ni kujitahidi kaka!

**Birasa:** Haya basi Kalisa, naomba kukimbia nyumbani kabla ya jua kutua. Tuonane kesho inshallah!

**Kalisa:** Sawa Birasa. Kesho pia ni siku. Kwaheri.

**Birasa:** Kwaheri ya kuonana.

## Maswali ya ufahamu

1. Mwezi wa Januari una Jumapili ngapi?
2. Tarehe 5 mwezi wa Mei ni siku gani?
3. Mwaka wa 2017 una siku ngapi?
4. Mwezi wa Septemba una Jumatano ngapi?
5. Sikukuu ya Mashujaa wa Taifa iliadhimishwa siku gani katika kalenda iliyo hapo juu?
6. Krismasi itaadhimishwa siku gani katika kalenda iliyo hapo juu?
7. Sikukuu ya mwaka mpya 2017 iliadhimishwa siku na tarehe gani?
8. Mwezi wa Agosti una siku ngapi?
9. Mwezi wa Disemba una Alhamisi ngapi?
10. Ni miezi mingapi isiyokuwa na sikukuu katika kalenda iliyo hapo juu? Itaje.

## 9.2 Msamiati kuhusu kalenda ya mwaka

### Zoezi la 9.1

(i) *Kutokana na mazungumzo kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka mliyoyasoma hapo awali, katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika inapohitajika.*

1. ***Jumamosi*** ni siku inayotangulia Jumapili.
2. Huu ni ***mwezi*** wa Ramadhani.
3. ***Siku*** hii imekuwa ya mikutano mingi.
4. Mwezi wa kwanza katika ***kalenda*** ya mwaka ni Januari.
5. ***Mwaka*** ujao tutazuru nchi ya Kenya.
6. Sherehe za Krismasi hufanyika mwezi wa ***Disemba***.
7. ***Tarehe*** mbili mwezi ujao tutasafiri kuelekea kijijini kwetu.
8. Tutafungua shule mwezi ***Mei.***

(ii) *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika Zoezi la 1 (i) hapo juu.*

## 9.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mtazame mchoro ufuatao wa kalenda ya mwaka wa 2017 na kujadili.*

# Kalenda ya 2017

**Januari**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**Februari**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | | | | |

**Machi**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

**Aprili**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | | | | | | |

**Mei**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | 31 | | | |

**Juni**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | |

**Julai**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | 31 | | | | | |

**Agosti**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

**Septemba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

**Oktoba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**Novemba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | | |

**Disemba**

| Su | Mo | Tu | We | Th | Fr | Sa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

*Katika makundi yenu, jadilini kuhusu namna ya kuisoma kalenda hiyo ya mwaka wa 2017 na kuielewa kimatumizi. Waelezee wenzako:*

1. Miezi yote iliyo na siku thelathini.
2. Miezi yote iliyo na siku thelathini na moja.
3. Mwezi ulio na siku chache kuliko miezi mingine.
4. Miezi iliyo na Jumapili nyingi kuliko mingine.
5. Miezi iliyo na sikukuu rasmi za kusherehekewa.
6. Mwezi wa Disemba una Jumapili ngapi?
7. Tarehe ya kwanza katika mwezi wa Septemba ni siku gani?
8. Tarehe kumi mwezi wa Agosti ni siku gani?

**Maelezo muhimu!**

- ***Kalenda*** ni kifaa kinachoonyesha siku, tarehe na miezi katika mwaka.
- Mwaka una miezi kumi na miwili ambayo ni: ***Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba*** na ***Disemba***.
- Siku katika kila mwezi huanzia Jumapili hadi Jumamosi.
- Mwaka mmoja una wiki hamsini na mbili.
- Wiki moja ina siku saba ambazo ni: ***Jumapili, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa*** na ***Jumamosi***.
- Katika kalenda, siku za Jumapili huandikwa kwa kutumia wino wa rangi tofauti.
- Siku za matukio makuu ya sherehe za kitaifa na kijamii huandikwa kwa kutumia wino wa rangi tofauti.

## 9.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha mwigize mazungumzo mliyoyasoma hapo awali kati ya Birasa na Kalisa kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka.*

## 9.5 Sarufi

### Matumizi ya herufi kubwa na alama za uandishi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni kifungu kifuatacho kisha mbainishe maneno yote yaliyotumia herufi kubwa pamoja na alama mbalimbali za uandishi na hapo baadaye mjibu maswali ya tathmini yanayofuata.*

Biruta ni mwalimu mkuu katika shule ya sekondari ya Kamashashi iliyo mjini Kigali. Biruta anaishi Gikondo. Yeye ni mwalimu mwenye bidii na kila mara tunapochelewa shuleni yeye hutuuliza, “Kwa nini mmechelewa leo?” Sisi humwomba msamaha naye huturuhusu kwenda darasani.

Jumamosi iliyotangulia sherehe za Krismasi tulikutana na mwalimu Biruta katika duka la kuuza vitabu. Alishangaa na kuniuliza, “Ooh! Kumbe wewe unapenda kusoma hivi?” Nikamjibu kuwa ninapenda sana kununua vitabu vya hadithi za Kiswahili na Kiingereza pamoja na vya Historia na Hisabati. Tukiachana, mwalimu Biruta alinikumbusha kuwa shule yetu itafunguliwa tarehe 9/05/2017.

## Maswali ya tathmini

1. *Eleza matumizi mbalimbali ya herufi kubwa kutokana na kifungu kifupi mlichosoma hapo awali kumhusu Biruta.*

   **Kwa mfano:** *Biruta anaishi Gikondo.*

   **Matumizi:** Herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa jina la mtu (*Biruta*) na jina la mahali (*Gikondo*).

2. *Eleza matumizi mbalimbali ya alama nyingine za uandishi kutokana na kifungu mlichosoma hapo juu kisha mwonyeshe matumizi katika sentensi.*

   **Kwa mfano:** Nukta (.)

   **Matumizi:** Nukta imetumika mwishoni mwa sentensi kamili.

   **Mfano wa sentensi:** *Biruta ni mwalimu mkuu katika shule ya sekondari ya Kamashashi iliyo mjini Kigali.*

### Zoezi la 9.2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, rekebisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia alama za uandishi kwa usahihi.*

**Kwa mfano:** neza ataenda shule jumatatu

**Jibu:** Neza ataenda shule Jumatatu.

1. kwa nini ulichelewa shuleni
2. lo umebeba mzigo huo pekee yako
3. mama alienda sokoni kununua ndizi machungwa viazi na nanasi
4. paka amekunywa maziwa
5. ngabo atakuja lini

### Zoezi la 9.3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, rekebisheni kifungu hiki kwa kutumia alama za uandishi pamoja na herufi kubwa kwa usahihi.*

siku moja nilienda sokoni kununua ndizi sukari samaki mboga na machungwa. njiani nilikutana na rafiki yangu birasa. alishangaa kuniona na kusema ah kumbe wewe pia huja sokoni nikamjibu kuwa mimi hupenda kumsaidia mama kununua bidhaa mbalimbali. nilimuuliza umekuja kununua nini. akanijibu kuwa alikuja kununua mboga na samaki

## Tathmini ya mada ya 2

**Zoezi la 1**

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha mjadili maswali yafuatayo. Waelezee wenzako kuhusu:*

1. Shughuli zinazofanyika wakati wa sikukuu ya Pasaka kwa Wakristo.
2. Shughuli zinazofanyika wakati wa sikukuu ya *Idi ul Fitri* kwa Waislamu.
3. Shughuli na burudani zinazofanyika katika sherehe ya harusi.
4. Sherehe ya Kiislamu ya *Idi ul Adha* huadhimishwa lini? Jadili shughuli zinazofanyika wakati wa sherehe hiyo.
5. Sherehe ya Kikristo ya Krismasi huadhimishwa lini? Jadili shughuli zinazofanyika wakati wa sherehe hiyo.

**Zoezi la 2**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, rekebisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia alama za uandishi kwa usahihi*

**Kwa mfano:** pasaka iliadhimishwa tarehe gani

**Jibu:** Pasaka iliadhimishwa tarehe gani?

1. baadhi ya sherehe katika kalenda yetu ni pasaka krismasi na umuganura
2. siku ya kwanza ya wiki ni jumapili katika kalenda ya mwaka
3. kamana anaishi wapi
4. lo simu yangu imeanguka majini
5. kilo moja ya chumvi huuzwa faranga mia mbili 200

**Zoezi la 3**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi zifuatazo katika wakati ujao.*

**Kwa mfano:** Baba alinunua maji, soda na mkate.

**Jibu:** Baba atanunua maji, soda na mkate.

1. Mwalimu alitufundisha Hisabati.
2. Ng'ombe alikunywa maji mengi.
3. Babu alitusimulia hadithi nzuri.
4. Sikukuu ya Krismasi iliadhimishwa kwa sherehe kubwa.
5. Manzi alinunua vitabu na kalamu.

### Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi kwa kutumia vitenzi vya silabi moja vifuatavyo katika wakati uliopita hali kanushi.*

**Kwa mfano:** kuja

**Jibu:** Mwalimu hakuja shuleni jana.

1. kunywa
2. kula
3. kuwa
4. kuja
5. kufa

### Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tajeni majina ya alama za uandishi zifuatazo kisha mtunge sentensi moja kwa kila alama.*

**Kwa mfano:** .

**Jibu:** ***Nukta***

**Sentensi:** *Tutaadhimisha sikukuu ya Ukombozi mwezi Julai*.

1. ?
2. !
3. ,
4. :
5. ( )
6. ’

### Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, wasimulie wenzako kuhusu sikukuu yoyote mliyoadhimisha kwa kuzingatia wakati uliopita.*

### Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo katika hali yakinishi na hali kanushi kwa kuzingatia wakati ujao.*

**Kwa mfano:** andika

**Jibu:** ***(Yakinishi):*** Mwanafunzi ataandika ubaoni.

***(Kanushi):*** Mwanafunzi hataandika ubaoni.

1. sherehekea
2. kula
3. adhimisha
4. kunywa
5. soma

### Zoezi la 8

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, rekebisheni kifungu hiki kwa kutumia alama za uandishi pamoja na herufi kubwa kwa usahihi.*

sikukuu ya mwaka mpya huadhimishwa tarehe moja januari siku ya mashujaa huadhimishwa tarehe moja mwezi februari je wewe uliadhimisha sikukuu ya mwaka mpya kwa njia gani waislamu wana sherehe mbili kuu ambazo ni idi ul fitri pamoja na idi ul adha Wakristo vilevile wana sherehe mbili kuu ambazo ni krismasi pamoja na pasaka je wewe husherehekea sikukuu gani ya kidini

### Zoezi la 9

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, rekebisheni sentensi hizi kwa kutumia alama za uandishi pamoja na herufi kubwa kwa usahihi.*

1. *rais aliongoza sherehe ya siku ya uhuru katika uwanja wa gikondo*
2. *je wewe ulihudhuria sherehe ya umuganura mwaka jana*
3. *lo sikujua unaweza kuimba vizuri hivyo kwenye sherehe hiyo*

## Faharasa

**sikukuu:** siku yenye shamrashamra ya kuadhimisha tukio fulani kama vile: *Krismasi, Idi ul Fitri, Siku ya Uhuru* n.k.

**sherehe:** shamrashamra zinazofanywa ili kuadhimisha tukio fulani kama vile: *harusi*, *unyago* n.k; ***tamasha***

**sherehekea:** burudika kwa kula, kunywa na kucheza densi kwenye shughuli ya furaha

**adhimisha:** fanya shughuli za kufurahia siku kwa kukumbuka na kuheshimu tukio muhimu linalohusika

**maarufu:** -enye kujulikana sana, -enye kufahamika sana mahali pengi; ***mashuhuri***

**uhuru:** hali ya kuishi bila kutawaliwa na mtu au nchi nyingine

**ukombozi:** matendo au vita vya kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge

**unyonge:** hali ya kutokuwa na nguvu, hali ya kuwa na udhaifu

**shujaa:** mtu mwenye ujasiri, mtu awezaye kukabili jambo la hatari bila woga

**siasa:** shughuli za serikali za kuendeleza maisha ya wananchi

**kalenda:** kifaa kitumikacho kuonyesha idadi ya siku, wiki na miezi kwenye karatasi au kitambaa, simu za mkononi, saa au kompyuta

**rasmi:** inayofuata utaratibu na sheria zilizowekwa

**kukomboa:** kutoa mtu katika hali ya kukandamizwa, kudhulumiwa au kutawaliwa na mtu mwingine

**tukio:** jambo lililofanyika au kutokea; ***tokeo***

**serikali:** mfumo au chombo chenye mamlaka ya kutawala nchi au eneo fulani

**thamani:** ubora wa kitu kutokana na hali yake na umuhimu wake katika jamii

**mkristo:** mtu anayefuata mwongozo wa Yesu Kristo

**kimbari:** kutenga watu ukitumia rangi, kabila, dini, taifa n.k.

**utawala:** namna au matendo ya kuendesha shughuli za kutawala za serikali

**wakoloni:** watu wa taifa la kigeni wanaotawala nchi nyingine kwa niaba ya nchi yake

# SURA YA TATU

## MADA KUU 3: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

**Mada Ndogo:** **Midahalo na mijadala kuhusu shughuli za maendeleo na uzalishajimali dhidi ya umaskini nchini**

### SOMO LA 10: Mdahalo

### 10.1 Mdahalo kuhusu '*Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi kuliko biashara*'

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mchoro ufuatao kisha mjadili kuhusu kinachoendelea katika mchoro wenyewe. Baada ya kujadiliana, someni kifungu cha mdahalo kinachofuata kisha mjibu maswali yanayofuata.*



**Mwenyekiti:** Mabibi na mabwana, ndugu wasemaji na wasikilizaji hamjambo! Mada yetu ya mdahalo wa leo ni: "*Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi kuliko biashara*". Ningependa kuwakumbusha kuwa kila mzungumzaji atapewa muda wa kutoa hoja zake. Vilevile, muda uliopangwa wa kutoa hoja utazingatiwa. Kwa sasa, ningependa kumkaribisha Bwana Bigirimana ambaye ndiye

| | |
|---|---|
| | msemaji mkuu wa kwanza wa upande wa watetezi ili atoe hoja zake. |
| **Bigirimana:** | Asante Mwenyekiti. Ni dhahiri kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo ya wananchi. Watu wameelimishwa ili waweze kuwa na uelewa wa mahitaji ya jamii zao na hatimaye kubuni mikakati ya kuanzisha miradi ya kuboresha na kuendeleza maisha yao. Kupitia elimu, tumeweza kupata teknolojia ya kuboresha maisha yetu. Asante Mwenyekiti. |
| **Mwenyekiti:** | Asante Bigirimana. Ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa upande wa upinzani Binti Mukamwiza ili naye atoe hoja zake. |
| **Mukamwiza:** | Asante Mwenyekiti. Mimi sikubaliani kabisa na maoni ya msemaji ambaye amenitangulia kuwa tuko nyuma kimaendeleo kwa sababu ya ukosefu wa walioelimika ila ni kwa kuwa biashara katika nchi zetu ni chache. Biashara zinafaa zikuzwe kwa kiwango cha kimataifa ambapo tutaweza kuwa na mauzo yenye kutuletea pesa nyingi za kigeni. Pesa hizo ndizo zinazotumiwa katika miradi mingi ya kimaendeleo nchini. Asante sana mwenyekiti. |
| **Mwenyekiti:** | Kwa sasa, ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa pili ili naye atoe hoja zao. Karibu Mukandayisenga kutoka katika upande wa utetezi. |
| **Mukandayisenga:** | Asante Mwenyekiti. Mtu ambaye ameelimika anaweza kufanya mambo mengi kwa njia bora kuliko mtu asiyeelimika. Wapinzani wanasema kwamba ni bora biashara ziwe nyingi ili tuweze kujipatia pesa nyingi kutokana na biashara hizo lakini lazima ifahamike kuwa biashara hizi hupangwa na watu walioelimika. Kwa kweli, elimu ni muhimu kuliko biashara kwani bila elimu biashara haiwezi kufanyika vyema. Asante Mwenyekiti. |

**Mwenyekiti:** Asante sana Mukandayisenga. Ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa pili kutoka upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake. Karibu sana Bwana Muhirwa.

**Muhirwa:** Asante Mwenyekiti. Ili nchi iendelee inahitaji pesa za kujenga shule, kulipa walimu, kulipia mahitaji muhimu katika sekta ya elimu, n.k. Bila biashara, pesa hizo zitatoka wapi? Mimi naona kwamba jambo la msingi katika maendeleo ya nchi ni biashara. Asante Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Sasa nitawapa fursa wasikilizaji washiriki ili watoe mchango wao kuhusu mada yetu.

**Msikilizaji mshiriki 1:** Bwana mwenyekiti, naona kwamba mawazo yote yaliyotolewa kutoka pande zote mbili ni mazuri. Lakini, ninafikiria kwamba elimu na biashara yote ni mambo muhimu ya kuboresha uchumi wa nchi yetu. Bila elimu hatuwezi kuwazia miradi ya biashara na namna ya kuiendeleza na kuidumisha ili iweze kutuletea mafanikio. Asante mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Naona kuna binti mmoja pale ambaye naye anataka kutoa hoja zake. Karibu binti.

**Msikilizaji mshiriki 2:** Mimi sikubaliani kabisa na maoni ya msemaji ambaye amenitangulia. Hatuwezi kuweka kwa kiwango kimoja nafasi ya elimu na ya biashara katika kuendeleza nchi yetu. Ni lazima tuelewe kwamba elimu ndiyo ya kwanza na baadaye mambo mengine hufuata. Asante Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asanteni sana wasemaji, wasikilizaji na washiriki wote, naona kuwa watu wengi wangependa kutoa maoni mengine lakini muda hauturuhusu kwa sasa. Naomba tukamilishie mdahalo wetu hapa kisha tutauendeleza kesho inshallah. Asanteni nyote kwa kushiriki.

## Maswali ya ufahamu

1. Mada ya mdahalo iliyokuwa ikizungumziwa ilikuwa ipi?
2. Eleza tofauti kati ya watetezi na wapinzani.
3. Bigirimana alitoa hoja zipi?
4. Mukamwiza alitoa hoja zipi?
5. Mukandayisenga alitoa hoja gani?
6. Eleza hoja ambazo Msikilizaji mshiriki 1 alitoa.
7. Msikilizaji mshiriki 2 alitoa hoja zipi?
8. Taja jina jingine la 'mdahalo'.
9. Mwenyekiti hufanya kazi gani katika shughuli za mdahalo?

## 10.2 Msamiati kuhusu mdahalo

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha mazungumzo yaliyotangulia na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 10.1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo.*

1. Alitupatia ***fursa*** ya kueleza shughuli za maendeleo ya kijiji chetu.
2. Mukeshimana alitoa ***hoja*** nzuri katika mazungumzo yetu.
3. Sisi ***tulitetea*** mawazo yake kwa sababu alisema ukweli.
4. Mimi ***ninapinga*** mawazo ya watu wanaotaka kuendelea kuishi kwa kutegemea misaada tu.
5. Nyirahabineza alichaguliwa kuwa ***mwenyekiti*** wa Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda (CHAWAKIRWA).
6. Wageni hawa walikuja ***kuwekeza*** nchini mwetu na wanaendelea kupata faida nyingi.
7. Mafunzo ya rafiki yangu yalichukua ***gharama*** kubwa.
8. ***Matokeo*** ya mtihani wetu ni mazuri kwa sababu tumefaulu.
9. Tujiepushe na ulevi kwa sababu ni ***kikwazo*** kwa maisha mazuri ya watu.
10. Tulianzisha biashara ya kufuga kondoo na ***pato*** letu linaongezeka kila mwaka.

### Zoezi la 10.2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, kamilisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:* ***walipiga makofi, maarifa, mshiriki, kutambua, itatunufaisha, anafananisha.***

**Kwa mfano:** Baada ya ____________ kuwa Bwiza hakufaulu katika somo la Kiswahili niliamua kumsaidia.

**Jibu:** Baada ya ***kutambua*** kuwa Bwiza hakufaulu katika somo la Kiswahili niliamua kumsaidia.

1. Watu hawa wana ____________ mbalimbali ya kutekeleza miradi.
2. Washiriki wote wa mkutano ____________ baada ya kusikia hoja nzuri za Kayisabe na wenzake.
3. Mwenyekiti wa mkutano wetu anasema kuwa kila ____________ anapaswa kutoa hoja zake.
4. Mtu huyu ____________ elimu na utajiri.
5. Kazi hii ____________ wote kwa kutuwezesha kupata pesa za kujisaidia.

### Zoezi la 10.3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni maneno yaliyoandikwa katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B.*

**Kwa mfano:** **1** ⟶ **C**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. mwenyekiti | A. mazungumzo kati ya watu wenye mitazamo tofauti |
| 2. mdahalo | B. jambo muhimu |
| 3. msingi | CH. mtu aliyechaguliwa kuongoza mdahalo |
| 4. wanatatua | D. ufupisho |
| 5. muhtasari | E. wanaondoa tatizo |

## 10.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini maswali yafuatayo na mwelezane kuhusu:*

1. Mdahalo ni nini?
2. Toa mifano ya mada mbili zinazoweza kuzungumziwa katika mdahalo.
3. Ni watu gani ambao hushirikishwa katika mdahalo?
4. Watu hao huwa na mawazo au misimamo tofauti. Eleza misimamo hiyo.
5. Taja tabia za kujiepusha katika mdahalo.

## Zoezi la 10.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni herufi zilizoachwa ili kuunda neno kamili.*

**Kwa mfano:**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | | U | N | G | | M | | O |

**Jibu:**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | **Z** | U | N | G | **U** | M | **Z** | O |

1.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | I | N | | A | N | |

2.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | S | | I | R | I | | I |

3.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | I | K | I | | I | Z | A | | I |

4.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | A | H | | L | |

### Maelezo muhimu!

- Mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mitazamo tofauti huitwa ***mdahalo***.
  - Mtazamo wa kwanza hutoa hoja zinazotetea au kuunga mkono wazo kuu.
  - Mtazamo wa pili hutoa hoja za kupinga au kukataa wazo kuu.
- Washiriki wa mdahalo ni:

**1. Mwenyekiti:**

- Huongoza mazungumzo au majadiliano.
- Hupanga muda utakaotumiwa na kila msemaji kutoa hoja.
- Huchagua wasemaji katika mdahalo.
- Hupigisha kura baada ya mazungumzo ili kutaka kujua upande ulioshinda kati ya upande wa watetezi na ule wa wapinzani.

**2. Katibu:**

- Huandika na kusoma hoja za wasemaji wote.
- Hutangaza matokeo ya kura zilizopigwa baada ya mazungumzo.

**3. Watetezi:**

- Hawa ni wasemaji wanaotetea mada au wazo kuu linalozungumziwa.

**4. Wapinzani:**

- Hawa ni wasemaji wanaopinga mawazo yanayotetea wazo kuu la mada.

**5. Wasikilizaji washiriki:**

- Hawa wanashiriki kwa kusikiliza hoja za pande mbili: upande wa utetezi na upande wa upinzani.

Baadhi ya ***tabia za kuepuka*** katika mdahalo ni: *matumizi ya lugha yenye matusi na uchochezi, kutohifadhi wakati uliotengewa, kupandwa na hasira upande wako unaposhindwa,* n.k.

## 10.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kuandaa mdahalo

*Katika makundi ya wanafunzi wanane wanane chagueni moja kati ya mada zifuatazo kisha mwandae mdahalo wenu.*

1. Elimu ndio msingi wa maisha mazuri.
2. Wazazi wana nafasi kubwa katika malezi ya watoto wao kuliko walimu.
3. Ni lazima viongozi wa kidini washirikiane na wanasiasa katika mipango ya maendeleo ya wananchi.
4. Vitabu ndivyo vifaa muhimu katika elimu.

**Katika maandalizi yenu, zingatieni mambo yafuatayo:**

- Jadilini maana ya msamiati uliotumiwa katika mada mlizopewa ili muweze kuelewa mada hizo.
- Hakikisheni kuwa mnaelewa jambo muhimu linalozungumziwa katika kila mada.
- Hakikisheni kuwa mmechagua mwenyekiti, katibu, wasikilizaji washiriki, watetezi na wapinzani.
- Kila mzungumzaji aandae na kupanga hoja zake vizuri.
- Kila mzungumzaji anapaswa kuwa na nidhamu kwa kuheshimu maelekezo ya mwenyekiti.

## 10.5 Sarufi: Wakati uliotimilika, tungo yakinishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zinazofuata katika umoja na wingi kisha mwelezane ugunduzi wenu na baadaye mjibu zoezi linalofuata.*

| Umoja/ Tungo yakinishi | Wingi/ Tungo yakinishi |
|---|---|
| **Mimi** ni***me***toa hoja zangu. | **Sisi** tu***me***toa hoja zetu. |
| **Wewe** u***me***toa hoja zako. | **Nyinyi** m***me***toa hoja zenu. |
| **Yeye** a***me***toa hoja zake. | **Wao** wa***me***toa hoja zao. |

*Je, mmegundua nini?*

### Zoezi la 10.5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi moja moja kwa kutumia kitenzi **zungumza** kwa kutumia kiambishi '**me**' kama kilivyotumiwa katika tungo zenye kitenzi **toa** zilizo hapo juu. Tumia nafsi: mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi na wao.*

**Kwa mfano:**

***Mimi*** *ni**mezungumza** na mwalimu wangu.*
***Sisi*** *tu**mezungumza** na walimu wetu.*

### Maelezo muhimu!

- Kiambishi ***'me'*** kinarudiwarudiwa katika vitenzi vyote baada ya viambishi nafsi ***ni, u, a, tu, m*** na ***wa***. Kiambishi ***'me'*** ni kiambishi cha ***wakati uliotimilika, tungo yakinishi***.
- Wakati uliotimilika huonyesha kuwa tendo tayari limefanyika na kumalizika.
  **Kwa mfano:**
  - Mimi *ni**me**fanya* zoezi langu. (zoezi tayari limeshafanywa)
  - Kageruka *a**me**ondoka* leo. (tendo la kuondoka tayari limeshamalizika)

## Matumizi ya wakati uliotimilika katika sentensi


*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kwa kuziambatisha pamoja na michoro iliyopo. Elezaneni mlichogundua.*




1. Mama a***me***pika wali.



2. Kaka yangu a***me***lala.



3. Mwalimu a***me***simama mbele ya wanafunzi.



4. Gatete a***me***keti kwenye stuli.



5. Gasimba a***me***jua kuandika.

## Zoezi la 10.6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kitenzi kinachofaa katika wakati uliotimilika, tungo yakinishi.*

**Kwa mfano:** Mwalimu ______ (kueleza) vizuri mambo yote muhimu.

**Jibu:** Mwalimu ***ameeleza*** vizuri mambo yote muhimu.

1. Sisi na viongozi wetu __________(kujadiliana) kuhusu umuhimu wa Kiswahili.
2. Wewe _________ (kutazama) mchezo wa kandanda kwenye runinga.
3. Mama yangu _________ (kuagiza) bidhaa nyingi kutoka Uchina.
4. Mtetezi huyu na wasikilizaji washiriki wote__________(kuzungumzia) mambo muhimu.
5. Mlango wa nyumba hii _________ (kufunguliwa) ili wageni wote waingie.
6. Kisu changu __________ (kupotea).
7. Nyumba zile ________ (kupakwa) rangi na mafundi wawili.
8. Vitabu vingi vya Kiswahili _________ (kuchapishwa).
9. Midahalo miwili __________ (kushirikisha) wasemaji wenye hoja nzuri.
10. Mimi __________ (kuimba) wimbo wa kumsifu Mungu katika ibada yetu.

### 10.5.1 Wakati uliotimilika, tungo kanushi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zinazofuata katika umoja na wingi kisha mtunge sentensi zinazofanana nazo katika nafsi zote.*

| Tungo yakinishi | | Tungo kanushi |
|---|---|---|
| **Umoja** | ***Mimi*** ni***me***fika asubuhi. | ***Mimi*** si***ja***fika asubuhi. |
| | ***Wewe*** u***me***fika asubuhi. | ***Wewe*** hu***ja***fika asubuhi. |
| | ***Yeye*** a***me***fika asubuhi. | ***Yeye*** ha***ja***fika asubuhi. |
| **Wingi** | ***Sisi*** tu***me***fika asubuhi. | ***Sisi*** hatu***ja***fika asubuhi. |
| | ***Nyinyi*** m***me***fika asubuhi. | ***Nyinyi*** ham***ja***fika asubuhi. |
| | ***Wao*** wa***me***fika asubuhi. | ***Wao*** hawa***ja***fika asubuhi. |

### Zoezi la 10.7

a) *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi moja moja kwa kutumia kitenzi* ***imba*** *katika wakati uliotimilika, hali yakinishi. Tumia nafsi:* ***mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi*** *na* ***wao.***

b) *Andikeni sentensi zenu katika hali kanushi.*

### Maelezo muhimu!

- Kiambishi ***'me'*** *kimetumika ku*onyesha ***wakati uliotimilika katika tungo yakinishi.***
- Katika wakati uliotimilika, kiambishi ***'ja'*** kinatumiwa katika tungo kanushi badala ya kiambishi ***'me'*** cha tungo yakinishi.

### Zoezi la 10.8

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi hizi katika tungo kanushi.*

**Kwa mfano:** Wewe umeimba wimbo mzuri sana.

**Jibu:** Wewe ***hujaimba*** wimbo mzuri sana.

1. Yeye ameagiza bidhaa nyingi kutoka Kigali.
2. Mimi nimezunguka mjini kwa gari.
3. Mtoto wangu amefaulu mitihani yake.
4. Nyumba yangu imesafishwa.
5. Mgomba umechomwa.

### Zoezi la 10.9

*Baada ya kukanusha tungo katika zoezi la 10.8, ziandike katika wingi.*

**Kwa mfano:** Wewe ***hujaimba*** wimbo mzuri sana. (umoja, tungo kanushi)

**Jibu:** Nyinyi hamjaimba nyimbo nzuri sana. (wingi, tungo kanushi)

## SOMO LA 11: Mjadala

### 11.1 Mjadala kuhusu '*Nafasi ya ukulima katika uzalishajimali dhidi ya umaskini*'

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu kinachoendelea katika michoro ifuatayo kisha msome kifungu cha mjadala kinachofuata kuhusu nafasi ya kilimo katika shughuli za uzalishajimali dhidi ya umaskini na hapo baadaye mjibu maswali yanayofuata.*





**Mwenyekiti:** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliofika hapa leo hamjambo! Mada ya mjadala wetu wa leo inahusu nafasi ya ukulima na ufugaji katika uzalishaji mali. Nyinyi nyote ni wataalamu katika sekta hizi mbili ambazo ni nguzo ya uzalishajimali na upiganaji dhidi ya umaskini nchini mwetu. Bila kupoteza muda ningependa kumkaribisha Kawera atoe hoja zake kuhusu mada yetu.

**Kawera:** Asante sana mwenyekiti. Mimi nafikiri kwamba ukulima tunaohitaji ni wa kisasa. Tatizo lililopo ni kwamba kila mkulima anataka kupanda mimea yake mwenyewe katika shamba lake dogo. Serikali yetu inapaswa kuwaelekeza wakulima namna ya kuweka mashamba yao pamoja na kupanda zao moja katika mashamba hayo yote. Hili likizingatiwa, nafikiri kwamba umaskini tutaupiga kisogo.

**Mwenyekiti:** Asante Kawera kwa mawazo yako. Ningependa kumkaribisha Bagirishya naye aseme jambo. Karibu.

**Bagirishya:** Asante sana Mwenyekiti. Kwa kweli, ni vyema wakulima wetu waelewe umuhimu wa kujiweka pamoja kama wanavyosema waswahili 'umoja ni nguvu'. Mashamba hayo yakiunganishwa na kupandwa mimea sawa, mavuno yatakuwa mengi na wakulima wetu wataweza kupata soko na kuuza mazao yao kwa wingi. Vilevile, wanahitaji kutumia mbegu zilizofanyiwa majaribio na taasisi ya kilimo. Pia, taasisi hii ihakikishe kwamba imewapa wakulima mbolea nzuri kwa bei nafuu. Asanteni.

**Mwenyekiti:** Asante sana Bagirishya kwa maoni yako. Tumkaribishe Mukandayisenga.

**Mukandayisenga:** Asante sana mwenyekiti. Mimi nafikiri umaskini unatokana na uvivu wa baadhi ya watu. Kuna watu wanaotaka kula lakini ukichunguza vizuri unakuta kwamba hawataki kufanya kazi. Ni lazima kila mtu aelewe kwamba kazi ndiyo msingi wa maisha mazuri. Kuunganisha mashamba na kupanda mazao sawa hakuwezi kuleta mafanikio iwapo watu hao hawana bidii katika shughuli hii. Asante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Nawashukuru sana kwa mchango wenu kwa kuonyesha nafasi ya ukulima na ufugaji katika njia za uzalishaji mali dhidi ya umaskini. Ni kweli kwamba kila mtu akitimiza wajibu wake nchi yetu itaweza kuwa tajiri, kupata chakula cha kutosha kwa wananchi na hata kubakiza chakula cha kuuza nje ya nchi yetu kiasi cha kukuza uchumi wetu. Nawashukuru tena kwa mawazo yenu mazuri. Mdahalo mwingine utafanyika wiki ijayo siku na saa kama hii ya leo. Asanteni na karibu tena.

## Maswali ya ufahamu

1. Mada ya mjadala ilikuwa ipi?
2. Eleza tofauti kati ya ukulima na ufugaji.
3. Tatizo linaloathiri kilimo kulingana na Kawera ni lipi?
4. Serikali inashauriwa kufanya nini ili kusuluhisha matatizo ya kilimo?
5. Bagirishya alitoa hoja gani?
6. Mukandayisenga alitoa hoja gani?
7. Eleza hitimisho ambalo Mwenyekiti alitoa.

## 11.2 Msamiati kuhusu ukulima

*Jipangeni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, kisha mtafute maana ya msamiati mpya katika kifungu cha mjadala kilichotangulia. Tafuteni maana ya msamiati huo kulingana na matumizi yake katika kifungu hicho. Tumieni kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 11.1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi zenu kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.*

1. Taasisi ya kilimo imewaletea wakulima ***mbegu*** nzuri za mahindi.
2. Nyanya na vitunguu vinanunuliwa kwa ***bei nafuu*** mjini Kigali.
3. Ni lazima kila mkulima aache ***uvivu*** na kufanya kazi kwa bidii.
4. ***Mtaalamu*** mmoja wa kilimo ameonyesha namna nzuri ya kupanda migomba.
5. Mkulima huyu ana ***bidii*** sana katika shughuli zake.
6. Watu hawa wanatimiza ***wajibu*** wao wa kufundisha wakulima.
7. ***Wadau*** wote wa kilimo wamekutania mjini Kigali.
8. Serikali ya Rwanda inatenga faranga nyingi za kuendesha ***sekta*** za kilimo na ufugaji.

### Zoezi la 11.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tumieni mshale kwa kuhusisha maneno katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B.*

| | |
|---|---|
| 1. mavuno → | A. jambo ambalo huzungumziwa na kujadiliwa |
| 2. mjadala | B. mazungumzo yanayohusu mada mahususi ambayo hufanywa kwa kujenga hoja |
| 3. zao | CH. mazao yanayozalishwa shambani; kitu ambacho mtu hupata kama matokeo ya jambo alilofanya |
| 4. taasisi | D. chombo cha kitaaluma kinachotoa mafunzo au kufanya uchunguzi wa mambo mbalimbali |
| 5. mada | E. kinachotokana na mmea; mmea unaotokana na mbegu |

(Mfano: 1. mavuno → CH.)

## 11.3 Matumizi ya lugha: Zoezi la jedwali

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jazeni nafasi hizi kwa kuzingatia majibu ya maelezo yaliyo hapo chini:*

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1/2 | | 3 | | | 4 | | ■ | ■ | ■ | 5 |
| | ■ | | ■ | ■ | | ■ | 6/7 | | | |
| 8 | | | ■ | ■ | | ■ | | ■ | ■ | |
| | ■ | 9 | | ■ | 10 | | | | ■ | |
| ■ | ■ | | ■ | ■ | | ■ | | ■ | ■ | |
| 11 | | | | ■ | ■ | 12 | | | ■ | |
| ■ | ■ | | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | 13 | ■ |
| 14 | | | | 15 | | | | ■ | | ■ |
| ■ | ■ | ■ | ■ | | ■ | ■ | ■ | ■ | | ■ |
| 16 | | | | | | | ■ | ■ | | ■ |

### Kwenda kulia

1 Mazungumzo kati ya watu wenye mitazamo tofauti kuhusu mada maalumu
6 Uchaguzi wa kupata mshindi
8 Maombi yanayoelekezwa kwa Mungu
9 Neno lionyeshalo kuwa hakuna kingine
10 Maelezo ya kupinga au kuunga mkono
11 Kitu kilichotengenezwa kwa ajili ya kukalia
12 Kinachotokana na mmea
14 Anakataa kuunga mkono
16 Mazungumzo ya kujenga hoja yanayofanywa kwa ajili ya kufafanua jambo

### Kwenda chini

2 Jambo linalozungumzwa au kujadiliwa
3 Anaunga mkono
4 Chombo cha mawasiliano
5 Mtu anayeandika mawazo ya wasemaji na washiriki wengine katika mdahalo
7 Kuwa kwa wingi
13 Kitu anachopata mtu baada ya kazi
15 Isipokuwa

### Maelezo muhimu!

- ***Mjadala*** ni mazungumzo kuhusu jambo maalum.
- Watu wanaoshiriki katika mazungumzo haya hutoa ***hoja*** zao kuhusu jambo hilo.
- Jambo ambalo linazungumziwa huhitaji kufafanuliwa na kutolewa maelezo.
- Katika mjadala kila mtu aliye na hoja huonyesha kuwa anataka kusema na hupewa muda wake ili atoe hoja zake.
- Msemaji anaweza kutetea au kupinga mawazo ya wengine.
- Katika mjadala kuna kiongozi anayeongoza mazungumzo.
- Kiongozi huchagua anayezungumza na kuongoza mazungumzo na kuhifadhi nidhamu.
- Washiriki nao hutoa hoja zao kuhusu mada iliyotolewa mpaka wafikie uamuzi wao wa mwisho.
- Hakuna kura zinazopigwa kama ilivyo katika mdahalo.

## 11.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kuandaa mjadala

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, chagueni moja kati ya mada zifuatazo na kuandaa mdahalo wenu.*

1. Umuhimu wa biashara katika uzalishajimali nchini Rwanda.
2. Umuhimu wa uongozi bora katika uzalishajimali dhidi ya umaskini.
3. Vikwazo vya kufanikisha kazi miongoni mwa vijana.
4. Nafasi ya shule za ufundi katika maendeleo na uzalishajimali nchini Rwanda.

## 11.5 Sarufi: Kauli asili na kauli taarifa

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mjibu maswali yaliyo hapo chini.*

| Sentensi A | Sentensi B |
|---|---|
| 1. “Kila mshiriki atapewa muda wa kutoa hoja zake.” Mwenyekiti anasema. | 1. Mwenyekiti anasema kuwa kila mshiriki angepewa muda wa kutoa hoja zake. |

| | |
|---|---|
| 2. "Mimi sikubaliani na msemaji wa kwanza." Msikilizaji mshiriki anasema. | 2. Msikilizaji mshiriki anasema kwamba yeye hakubaliani na msemaji wa kwanza. |
| 3. "Sisi tunaunga mkono mawazo ya upande wa utetezi." Wasikilizaji washiriki hawa wanasema. | 3. Wasikilizaji washiriki hao wanasema kwamba wao wanaunga mkono mawazo ya upande wa utetezi. |

*Je, mmegundua nini?*

**Zoezi la makundi**

1. *Linganisheni sentensi katika sehemu A na sentensi katika sehemu B kwa kuonyesha sifa zake.*
2. *Tungeni sentensi mbili zenye sifa kama za sentensi za sehemu A na kuziandika kwa kuzingatia sifa za sentensi katika sehemu B.*

## Maelezo muhimu!

- Sentensi katika kundi A zinarudia maneno yaliyotamkwa na mtu bila kubadilisha chochote katika kauli yake.
- Kauli hiyo imeandikwa kwa kutumia alama za usemi (**" "**) na kuanza kwa herufi kubwa.

**Kwa mfano:** *Mwalimu alisema, "Mimi nitafundisha somo la Kiswahili."*

- Sentensi katika kundi B zinalenga kutuambia maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine bila kuyarudia kama yalivyokuwa katika kauli yake ya kwanza.

**Kwa mfano:** *Mwalimu alisema kwamba yeye atafundisha somo la Kiswahili.*

- Sentensi katika kundi A zinaonyesha kauli ya mtu katika hali yake ya kwanza na kauli hiyo inaitwa ***kauli asili.***
- Sentensi katika kundi B zinatoa taarifa au habari ya kauli au maneno yaliyosemwa na mtu mwingine bila kuongeza wala kupunguza maana ya jambo aliloeleza. Kauli hiyo inaitwa ***kauli taarifa.***
- Katika kauli ya taarifa mambo haya huzingatiwa:
  - ***Nafsi hubadilika***
    - ***Mimi*** hubadilika na kuwa ***yeye***
    - ***Sisi*** hubadilika na kuwa ***wao***

## Zoezi la 11.3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, badilisheni sentensi hizi za kauli asili ziwe katika kauli taarifa.*

**Kwa mfano:** Mkulima mmoja anasema, “Mimi nitapata mavuno mengi sana.”

**Jibu:** Mkulima mmoja anasema kwamba yeye atapata mavuno mengi sana.

1. Wazungumzaji hawa wanasema, “Sisi tunapenda kutoa maoni yetu.”
2. “Kabera atajijengea nyumba nzuri.” Mwanafunzi mmoja anasema.
3. “Mimi nitaingia darasani saa nane kamili.” Ndayisaba anasema.
4. Wakulima wanasema, “Mvua itanyesha na mimea yetu itastawi.”
5. Baba yangu anasema, “Ni lazima watoto wote wasome kwa bidii.”
6. “Sisi tutasaidia wakulima wetu kupata mbegu nzuri.” Mkuu wa wilaya anasema.
7. “Mimi ninahitaji dereva mwenye ujuzi.”Mkuu wa kiwanda hiki anasema.
8. Mama yangu anasema, “Kisu changu kimepotea.”
9. “Kitanda changu ni kizuri.” Mgeni mmoja anasema.
10. “Mimi sikubaliani na mawazo ya mtetezi wa pili.” Mpinzani huyu anasema.

## Zoezi la 11.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, badilisheni sentensi hizi kutoka kauli taarifa na kuziweka katika kauli asili.*

**Kwa mfano:** Mama alisema kuwa alitaka kwenda sokoni.

**Jibu:** “Ninataka kwenda sokoni.” Mama alisema.

1. Baba aliniambia kuwa nikifika Kigali ninunue sare mpya.
2. Kaka alisema kuwa hakutaka kwenda shambani.
3. Mwalimu alisema aende hapo.
4. Kalisa alisema kuwa yeye aliandika barua hiyo.
5. Birasa alishangaa kuwa yeye hawezi kubeba mzigo huo.
6. Mwalimu mkuu aliuliza sababu yake ya kulia.

**SOMO LA 12: Mjadala**

## 12.1 Mjadala kuhusu '*Ufugaji kama njia ya kupigana na umaskini nchini*'

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni na mjadili kuhusu kinachoendelea katika michoro hii kisha msome kifungu kilicho hapo chini na baadaye mjibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*







**Mwenyekiti:** Mabibi na mabwana mliokuja hapa leo hamjambo! Mjadala wetu wa leo unahusu nafasi na umuhimu wa ufugaji katika shughuli za uzalishaji mali nchini mwetu. Nafikiri kwamba kila mtu anaweza kutoa mchango wake kwa kudhihirisha jinsi ufugaji unavyoweza kuwa njia ya kujiendeleza na kuboresha maisha yetu dhidi ya umaskini. Ningependa kumkaribisha Bwana Niyibizi atoe maoni yake kuhusu mada yetu.

**Niyibizi:** Asante sana Mwenyekiti. Ni kweli kabisa kuwa ufugaji ni muhimu sana katika kuboresha maisha yetu. Afya ya miili yetu itaboreka kutokana na maziwa, nyama na hata mafuta yanayotoka kwa mifugo yetu. Kutokana na haya, miili yetu itakuwa na nguvu na uwezo wa kupambana na magonjwa mbalimbali. Mifugo pia humsaidia mfugaji kupata pesa za kutimizia mahitaji mengine. Asante Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Bwana Niyibizi. Namkaribisha Nyiraneza achangie katika mada ya leo.

**Nyiraneza:** Asante sana Mwenyekiti kwa fursa hii. Ufugaji una nafasi kubwa kabisa katika maisha yetu. Mtu anapopatwa na

uhaba wa fedha anaweza kuuza mnyama mmoja akatatua shida yake. Mambo mengine mengi huweza kutekelezwa kutokana na mapato ya ufugaji. Asante sana Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Binti Nyiraneza kwa mawazo yako mazuri. Nafasi kwako Bi Muhirwa.

**Muhirwa:** Asante sana Mwenyekiti. Kama tunavyojua, nchi yetu haina maeneo makubwa ya kutengea shughuli za ufugaji pekee bali pia shughuli nyingine kama vile: shughuli za viwanda, kilimo, na hata biashara za aina mbalimbali. Mifugo michache iliyopo haiwezi kutatua shida za wafugaji. Ni vyema kutilia mkazo shughuli nyingine za kuzalisha mali kama vile: biashara, ujenzi, viwanda na kadhalika kwa sababu shughuli hizi ndizo zinazoweza kuleta pesa nyingi na kuwapa kazi watu wengi zaidi kuliko ufugaji. Asante sana Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Bi Muhirwa kwa mchango wako. Karibu Bwana Rwambibi.

**Rwambibi:** Asante sana Mwenyekiti. Ufugaji ni muhimu sana kwani ndio unaofanya kilimo kuwa bora. Ufugaji huleta rutuba inayotumiwa katika mashamba yetu na kustawisha mimea. Vilevile, katika ufugaji wa leo, watu wanafuga ng'ombe wa kisasa wenye kuleta maziwa mengi ambayo huwa na mapato mengi yanapouzwa. Zaidi ya hayo, viwanda navyo vinahitaji malighafi ili kutengeneza vyakula, vinywaji, mafuta, nguo na kadhalika. Malighafi hiyo hupatikana kutokana na ufugaji au kilimo. Ufugaji ni shughuli muhimu sana katika kupigana na umaskini na kuboresha maisha yetu. Asante sana Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asanteni washiriki wote katika mjadala wetu. Nawashukuru tena kwa maoni yenu mliyotoa kuhusu mada ya mjadala wa leo. Bila shaka, kila mtu ameweza kuelewa umuhimu wa ufugaji na jinsi ambavyo unaweza kuchangia katika kupigana na umaskini ili kutuwezesha kuwa na maisha mazuri. Asanteni nyinyi nyote kwa kuweza kushiriki katika mjadala wetu.

## Maswali ya ufahamu

1. Mjadala uliosoma ulihusu nini?
2. Bwana Niyibizi alitoa maoni gani kuhusiana na mada husika?
3. Nyiraneza alichangia mjadala kwa hoja zipi?
4. Muhirwa alitoa hoja zipi kuhusiana na umuhimu wa ufugaji?
5. Eleza hoja alizotoa Bwana Rwambibi.
6. Mwenyekiti alihitimisha vipi mjadala huu?

## 12.2 Msamiati wa mjadala kuhusu ufugaji

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya katika kifungu cha mazungumzo hapo juu na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 12.1

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi zenu kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.*

1. Watoto wanapenda kunywa ***maziwa*** ya ng'ombe.
2. Ni lazima sisi ***tupambane*** na umaskini kwa kufanya kazi kwa bidii.
3. Mtoto huyu ana shida ya kukosa ***karo*** ya shule.
4. Mfugaji huyu ***ametenga*** mnyama huyu mgonjwa ili asiambukize wanyama wengine.
5. ***Kiwanda*** hiki kitafanya kazi kubwa ya kutengeneza nguo nyingi.
6. Si vizuri ***kupuuza*** ushauri wa viongozi wetu.
7. Mzungumzaji huyu ***amegusia*** umuhimu wa mifugo nchini Rwanda.
8. Eneo hili lina mazao mazuri kwa sababu lina ***rutuba*** nyingi.
9. Viwanda vyetu vinahitaji ***malighafi*** nyingi kutokana na kilimo.
10. Mazungumzo yetu yamefikia ***kikomo*** kwa sasa.

### Zoezi la 12.2

*Chagueni neno kati ya yafuatayo ili kukamilisha sentensi hizi kwa usahihi:*

***mjadala, hoja, umoja, umaskini, mifugo, mbolea, maziwa***

**Kwa mfano:** Ng'ombe wanatupatia ________________ ya kuweka katika mimea yetu.

**Jibu:** Ng'ombe wanatupatia ***mbolea*** ya kuweka katika mimea yetu.

1. Wizi wa ____________ unaweza kuleta hasara kubwa kwa wafugaji na kuwarudisha katika hali ya ____________.
2. Watu wengi wanapenda kunywa _________ ili kupambana na magonjwa mbalimbali.
3. Wafugaji hawa wamejiunga katika shirika kubwa kwa sababu wanajua kwamba __________ ni nguvu.
4. ___________ wetu umetufurahisha sana kwa sababu washiriki wote walitoa _________ nzuri.

## 12.3 Matumizi ya lugha: Kuunda maneno kamili

*Katika makundi ya mawafunzi wawili wawili, jaribuni kupanga sehemu za maneno zifuatazo ili kuunda maneno kamili.*

**Kwa mfano:** zi-te-m-te

**Jibu:** mtetezi

1. da-m-lo-ha
2. ki-mwe-ti-nye
3. zu-m-ngu-ji-za-m
4. pi-u-ni-nza
5. ja-la-da-m
6. li-u-sha-ji-za li-ma
7. fu-ji-u-ga
8. ku-m-li-ma
9. o-ma-ni
10. li-ki-mo

### Zoezi la 12.3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jaribuni kupanga maneno yafuatayo ili kuunda sentensi kamili na sahihi.*

1. kazi lazima zinakwamisha za uvivu na ulevi tabia kwa sababu ni na kujiepusha mbaya.
2. ya na kazi ufugaji za kilimo zinaweza raia kupigana wengi kuwasaidia umaskini dhidi.
3. waweze bidii kazi mazuri kwa wafanya ni lazima watu ili kuwa maisha na wote.
4. hushiriki katika na wengi kwa mjadala zao kutoa mdahalo watu hoja.
5. namna kuhusu sisi maendeleo kazi umuhimu na miradi wa tunajadiliana ya kuanzisha ya.

## 12.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kuandaa mjadala

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha mwandae mjadala kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:*

1. Kazi muhimu za kuleta maendeleo kwa wananchi
2. Tabia za kujiepusha ili kufanikisha kazi.

## 12.5 Sarufi: Mabadiliko ya kauli asili na kauli taarifa

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni kwa makini sentensi zifuatazo ili muweze kujibu maswali yaliyo hapo chini:*

| Sentensi A | Sentensi B |
|---|---|
| 1. Mzazi mmoja alisema, "Watoto wangu wananisaidia katika shughuli zangu." | 1. Mzazi mmoja alisema kuwa watoto wake wanamsaidia katika shughuli zake. |
| 2. Mwalimu Mkuu alisema, "Wanafunzi wote watafanya jaribio kesho." | 2. Mwalimu Mkuu alisema kwamba wanafunzi wote wangefanya jaribio siku iliyofuata. |
| 3. Vijana wale waliuliza, "Nyinyi mnataka kuanzisha kampuni wapi?" | 3. Vijana wale waliwauliza mahali ambapo walitaka kuanzisha kampuni. |
| 4. Wafanyakazi walisema, "Leo tunafurahia matunda ya kazi yetu." | 4. Wafanyakazi walisema kwamba siku hiyo walifurahia matunda ya kazi yao. |
| 5. Kiongozi wa shirika lile alisema, "Kila mfanyakazi anapaswa kufika hapa mapema sana." | 5. Kiongozi wa shirika lile alisema kuwa kila mfanyakazi alipaswa kufika hapo mapema sana. |
| 6. Dereva aliuliza, "Nani anataka kufika mjini Kigali? " | 6. Dereva aliuliza mtu ambaye alitaka kufika mjini Kigali. |

### Zoezi la 12.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jibuni maswali yafuatayo:*

1. Linganisha sentensi katika A na sentensi katika B kwa kuonyesha sifa zake.
2. Tunga sentensi sita kwa kuzingatia sentensi katika A na kuziandika tena kwa kuzingatia sifa za sentensi katika B.

## Maelezo muhimu!

- Sentensi katika A ni za ***kauli asili*** na sentensi katika B zimeandikwa katika ***kauli taarifa***.
- Kutokana na kitenzi ***sema*** au ***uliza*** katika wakati uliopita, sentensi za kauli asili zimetanguliwa na kitenzi '*alisema*' au '*aliuliza*'.

**Kwa mfano:**

- *Wafanyakazi walisema, "Leo tunafurahia matunda ya kazi yetu."*
- *Dereva aliuliza, "Nani anataka kufika mjini Kigali?"*
- *Mwanafunzi mmoja aliuliza, "Mdahalo utafanyiwa wapi?"*

- Alama ya kuuliza (?) na alama za kufunga na kufungua (" ") huwa hazitumiwi katika kauli taarifa.

**Kwa mfano:** *Dereva aliuliza mtu ambaye alitaka kufika mjini Kigali.*

- Mambo yafuatayo hubadilika wakati wa kugeuza sentensi za kauli asili na kuziandika katika kauli taarifa:

**i) Nyakati**

Wakati uliopo ***(-na-)*** huwa wakati uliopita ***(-li-)***

Wakati ujao ***(-ta-)*** hutumia ***(-nge-)***

**ii) Vivumishi vionyeshi**

*Hapa* huwa *hapo*

*Watu hawa* huwa *watu hao*

*Kitu hiki* huwa *kitu hicho*

**iii) Vivumishi vimilikishi**

*Changu* huwa *chake*

*Wetu* huwa *wao*

*Zetu* huwa *zao*

*Wangu* huwa *wao*

**iv) Vielezi vya wakati**

*Leo* huwa *siku hiyo*

*Sasa* huwa *wakati huo*

*Kesho* huwa siku *iliyofuata*

**v) Maneno ya kuuliza maswali**

*Nini* huwa *kitu ambacho*

*Nani* huwa *mtu ambaye*

*Nyumba gani* huwa *nyumba ambayo*

*Kitu gani* huwa *kitu ambacho*

*Wapi* huwa *mahali ambapo*

### Zoezi la 12.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, badilisheni sentensi zifuatazo ziwe katika kauli taarifa.*

**Kwa mfano:** Wanafunzi wote walisema, "Sisi tunatakiwa kufaulu katika mitihani yote ya muhula huu."

**Jibu:** Wanafunzi wote walisema kwamba wao walitakiwa kufaulu katika mitihani yote ya muhula huo.

1. Seremala mmoja alisema, "Mimi ninaunda vitanda vikubwa."
2. Mfugaji alisema, "Wanyama wetu wanakosa maji."
3. Mwalimu alisema, "Wanafunzi hawa wanaenda kucheza."
4. Mtoto wake alisema, "Mimi nitaenda kuchota maji pamoja na ndugu yangu."
5. Bwana yule aliuliza, "Unataka nini hapa?"

## Tathmini ya mada ya 3

### Zoezi la 1

1. *Katika makundi ya wanafunzi watano watano, andaeni mdahalo kuhusu:* *'**Shule za umma ni bora kuliko shule za kibinafsi**'.*
2. *Katika makundi yenu, jadilini kuhusu majukumu ya wahusika hawa wa mdahalo:*

   a) Mwenyekiti b) Katibu ch) Wapinzani d) Watetezi

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, andaeni mjadala kuhusu:*
*'**Athari za mavazi ya kisasa kwa wanajamii**'.*

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi hizi katika tungo kanushi.*

**Kwa mfano:** Wewe umeimba wimbo mzuri sana

**Jibu:** Wewe **hujaimba** wimbo mzuri sana

1. Yeye ameagiza bidhaa nyingi kutoka Kigali.
2. Mimi nimezunguka mjini kwa gari.

3. Mtoto wangu amefaulu mitihani yake
4. Nyumba yangu imesafishwa.
5. Mgomba umechomwa.
6. Kazi hii imefanywa vizuri.
7. Kitabu chako kimeharibika.
8. Utambi umekauka.
9. Udevu mrefu umenyolewa.
10. Barua imetumwa.

## Zoezi la 4

*Baada ya kukanusha sentensi zilizo katika zoezi la 3 lililo hapo juu, ziandike tena katika wingi.*

**Kwa mfano:** Wewe ***hujaimba*** wimbo mzuri sana (umoja, tungo kanushi)
**Jibu:** Nyinyi hamjaimba (wingi, tungo kanushi)

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi hizi katika wingi.*

**Kwa mfano:** Kisu kimeibiwa
**Jibu:** Visu vimeibiwa.

1. Kiti kimevunjika
2. Mtu huyu ametuimbia vizuri.
3. Mzee huyu amelewa.
4. Mwanafunzi huyu ameelewa somo la Kiswahili.
5. Ng'ombe wangu amezaa leo.
6. Mto huu umefurika.
7. Kiongozi amewasili mapema.
8. Mbwa amekula chakula.
9. Uso wake umeharibika.
10. Mguu wangu umetibiwa vizuri.

## Zoezi la 6

*Baada ya kuandika wingi wa sentensi katika zoezi la 3 lililo hapo juu, ziandike upya katika tungo kanushi.*

**Kwa mfano:** Visu vimeibiwa. (wingi, tungo yakinishi)
**Jibu:** Visu havijaibiwa. (wingi, tungo kanushi)

## Zoezi la 7

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kamilisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:*

***walipiga kura, wanatushawishi, uchumi, dhahiri, kuinua***

1. Kila mwananchi anapaswa kufanya kazi kwa bidii ili ________ kiwango cha maisha yake.
2. ________________ wa nchi yetu utastawi baada ya kuanzisha miradi mingi mizuri.
3. Viongozi hawa ____________ kutumia mbinu za kisasa katika shughuli zetu za kilimo na ufugaji.
4. Ni __________ kwamba raia wa Rwanda walipata maisha mazuri baada ya kuanzishwa kwa shughuli za '*Gira inka Munyarwanda*'.
5. Juzi wanafunzi wote ____________ kwa sababu Mkuu wa shule alitaka orodha ya viongozi wa madarasa yote.

## Zoezi la 8

*Katika makundi yenu, kamilisheni sentensi hizi kwa neno sahihi kati ya haya:*

***aliwahimiza, ufugaji, uzalishaji, wanaunga mkono, maziwa, kilimo***

1. Kiwanda hiki cha kutengeneza mafuta kinaagiza ____________ kutoka kwa wafugaji wengi wilayani Nyagatare.
2. __________ mali unategemea sana shughuli za ________ na ________ kwa sababu shughuli hizo zinafanywa na watu wengi nchini.
3. Watu hawa ________ miradi ya maendeleo ya nchi yetu kwa sababu wanashirikiana sana na viongozi wao.
4. Mkuu wa wilaya yetu ________ wakulima kupanda miti mingi katika mashamba yao.

### Zoezi la 9

*Katika makundi yenu, badilisheni sentensi hizi ziwe katika kauli taarifa.*

1. Rais alisema, “Kila mwananchi anaweza kujitajirisha kwa kufanya kazi kwa bidii.”
2. Mkuu wa shule alisema, “Wanafunzi wawili hawajui kusoma vizuri.”
3. Wafanyakazi walisema, “Hatutaki kufanya kazi na watu wavivu.”
4. Wazazi waliuliza, “Nani anaenda kununua mavazi ya watoto wetu?”
5. Mkulima alisema, “Mvua hainyeshi sana siku hizi.”

### Zoezi la 10

*Katika makundi yenu, badilisheni sentensi hizi ziwe katika kauli asili.*

1. Kalisa alimwambia shangazi yake kuwa kesho yake angeenda Kigali.
2. Bagirishya alisema huku akitetemeka kuwa chumbani mwake mlikuwa na nyoka.
3. Kasisi alituambia kuwa ikiwa tungependa kuendelea vyema maishani, ingebidi tuwe na heshima.
4. Daktari alituambia kuwa UKIMWI ni ugonjwa hatari sana.
5. Baba aliniuliza idadi ya mabao tuliyofungwa mchezoni.

## Faharasa

| | |
|---|---|
| biashara: | shughuli ya kununua na kuuza bidhaa |
| elimu: | mafunzo yanayotolewa kwa watu |
| mwenyekiti: | mtu anayeteuliwa kuongoza chama, mkutano au mjadala |
| hoja: | maelezo ya kupinga au kuunga mkono jambo linalojadiliwa |
| msemaji: | mtu mwenye jukumu la kunena katika mkutano au mjadala; ***mnenaji*** |
| upinzani: | upingaji |
| uchumi: | mapato na matumizi ya watu katika nchi |
| miradi: | shughuli anayofanya mtu inayompatia kipato |
| sekta: | eneo au sehemu yenye shughuli maalumu |
| alitetea: | alipigania hoja yake |
| alipinga: | alikataa; alitofautiana na |
| mdahalo: | mjadala kuhusu mada fulani unaofanywa na watu wenye mitazamo tofauti |
| mjadala: | mazungumzo yanayohusu mada fulani ambayo hufanywa kwa kujenga hoja |
| ufugaji: | kazi ya kutunza wanyama au ndege |
| mkulima: | mtu anayelima shamba lake ili kukidhi mahitaji yake |
| kilimo: | kazi ya kulima na kupanda mazao shambani |
| rutuba: | virutubisho au mbolea ya kutosha kuwezesha mimea kunawiri |
| mifugo: | neno la jumla kwa wanyama wote wafugwao |
| fursa: | nafasi |
| mapato: | pesa au mali inayopatikana kutokana na biashara au baada ya kazi |
| malighafi: | vitu ambavyo hutumika kutengeneza vitu vingine |
| umaskini: | hali ya kutokuwa na mali; ***ukata*** |

# SURA YA NNE

## MADA KUU 4: UIMARISHAJI WA STADI YA UANDISHI NA MASIMULIZI KUPITIA LUGHA YA KISWAHILI

**Mada Ndogo:** **Utungaji wa insha**

## SOMO LA 13: Sehemu kuu za insha


### 13.1 Kifungu kuhusu somo la Kiswahili

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni michoro hii kisha msome kifungu cha habari kilicho hapo chini na kujibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*










Bwana Gasimba ni mwalimu wetu wa somo la Kiswahili. Wanafunzi katika shule ya sekondari ya Mtume Paulo, Rurango wanampenda sana mwalimu huyu. Yeye ni mpole, mwenye bidii katika kazi yake, mcheshi na anayependa kuwasaidia wanafunzi wenye matatizo mbalimbali. Mwalimu huyu anaifahamu lugha ya Kiswahili sana kwani yeye huizungumza kila mahali: sokoni, kanisani, mtaani na hata nyumbani kwake.

Jana, Bwana Gasimba alitufundisha somo la Kiswahili kuhusu uandishi wa insha. Wanafunzi wote walifurahia somo hili sana kwa sababu lilihusisha masimulizi ya kufurahisha. Mwalimu alitusimulia kuhusu siku yake ya harusi, mashindano ya michezo ya timu aliyochezea pamoja na kututolea maelezo kuhusu mazingira ya nchi yetu. Katika somo hili, mwalimu wetu pia alitusomea insha mbalimbali kuhusu madhara ya uvivu, umuhimu wa

malezi bora pamoja na umuhimu wa elimu maishani. Pia, tulifundishwa namna ya kuandika insha bora yenye kuzingatia sehemu zake kuu. Wanafunzi walimsikiliza mwalimu kwa makini huku wakiandika maelezo yote kwenye madaftari yao.

Jioni nilipofika nyumbani nilivua sare yangu, nikaoga kisha nikaenda jikoni kumsaidia mama kutayarisha chakula cha jioni. Kila wakati mama hunishauri kuwa uvivu ni adui wa maendeleo. Baadaye tulikula kwa pamoja chakula cha jioni nami nikachukua kitabu changu ili kufanya marudio ya somo la Kiswahili.

Niliweza kujisomea kuhusu sehemu kuu za insha. Nilielewa kuwa sehemu ya kwanza huwa ni mada. Sehemu hii ni muhimu kwa sababu ndiyo kichwa cha insha. Sehemu ya pili huwa ni utangulizi ambao ndio mwanzo wa insha. Mwalimu alitueleza kuwa utangulizi unafaa kuwa mfupi na humsaidia msomaji kuelewa na kuwa na picha ya mambo muhimu yatakayozungumziwa katika insha nzima. Sehemu nyingine za insha ambazo ni muhimu ni mwili wa insha ambao huhusu kinachozungumziwa katika insha pamoja na hitimisho ambalo huhusisha sentensi chache za kumalizia insha. Kwa vile mwalimu wetu alitueleza haya yote kwa njia wazi niliyaelewa kabisa. Nilijiambia moyoni kuwa kila mara nikiandika insha nitayazingatia yote hayo tuliyofundishwa na mwalimu wetu. Nadhamiria kuwa mwanafunzi bora katika somo la Kiswahili na vilevile katika masomo mengine. Pia, nadhamiria kuepukana na uvivu kwani kama anavyoniambia mama kila wakati uvivu huzuia maendeleo na kufaulu maishani.

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, someni tena kifungu kilicho hapo juu kisha mjibu maswali yafuatayo.*

1. Wanafunzi wa shule ya Mtume Paulo walimpenda mwalimu yupi?
2. Taja tabia za Bwana Gasimba.
3. Mtu ambaye ni mcheshi ni mtu mwenye tabia ya aina gani?
4. Kwa nini somo la insha liliwafurahisha wanafunzi?
5. Katika insha, mada na utangulizi huhusu nini?
6. Katika insha mwili wa insha huhusu nini?
7. Mwanafunzi anahitajika kuandika nini katika hitimisho la insha?
8. Je, umejifunza nini kutokana na kifungu hiki?

## 13.2 Msamiati kuhusu sehemu za insha

*Kutokana na kifungu cha habari ulichosoma hapo juu, katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maana ya msamiati mpya uliojitokeza unaohusiana na sehemu za insha. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika panapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***mada*** – neno au sentensi ambayo inatambulisha jambo linalozungumziwa katika insha iliyoandikwa. Aghalabu mada ya insha huwa haizidi maneno manane.

**Zoezi la 13.1**

A. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kulingana na jinsi ulivyotumika katika kifungu cha habari mlichosoma hapo awali.*

1. ***Somo*** la Kiswahili litaanza kesho saa mbili asubuhi.
2. Mutoni aliandika ***insha*** bora kuliko wanafunzi wenzake.
3. ***Utangulizi*** wa insha yako unavutia.
4. ***Mwili wa insha*** hubeba ujumbe wa insha nzima.
5. Sharti kila insha iwe na ***hitimisho***.
6. ***Masimulizi*** ya mwalimu wetu yalitufurahisha darasani.

B. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika Zoezi 1A lililo hapo juu.*

### Maelezo muhimu!

**Sehemu kuu za insha ni:**

**1. Mada au kichwa cha insha**

Mada ya insha hutambulisha jambo linalozungumziwa katika insha. Mada ya insha haifai kuzidi maneno manane. Mara nyingi mada ya insha huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Lazima mada iwe na mvuto kwa msomaji.

**2. Utangulizi au mwanzo wa insha**

Utangulizi wa insha mara nyingi huwa ni aya moja tu. Unafaa kuvutia kwa kiwango cha juu ili kumpa msomaji hamu ya kutaka kusoma insha nzima.

**3. Mwili wa insha**

Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu inabeba ujumbe kamili wa insha nzima. Aya nyingi huandikwa hapa na ni bora aya hizi ziandikwe kwa namna ya kutiririsha matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha.

**4. Hitimisho au mwisho wa insha**

Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyoandikwa katika mwili wa insha kwa namna ya kuvutia msomaji.

## 13.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha mjadili kuhusu sehemu kuu za insha mnazozifahamu. Hakikisheni kuwa mmejibu maswali haya.*

1. Mada ya insha huhusu nini?
2. Utangulizi wa insha huandikwa kwa kuzingatia mambo gani?
3. Mwili wa insha huhusu nini?
4. Hitimisho huandikwa vipi?
5. Lugha inayotumika kuandika insha huwa ya aina gani?

## 13.4 Kusikiliza na kuzungumza: Somo la imla

**Zoezi la Imla**

Sikiliza kwa makini sentensi utakazosomewa na mwalimu wako kisha uzinakili katika daftari lako kwa kuzingatia alama sahihi za uandishi.

## 13.5 Sarufi

### Ngeli ya U-ZI

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha msome aya ifuatayo na mworodheshe majina yaliyo katika ngeli ya U-ZI.*

Bwana Gasimba anaishi katika nyumba nzuri na kubwa inayoonyesha utajiri wake. Nyumba yake ina vyumba vingi. Kuta za vyumba hivi zimepakwa rangi ya kupendeza. Bwana Gasimba huwa na furaha kila wakati. Uso wake huwa na tabasamu kwa kila mtu. Wafanyakazi wake hutumia fagio kufagia vyumba vyote. Bwana Gasimba ana mazoea ya kutembea na ufunguo wa gari lake zuri mkononi. Nyimbo nzuri kutoka katika chumba cha kuwapokea wageni hufurahisha sana.

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia maneno mliyoorodhesha hapo juu.*




**Maelezo muhimu!**

Majina katika ngeli ya U-ZI katika sentensi hutumia kiambishi nafsi '***u-***' katika umoja na kiambishi nafsi '***zi-***' katika wingi.

**Kwa mfano:**

1. ***Ukuta*** wa nyumba yangu ***u***mepakwa rangi.
   ***Kuta*** za nyumba zetu ***zi***mepakwa rangi.
2. ***Wimbo*** mzuri ***u***meimbwa na mtoto.
   ***Nyimbo*** nzuri ***zi***meimbwa na watoto.

## Mifano ya majina na michoro yake katika ngeli ya U-ZI

| Umoja | Wingi |
|---|---|
|  1. **Ufunguo** |  **Funguo** |
|  2. **Ulimi** |  **Ndimi** |
|  3. **Upanga** |  **Panga** |
|  4. **Uzi** |  **Nyuzi** |
|  5. **Ukucha** |  **Kucha** |

*A. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kanusheni sentensi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** Ufunguo mpya umepotea.

**Jibu:** Ufunguo mpya haujapotea.

1. Ulimi wake umepona.
2. Upanga huu utatumika kukatia muwa.
3. Uzi wangu umekatika.
4. Ukucha wako umeumia.
5. Wimbo mrefu utaimbwa na wanafunzi.

*B. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi mlizokanusha hapo juu katika wingi.*

**Zoezi la 13.2**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi katika umoja na wingi kwa kutumia majina yafuatayo katika hali yakinishi.*

**Kwa mfano:** Fito

**Jibu:** ***Ufito*** mrefu utatumiwa kujengea nyumba.

***Fito*** ndefu zitatumiwa kujengea nyumba.

1. kurasa
2. ndevu
3. wakati
4. nyembe
5. upanga
6. ulimi

**Zoezi la 13.3**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, kanusheni sentensi mlizotunga katika zoezi la 13.2 lililo hapo juu.*

### 13.5.1 Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya sifa

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini sentensi zinazofuata (zenye michoro na picha) kisha mwelezane maneno yaliyopigiwa mistari ni ya aina gani.*



1. Ukuta ***mrefu*** umejengwa.




Kuta ***ndefu*** zimejengwa.



2. Uzi ***mwekundu*** umenunuliwa.



Nyuzi ***nyekundu*** zimenunuliwa.




3. Wembe ***mpya*** umenunuliwa.




Nyembe ***mpya*** zimenunuliwa.



4. Uso ***safi*** una kidonda.



Nyuso ***safi*** zina vidonda.

### Maelezo muhimu!

Maneno ambayo hutumiwa kutoa maelezo zaidi kuhusu nomino huitwa ***vivumishi***. Vivumishi vinavyoeleza namna nomino inavyoonekana na tabia ya nomino huitwa ***vivumishi vya sifa***.

**Mifano:**

1. Ukuta ***mrefu*** umejengwa.
2. Uso ***safi*** umepakwa mafuta.
3. Ukucha ***mchafu*** utakatwa.
4. Ufagio ***mpya*** utanunuliwa.

### Zoezi la 13.4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tambueni vivumishi vya sifa katika sentensi zinazofuata.*

**Kwa mfano:** Ufito mrefu umekatwa.

**Jibu:** '*mrefu*' ni kivumishi cha sifa

a) Wimbo mzuri umeimbwa na wanafunzi hawa.

b) Ukurasa mweupe umechafuliwa na mtoto yule.

ch) Fagio mpya zitauzwa sokoni na mama yangu.

d) Uzi mweusi utatumiwa kushonea nguo yake.

e) Ndevu ndefu zitanyolewa kesho.

### Zoezi la 13.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi hivi.*

**Kwa mfano:** -refu

**Jibu:** Waraka ***mrefu*** umeandikwa na Kabera.


1. -chafu
2. safi
3. -eusi
4. -kubwa
5. -dogo

## SOMO LA 14: Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha

### 14.1 Kifungu kuhusu malezi bora

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro ifuatayo kisha mjadili na mwelezane mnachokiona na hapo baadaye msome kifungu cha habari kilicho hapo chini na kujibu maswali yanayofuata.*







Malezi bora kwa watoto huanza mara wanapozaliwa. Ni jukumu la kila mzazi kumlea mtoto wake kwa njia zinazofaa na zinazokubalika katika jamii. Kila mtoto hukua kwa kuziiga na kuzifuata tabia za watu wanaomlea.

Wazazi wa Mutesi ni Byiringiro na Uwera. Hawa ni watu wenye bidii katika kazi zao. Mama yake huamka mapema na kuitayarishia familia yake kiamshakinywa, hufagia nyumba, huosha vyombo kisha huondoka kwenda sokoni kufanya biashara ya kuuza vyakula mbalimbali. Baba yake naye huwakama ng’ombe na kuwafungulia kutoka zizini. Tabia hizi za wazazi wake zimemfanya Mutesi kupenda kufanya bidii katika masomo yake na kazi zake za pale nyumbani. Yeye pia huamka mapema na kuwasaidia wazazi wake kufagia nyumba, kupika na hata kuwafungulia ng’ombe kutoka zizini.

Shuleni, Mutesi huongoza takriban katika masomo yote hasa somo la Kiswahili. Wanafunzi wengine hutaka kufanya marudio ya masomo yao naye. Jana jioni Mutesi alikuwa na Ngabo nyumbani kwao wakifanya marudio ya namna ya kuandika insha bora. Mutesi alimweleza Ngabo kuwa kabla ya kuanza kuandika insha yoyote, ni vyema kuelewa mada uliyopewa inahusu nini. Kisha ubuni akilini kisa chochote kuhusiana na mada hiyo. Kisa hicho kiweze kutiririka au kufululiza kutoka mwanzo hadi mwisho kwa kutumia aya kadhaa. Ni bora zaidi kutafuta kisa kilicho na mafunzo mema. Baada ya hapa sasa unaweza kukiandika kisa hicho katika daftari lako. Mambo mengine ya kuzingatia ni kama vile: kuandika kwa mwandiko unaoweza kusomeka kwa urahisi, kuepuka makosa ya kisarufi na kuzingatia urefu unaofaa.

Kila Jumapili, wazazi wa Mutesi huhakikisha kuwa wote wameenda kanisani. Mutesi anafahamu umuhimu wa kumcha Mungu, kuwatii watu wakubwa na hata wadogo, kuwakaribisha wageni vizuri, kusema asante anapofanyiwa jambo zuri au anapopewa kitu chochote. Mutesi amefundishwa umuhimu wa kuwasalimia watu kwa heshima na kutumia lugha yenye adabu. Walimu, wanafunzi na hata majirani wote wanampenda sana Mutesi. Yeye ameiga tabia nzuri za wazazi wake. Yeye ni mfano mwema wa kuigwa na watoto wengine.

## Maswali ya ufahamu

1. Eleza tabia za wazazi wa Mutesi.
2. Mutesi ameiga tabia zipi kutoka kwa wazazi wake?
3. Taja mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandika insha.
4. Malezi bora ni nini?
5. Umejifunza nini kutokana na kifungu ulichosoma hapo juu?

## Maswali ya uhakiki

1. Kifungu ulichosoma kina aya ngapi?
2. Taja majina ya watu waliozungumziwa katika kifungu ulichosoma.
3. Eleza tabia za watu uliowataja kutokana na kifungu ulichosoma.
4. Eleza mawazo makuu yanayozungumziwa katika kila aya.
5. Onyesha aya zinazojenga kila sehemu kuu ya insha uliyosoma.

**Maelezo muhimu!**

- Mkusanyiko wa sentensi ambazo zinazungumzia wazo moja kuu huitwa ***aya***.
- Ili aya ieleweke, sharti mwandishi atumie kwa usahihi alama za uandishi kama vile: *nukta, koma, mkato, herufi kubwa,* n.k.

## 14.2 Msamiati kuhusu uandishi wa insha

*Kutokana na kifungu cha mazungumzo ulichosoma hapo awali, katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maana ya msamiati mpya uliojitokeza na kuhusiana, kisha utunge insha. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika inapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***insha*** – mtungo unaoandikwa kuhusu kitu, mtu au jambo kwa kufululiza maneno katika sentensi hadi katika aya kwa njia ya kusimulia au kuhadithia jambo fulani hatua kwa hatua.

### Zoezi la 14.1

**A.** *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kulingana na jinsi ulivyotumika katika kifungu mlichosoma hapo awali.*

1. Mwalimu ameandika ***aya*** mbili za insha kwenye ubao.
2. ***Mada*** ya insha aliyotupa mwalimu wetu ni rahisi.
3. Sharti ***ubuni*** kisa akilini kabla ya kuandika insha.
4. Insha nzuri inafaa ***kutiririka*** kutoka mwanzo hadi mwisho.
5. Kila mwanafunzi anashauriwa kuwa na ***mwandiko*** safi.
6. Mwalimu wetu hukosoa makosa yote ya ***kisarufi***.
7. Ni jukumu la kila mzazi kumpa mwanawe ***malezi*** mema.
8. Mutesi ***aliziiga*** tabia nzuri za wazazi wake.

**B.** *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi kwa kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi za zoezi la 1A lililo hapo juu.*

**Maelezo muhimu!**

***Insha*** ni mtungo unaoandikwa kuhusu kitu, mtu au jambo kwa kufululiza maneno katika sentensi hadi katika aya kwa njia ya kusimulia au kuhadithia jambo fulani hatua kwa hatua. Insha inaweza kuandikwa katika mpango wa mazungumzo.

**Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha**

1. ***Mwandiko uwe safi:*** Maandishi yaonekane vizuri na yasomeke ili kurahisisha usomaji.
2. ***Urefu:*** Insha iwe na urefu wa wastani (insha isiwe fupi sana na isiwe ndefu sana).
3. ***Lugha ya insha:*** Sharti lugha sahihi, sanifu na rahisi kueleweka itumike ili kumvutia msomaji.

## 14.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha mjadili kuhusu mambo ambayo nyinyi huzingatia katika kuandika insha mbalimbali. Wanafunzi waelezane:*

1. Mada mbalimbali za insha mbalimbali.
2. Mambo wanayozingatia wanapoandika insha.
3. Namna ya kuboresha mwandiko usiofaa.
4. Kiasi cha urefu wa kuandika insha mbalimbali.
5. Mapambo mbalimbali yanayoweza kutumika katika kuandika insha.

## 14.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini kuhusu namna ya kuandika insha bora kwa kuzingatia kifungu mlichosoma hapo awali.*

## 14.5 Sarufi

### Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria


*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni michoro ifuatayo kisha muilinganishe na sentensi zilizo chini yake.*




1. a) Uzi ***huu*** utatumika kushonea nguo.
   b) Uzi ***huo*** utatumika kushonea nguo.
   ch) Uzi ***ule*** utatumika kushonea nguo.




2. a) Ufunguo ***huu*** ni wa gari la mama.
   b) Ufunguo ***huo*** ni wa gari la mama.
   ch) Ufunguo ***ule*** ni wa gari la mama.




3. a) Uso ***huu*** umepakwa mafuta.
   b) Uso ***huo*** umepakwa mafuta.
   ch) Uso ***ule*** umepakwa mafuta.

*Je, mmegundua nini?*

## Zoezi la 14.2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni wingi wa sentensi zinazofuata.*

1. Ukuta huu umekamilika kujengwa.
2. Uso huo una kidonda.
3. Ufagio ule umetumika kwa muda mrefu.
4. Uzi huu unahitajika na mama.
5. Wimbo huo unavutia.
6. Wembe ule ulimkata mtoto.

*Je, mmegundua nini?*

### Maelezo muhimu!

Maneno ambayo hutumiwa kuonyesha umbali wa nomino huitwa ***vivumishi viashiria***. Yaani ni maneno yanayoashiria iliko nomino. Kuna umbali wa aina tatu:

a) ***Karibu na mzungumzaji***

Kwa mfano: *Ukuta huu, uso huu, uzi huu* n.k.

b) ***Mbali kidogo na mzungumzaji***

Kwa mfano: *Ukuta huo. uso huo. uzi huo* n.k.

ch) ***Mbali sana na mzungumzaji***

Kwa mfano: *Ukuta ule, uso ule, uzi ule* n.k.

Vivumishi viashiria katika wingi hutegemea umbali wa nomino inayorejelewa:

a) Katika ngeli ya U-ZI, nomino ikiwa karibu na mzungumzaji, katika umoja kivumishi kiashiria kitakuwa '***huu***' na katika wingi kitakuwa '***hizi***'.

b) Katika ngeli ya U-ZI, nomino ikiwa mbali kidogo na mzungumzaji, katika umoja kivumishi kiashiria kitakuwa '***huo***' na katika wingi kitakuwa '***hizo***'.

ch) Katika ngeli ya U-ZI, nomino ikiwa mbali sana na mzungumzaji, katika umoja kivumishi kiashiria kitakuwa '***ule***' na katika wingi kitakuwa '***zile***'.

## Zoezi la 14.3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni umoja wa sentensi hizi.*

1. Kurasa hizi zimelowa maji.
2. Kucha hizi zitakatwa.
3. Funguo hizo ni za nyumba za walimu wetu.
4. Panga hizi zitatumika shambani.
5. Nyimbo hizo zinaimbwa vizuri sana.

## Zoezi la 14.4

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jazeni nafasi zilizo wazi kwa kuchagua vivumishi viashiria sahihi kutoka kwenye mabano.*

1. Ukuta ____________ umebomolewa. (zile, ule)
2. Fito ____________ zimevunjika. (hizo, hiyo)
3. Nyuzi ____________ za manjano zimeuzwa. (ile, zile)
4. Uso ____________ umevimba. (huu, hii)
5. Nyembe ____________ zitawakata watoto wale. (ile, zile)

## Zoezi la 14.5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia majina yafuatayo ya ngeli ya U-ZI.*

1. Wimbo
2. Waraka
3. Ukuta
4. Udevu
5. Unywele

# SOMO LA 15: Aina mbalimbali za insha

## 15.1 Kifungu kuhusu umuhimu wa adabu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii kisha mwelezane mnachokiona. Tangulizeni sentensi zenu kwa: Mimi ninaona…Hapo baadaye msome kifungu cha habari kilicho hapo chini na kujibu maswali ya ufahamu yanayofuata.*





Mutoni ni mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule ya sekondari ya Muhanga. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii shuleni na ana heshima. Walimu katika shule yake huwaomba wanafunzi wenzake wafuate mfano wake. Mutoni huwa nambari ya kwanza katika darasa lao. Wanafunzi wengi hutamani kuwa kama Mutoni.

Hali ya kimaisha nyumbani kwao ni ngumu. Wazazi wake wana uwezo mdogo wa kumtafutia karo, chakula pamoja na kutimiza mahitaji mengine ya nyumbani. Wanaishi katika nyumba ndogo katika kijiji duni.

Mama yake Mutoni anaugua ugonjwa wa kisukari. Baba yake naye ni mlemavu. Amelemaa mguu mmoja. Yeye hufanya kazi ndogo ndogo ila pesa anazopata hazitoshi kuikimu familia yake.

Walimu wote shuleni wanamjua Mutoni kutokana na uwezo wake mzuri katika masomo yake. Yeye ni mwanafunzi mtiifu, mpole na mwenye bidii na nidhamu. Anapenda kuwasaidia wanafunzi wenzake walio na matatizo katika masomo yao. Tabia hii ndiyo inayowafanya wanafunzi wenzake kumpenda na kumheshimu. Yeye ndiye kiranja mkuu shuleni mwao.

Licha ya sifa nzuri, Mutoni alikuwa hana uwezo wa kununua vitabu na sare ya shule. Sare yake ilikuwa na viraka vingi. Hali hii iliwahuzunisha walimu wake hasa mwalimu wa somo la Kiswahili ambaye aliamua kumsaidia. Alimnunulia sare mpya pamoja na vitabu vyote alivyohitaji. Pia, alimwahidi kumlipia karo ya chuoni iwapo angefaulu katika mtihani wake wa kitaifa.

Ufadhili huu uliwafurahisha wazazi wake. Mutoni aliapa kujikakamua zaidi katika masomo yake. Walipofanya mtihani wa kitaifa, Mutoni alikuwa mwanafunzi wa kwanza katika shule yao na hata wilaya yao. Mutoni na wazazi wake walifurahi sana. Walimshukuru Mungu sana. Mungu alimjaalia akajiunga na chuo kikuu cha Rwanda alikosomea udaktari. Baada ya miaka minne, Mutoni alipata kazi katika hospitali moja iliyoko Gikondo. Hapa ndipo alipopata uwezo wa kuwatibu na kuwatunza wazazi wake. Mutoni aliwajengea wazazi wake nyumba nzuri na kuajiri wafanyakazi wa kuwasaidia kazi za nyumbani. Wazazi wa Mutoni walifurahi sana kwa wema waliotendewa na mwanao.

## Maswali ya ufahamu

1. Eleza sifa za Mutoni.
2. Eleza hali ya familia ya Mutoni.
3. Kwa nini mwalimu wa somo la Kiswahili aliamua kumfadhili Mutoni?
4. Kwa nini wanafunzi walimpenda Mutoni?
5. Kozi ambayo Mutoni aliifanya chuoni ilikuwa na manufaa gani?

## Maswali ya uhakiki

1. Eleza namna mada inavyohusiana na insha uliyosoma.
2. Eleza mawazo makuu matatu yaliyojitokeza katika insha uliyosoma.
3. Andika mawazo hayo kwa maneno yako mwenyewe. Usizidi maneno sabini (70).

## 15.2 Msamiati kuhusiana na umuhimu wa adabu

*Kutokana na kifungu mlichosoma hapo awali, katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu maana ya msamiati mpya. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika panapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***wema*** **-** mambo mazuri anayoyafanya mtu

**Zoezi la 15.1**

**A.** *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, elezeni maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata kulingana na jinsi ulivyotumika katika kifungu mlichosoma hapo awali.*


1. Mutoni anasoma katika ***kidato cha tatu***.
2. Baba yangu amelipa ***karo*** yote ya muhula huu.
3. Mimi sina ***mahitaji*** mengi nyumbani.
4. Wao wanaishi katika ***kijiji duni***.
5. Mama yangu ni ***mpole*** na mwenye bidii.
6. Mutoni ndiye ***kiranja mkuu*** katika shule yao.
7. ***Sare*** za wanafunzi hawa ni mpya.
8. ***Ufadhili*** aliopata kaka yangu uliwafurahisha wazazi wetu.
9. Kamana anasomea kozi ya ***udaktari*** chuoni.

**B.** *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi za Zoezi la 1A.*

## 15.3 Matumizi ya lugha: Mifano ya insha

### 15.3.1 Insha ya wasifu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni michoro hii kisha msome mfano wa insha ifuatayo na mjadili maswali yanayofuata:*






Baba yangu anaitwa John Mugabo. Yeye ni mrefu na mwenye rangi ya ngozi ya maji ya kunde. Baba ana macho mazuri na nywele nyingi nyeusi kichwani. Yeye hupenda kuvalia suti kila wakati isipokuwa Jumamosi tunapoenda kucheza kandanda naye. Baba ni mchezaji hodari sana katika kandanda na yeye hufurahia sana mchezo huu.

Baba yangu ni mwalimu mkuu katika shule ya sekondari ya Kigali. Anaheshimiwa sana na walimu wote, wanafunzi na hata wazazi. Sifa zake nzuri ndizo humfanya baba apendwe na kila mtu. Yeye ni mkarimu, hupenda kuwasaidia watu walio na matatizo mbalimbali, ni mpole, ni mcheshi na mwenye heshima pia kwa wengine. Baba ana bidii sana katika kazi yake. Yeye huamka asubuhi na mapema kwenda kazini.

Mama yangu anampenda sana baba yangu kwa sifa zake nzuri. Baba anajulikana kwa kila mtu mjini Kigali. Wanafunzi wa shule yake hufanya vyema zaidi katika masomo yao chini ya uongozi wa baba yangu. Mimi pamoja na kaka yangu tunampenda sana baba yetu. Nikiwa mkubwa ningependa kuwa kama baba yangu. Mtu mwenye moyo safi kwa kila mtu.

## Maswali ya uhakiki

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadilini maswali yanayofuata kutokana na mfano wa insha ya wasifu uliotolewa hapo juu.*

1. Eleza insha mliyosoma ni ya aina gani.
2. Eleza mambo ya kuzingatia katika kuandika insha ya aina hii.
3. Pendekeza kichwa cha insha hii.
4. Eleza sifa ambazo ni za kimaumbile za baba anayezungumziwa katika insha mliyosoma.
5. Taja tabia za baba anayezungumziwa katika insha mliyosoma hapo juu.
6. Kwa nini watu wengi wanampenda baba huyu?
7. Ni nini kinachoonyesha kuwa baba huyu ana bidii katika kazi yake?

### Maelezo muhimu!


Insha zinazoeleza sifa nzuri au mbaya kuhusu maumbile ya mtu au kitu fulani huitwa ***insha za wasifu***.

## Zoezi la kuandika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni insha ya wasifu wako binafsi.*

## 15.3.2 Insha ya mazungumzo

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni mchoro huu kisha msome mfano wa insha ifuatayo na mjadili maswali yanayofuata:*



**Mgonjwa:** Hujambo daktari?

**Daktari:** Sijambo! Karibu uketi.

**Mgonjwa:** Asante daktari.

**Daktari:** Nikusaidie vipi?

**Mgonjwa:** Jina langu ni Kayitesi. Ninaumwa na tumbo sana.

**Daktari:** Pole sana Kayitesi. Tumbo lilianza kukuuma lini?

**Mgonjwa:** Tangu jana usiku. Hata sijalala. Ninaendesha na kutapika sana.

**Daktari:** Pole sana. Ulikula nini jana usiku?

**Mgonjwa:** Nilikula wali kwa kitoweo cha samaki.

**Daktari:** Mmmmhh! Wewe hunywa maji yaliyochemshwa?

**Mgonjwa:** Si kila siku daktari. Mimi hunywa maji yoyote bora yanayonekana kuwa safi.

| | |
|---|---|
| **Daktari:** | Ni vyema kunywa maji yaliyochemshwa kila siku. Chukua mikebe hii miwili uende pale msalani unileteee choo chako pamoja na mkojo wako ili tupime kujua kinachokudhuru. |
| **Mgonjwa:** | Sawa daktari. Asante. |
| **Daktari:** | Nakusubiri. |

## Maswali ya uhakiki

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini maswali haya kutokana na mfano wa insha mliyoisoma hapo juu.*

1. Eleza insha mliyosoma ni ya aina gani.
2. Eleza mambo ya kuzingatia katika kuandika insha ya aina hii.
3. Pendekeza kichwa cha insha hii.
4. Wazungumzaji katika mazungumzo haya ni kina nani?
5. Eleza kazi ya daktari katika jamii.
6. Daktari anamsaidia vipi Kayitesi?
7. Kayitesi anaugua wapi?

### Maelezo muhimu!

Insha zinazohusu mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi huitwa ***insha za mazungumzo***. Insha hizi huandikwa kwa mtindo wa tamthilia.

## Zoezi la maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, igizeni mazungumzo kati ya Daktari na Mgonjwa (Kayitesi) mliyosoma hapo awali.*

## Zoezi la kuandika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, bunini mazungumzo kati ya mwalimu na mwanafunzi kisha myaigize.*

# 15.4 Kusikiliza na kuzungumza

## Somo la imla


*Sikiliza kwa makini sentensi ambazo mwalimu wako atakusomea kisha uziandike kwa usahihi katika daftari lako.*

## 15.5 Sarufi


### Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha na michoro ifuatayo kisha muiambatanishe na sentensi zilizo chini yake.*

a)




b)




1. a) Uso ***wangu*** umepakwa mafuta.
   b) Nyuso ***zetu*** zimepakwa mafuta.

a)




b)




2. a) Ukucha ***wako*** unapendeza.
   b) Kucha ***zenu*** zinapendeza.

a)




b)




3. a) Waraka ***wake*** umewekwa kwenye bahasha.
   b) Nyaraka ***zao*** zimewekwa kwenye bahasha.

*Je mmegundua nini?*

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zilizo hapo juu. Maneno hayo ni ya aina gani? Yanarejelea nini?*

### Maelezo muhimu!

Maneno ambayo hutumiwa kuonyesha mtu, kitu au hali fulani inamilikiwa na nani huitwa ***vivumishi vimilikishi***. Vivumishi vimilikishi hutegemea nafsi tatu katika lugha ya Kiswahili ambazo ni:

1. Nafsi ya kwanza (Mimi – Sisi): *Uso* ***wangu*** *umeumia.* (umoja)
   *Nyuso* ***zetu*** *zimeumia.* (wingi)
2. Nafsi ya pili (Wewe – Nyinyi): *Uso* ***wako*** *umeumia.* (umoja)
   *Nyuso* ***zenu*** *zimeumia.* (wingi)
3. Nafsi ya tatu (Yeye – Wao): *Uso* ***wake*** *umeumia.* (umoja)
   *Nyuso* ***zao*** *zimeumia.* (wingi)

Vivumishi vimilikishi ni: ***-angu, -etu, -ako,-enu, -ake*** na ***-ao.***
Vivumishi hivi vinatumia kiambishi ***w-*** katika umoja na kiambishi ***z-*** katika wingi (***w****angu,* ***w****ako,* ***w****ake,* ***z****etu,* ***z****enu,* ***z****ao*).

## Mifano katika sentensi

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Wimbo ***wangu*** unavutia. | Nyimbo ***zetu*** zinavutia. |
| 2. Ukuta ***wangu*** umepakwa rangi. | Kuta ***zetu*** zimepakwa rangi. |
| 3. Unywele ***wako*** utanyolewa kesho. | Nywele ***zenu*** zitanyolewa kesho. |
| 4. Uso ***wako*** umevimba. | Nyuso ***zenu*** zimevimba. |
| 5. Uzi ***wake*** umepotea. | Nyuzi ***zao*** zimepotea. |
| 6. Ukurasa ***wake*** umeandikwa. | Kurasa ***zao*** zimeandikwa. |

### Zoezi la 15.2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia majina yafuatayo pamoja na vivumishi vimilikishi vilivyo kwenye mabano.*

**Kwa mfano:** Wimbo (wake)
Jibu: ***Wimbo wake*** ulipendwa na wasikilizaji wote.

1. Kurasa (zetu)
2. Ufa (wako)
3. Nyuzi (zenu)
4. Ufito (wangu)
5. Nyembe (zao)

## Zoezi la 15.3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi zifuatazo katika wingi.*

**Kwa mfano:** Waraka wangu umetumwa.
**Jibu:** Nyaraka zetu zimetumwa.

1. Ubao wake umepakwa rangi nyekundu.
2. Ukuta wako umeangukia nyumba yangu.
3. Ukucha wangu umeumia vibaya.
4. Wakati wako umekwisha.
5. Wimbo wake ulirekodiwa jana mjini Kigali.

## Zoezi la 15.4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi zifuatazo katika umoja.*

**Kwa mfano:** Nyembe kali zitatumika kukata kucha.
**Jibu:** Wembe mkali utatumika kukata ukucha.

1. Ndevu za wavulana wale zimekuwa ndefu sana.
2. Nywele za mabinti hawa ni nyeusi tititi.
3. Nyayo za watoto hao zina matope.
4. Nyakati za kusoma kwa wanafunzi zimekwisha.
5. Nyuso za wazee wale zimepakwa mafuta.

## Zoezi la 15.5

*Andika wingi wa majina haya ya ngeli ya U-ZI.*

1. Wayo
2. Wakati
3. Wimbo
4. Ufito
5. Upinde

## SOMO LA 16: Aina za insha

### 16.1 Kifungu kuhusu madhara ya uvivu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mchoro ufuatao kisha mjadili kuhusu kinachoendelea katika mchoro wenyewe. Hapo baadaye, msome kifungu kilicho hapo chini kuhusu madhara ya uvivu na mjibu maswali yanayofuata.*



Uvivu ni hali ya kutopenda au kutofanya kazi. Hii ni tabia ambayo ni mbaya na isiyokubalika katika maisha ya binadamu. Mtu mvivu hupenda tu kulala sana na kukaa bila kufanya kazi yoyote. Mtu yeyote hawezi kufikia malengo yake ikiwa atakuwa mvivu katika shughuli zake. Mtu mvivu hupatwa na matatizo mengi yakiwemo ukosefu wa chakula, pesa, kujiingiza katika ukorofi na mengineyo.

Uvivu hauna faida yoyote ila una madhara chungu nzima. Mtu asiyefanya kazi bila shaka atakosa pesa za kutimiza mahitaji yake ya kila siku. Ukosefu huu unaweza kumsababisha mtu huyu kujiingiza katika matendo ya uhalifu kama vile wizi na uuaji ili kupata pesa ambazo hakuzitolea jasho. Tabia hii ya wizi inaweza kumfanya mtu huyo kufungwa jela au hata kujeruhiwa na kuuawa na umma.

Mwanafunzi akiwa mvivu hawezi kufaulu katika masomo yake. Masomo yote katika mtaala wa elimu yanahitaji kufanyiwa bidii ili kuyaelewa hivyo

kufanya vyema katika mitihani yao. Lazima mwanafunzi ajitahidi kufika darasani mapema, kumsikiliza mwalimu kwa makini, kufanya kazi zake za ziada kwa wakati na hata kuweza kutenga muda wa kufanya marudio ya masomo yote wanayofundishwa. Mwanafunzi anapofaulu katika masomo yake huwa amepata ufunguo bora wa kufaulu maishani. Mwanafunzi huyu ataweza kupata kazi nzuri hivyo kupata pesa za kumwezesha kuyatimiza mahitaji yake ya kila siku pamoja na ya wanajamii wengine.

Watu wavivu huishia kuwa wasumbufu sana katika jamii. Hii ni kwa sababu wao huwa hawataki kufanya kazi ilhali wanataka wale chakula, wavae nguo na waishi. Kwa jasho la nani? Wengine huishia kuwa ombaomba kila mahali. Watasaidiwa hadi lini? Tabia kama hizi huwaudhi sana wanajamii wengi. Wengine hupatwa na matatizo mengi hadi kuishia kutumia dawa za kulevya kwa lengo la kujisahaulisha matatizo yao. Matumizi ya dawa hizi huwafanya watu hawa kujiingiza katika uhalifu kama vile ujambazi, ubakaji na hata mauaji. Afya zao huathirika sana.

Uvivu huleta umaskini, ujinga na kutoendelea kiuchumi kwa mtu binafsi na kwa nchi kiujumla. Tujiepushe na uvivu kwani uvivu ni adui wa maendeleo katika jamii.

## Maswali ya ufahamu

1. Eleza maana ya uvivu.
2. Eleza madhara ya uvivu.
3. Uvivu huathiri mwanafunzi kwa namna gani?
4. Nchi huathirika vipi kutokana na uvivu?
5. Afya za watu wavivu huweza kuathirika kwa njia gani?
6. Umejifunza nini kutokana na kifungu ulichokisoma?
7. Eleza namna ya kuepukana na uvivu.

## 16.2 Msamiati kuhusu madhara ya uvivu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu mlichokisoma hapo juu na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale inapohitajika.*

## Zoezi la 16.1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.*

1. ***Uvivu*** ni adui wa maendeleo kwa binadamu.
2. ***Dawa za kulevya*** huathiri afya ya mtu anayezitumia.
3. ***Umaskini*** na ujinga husababishwa na uvivu.
4. Mwanafunzi yule alifanya ***bidii*** katika masomo yake na akafaulu.
5. Usipojitahidi katika shughuli zako utaishia kuwa ***ombaomba***.
6. Mtu mvivu huweza kujiingiza katika ***uhalifu***.
7. Kamana ***alijitahidi*** katika mtihani wake wa kitaifa.

## Zoezi la 16.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kamilisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:*

***wasumbufu, dawa za kulevya, masomo, bidii, maendeleo, ombaomba.***

**Kwa mfano:** Watu walio wavivu huishia kuwa ________________ sana katika jamii.

**Jibu:** Watu walio wavivu huishia kuwa ***wasumbufu*** sana katika jamii.

1. ________________ wamejaa mjini.
2. Uvivu huathiri ________________ ya nchi.
3. Mwanafunzi mvivu hawezi kufanikiwa katika ________________ yake.
4. Ubakaji, ukorofi pamoja na matumizi ya ______________ yakomeshwe.
5. Mtu akifanya ______________ katika shughuli zake atafanikiwa.

## 16.3 Matumizi ya lugha: Aina za insha

### 16.3.1 Insha ya maelezo

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni michoro hii kisha msome mfano wa insha ifuatayo na mjadili maswali yanayofuata:*







Maji ni uhai. Mimea, wanyama pamoja na binadamu hawawezi kuishi bila ya kuwepo kwa maji. Maji yakikosekana ulimwenguni kote, viumbe wote wenye uhai wataangamia.

Maji huweza kupatikana katika bahari, ziwa, bwawa, mto na hata chemchemi. Mvua inaponyesha, watu, wanyama pamoja na mimea hupata maji ya kutumia.

Maji yana umuhimu mkubwa sana katika maisha ya binadamu. Binadamu hutumia maji kupikia, kunywa, kufulia nguo, kuogea, kuoshea vyombo na hata kusafishia nyumba. Binadamu huweza kupata chakula kutoka kwa mimea kwa kuinyunyizia maji hivyo kunawiri na kumpatia binadamu mazao mengi. Mimea pia hunyunyiziwa dawa za kuwakinga au kutibu magonjwa fulani. Dawa hizi huwa zimechanganywa na maji.

Wanyama pia huhitaji maji ili kuishi na kukua. Wao hunywa maji hayo. Wanyama hupigwa dawa za kuwakinga dhidi ya magonjwa mbalimbali. Dawa hizo huwa zimechanganywa kwa maji.

Njia nyingine za burudani ambazo huwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi yetu hutumia maji. Kwa mfano, vidimbwi vya kuogelea na maeneo yaliyo na wanyama wanaoishi majini kama vile mamba, kiboko na samaki wa aina mbalimbali.

## Maswali ya uhakiki

1. Waeleze wenzako insha uliyosoma ni ya aina gani?
2. Mambo gani huzingatiwa katika kuandika insha ya aina hii?
3. Eleza umuhimu wa maji kwa binadamu.
4. Eleza umuhimu wa maji kwa mimea.
5. Wanyama hufaidika vipi kutokana na maji?
6. Miti hutusaidia kwa njia ipi kupata maji?

### Maelezo muhimu!

Insha ambazo hutoa taarifa kuhusu mtu, kitu, mahali, hali au jambo fulani huitwa ***insha za maelezo***. Insha hizi huhitaji maelezo ya kweli wala siyo maelezo ya kubuni.

## Zoezi la kuandika

*Andika insha ya maelezo kuhusu vivutio vya utalii katika nchi ya Rwanda.*

## 16.3.2 Insha ya barua rasmi

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni mfano wa insha ifuatayo kisha mjadili maswali yanayofuata.*

Mary Mutoni,
Shule ya sekondari ya Gikondo,
S.L.P 4200,
GIKONDO.
20/03/2017

Kwa Mwalimu Mkuu,
Shule ya sekondari ya Gikondo,
S.L.P 4200,
GIKONDO.

Kwa Bw,
<u>KUH: KUOMBA RUHUSA YA KUPUMZIKA</u>
Ninaandika barua hii ili kuomba ruhusa ya kukosa kuhudhuria masomo yote ya leo. Jana sikuweza kuja shuleni kwa sababu niliamka nikijihisi mgonjwa. Mama alinipeleka hospitalini ambapo nilipata matibabu. Ninaugua malaria. Bado sijapata nafuu. Naendelea kumeza dawa nilizopewa.
Naomba uniruhusu nimalize dawa kisha nikipata nafuu nitarejea shuleni. Samahani sana kwa kutosema hili mapema.
Natumai utanielewa na kuniwia radhi.
Asante.
Wako mwaminifu,

Mary Mutoni.

### Maswali ya uhakiki

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini maswali haya kwa kurejelea mfano wa insha mliyosoma hapo juu.*

1. Eleza insha mliyosoma ni ya aina gani.
2. Eleza mambo ya kuzingatia katika kuandika insha ya aina hii.
3. Pendekeza kichwa cha insha hii.
4. Anwani ngapi zimetumika katika barua hii? Ni za kina nani?
5. Lengo la kuandika barua hii ni lipi?

**Zoezi la kuandika/Utafiti**

1. Tunga mfano wa barua ya kirafiki.
2. Eleza namna ya kuandika barua ya mwaliko. Buni mfano mmoja wa barua ya mwaliko.
3. Ni mambo gani huzingatiwa katika kuandika:
   i) Barua rasmi
   ii) Barua ya kirafiki
   iii) Barua ya mwaliko

## 16.4 Kusikiliza na kuzungumza

### Somo la imla





i) Sikiliza kwa makini insha ambayo mwalimu wako atakusomea kisha uiandike katika daftari lako.

ii) Kwa kufuata mfano wa insha uliyosomewa na mwalimu wako, buni insha yako mwenyewe inayofanana na hiyo.

## 16.5 Sarufi

### Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni michoro ifuatayo kisha muiambatanishe na sentensi zilizo chini yake.*

| | |
|---|---|
| <br>1. Ufunguo ***mmoja*** umepatikana. | <br>Funguo ***saba*** zimepatikana. |
| <br>2. Upanga ***mmoja*** umenunuliwa. | <br>Panga ***mbili*** zimenunuliwa. |
| <br>3. Wembe ***mmoja*** utatumika. | <br>Nyembe ***tatu*** zitatumika. |

*Je, mmegundua nini?*
*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zilizo hapo juu. Maneno hayo ni ya aina gani? Maneno hayo yanarejelea nini?*

## Zoezi la 16.3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia majina yafuatayo pamoja na vivumishi vya idadi.*

**Kwa mfano:** nyembe nane

**Jibu:** Mwalimu alinunua ***nyembe nane*** kutoka dukani.

1. Kuta (mbili)
2. Fagio (tatu)
3. Teo (nne)
4. Uzi (mmoja)
5. Nyuso (tano)
6. Nyaraka (kumi)

### Maelezo muhimu!

Maneno ambayo hutumiwa kutaja hesabu, idadi au kiasi cha vitu au viumbe fulani huitwa ***vivumishi vya idadi***.

Vivumishi vya idadi hugawika katika aina mbili:

***i)*** ***Vivumishi vya idadi kamili***, kwa mfano: *ukuta* ***mmoja****, kuta* ***nne****, uso* ***mmoja****, nyuso* ***tano****, upanga* ***mmoja****, panga* ***nane,*** n.k.

**Mifano katika sentensi:**

a) Uzi *mmoja* umepotea.
b) Nyuzi *tano* zimepotea.
ch) Ukuta *mmoja* umejengwa.
d) Kuta *nne* zimejengwa.

***ii)*** ***Vivumishi vya idadi isiyo kamili***, kwa mfano: *kuta* **chache**, *kurasa* **nyingi**, *nyimbo* **kadhaa**, *nyaraka* **tele,** n.k.

**Mifano katika sentensi:**

*a) Nyimbo nyingi ziliimbwa jana.*
*b) Nyaraka kadhaa zimepotea.*

## Zoezi la 16.4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia majina yafuatayo pamoja na vivumishi vya idadi.*

1. Wimbo (mmoja)
2. Kurasa (nyingi)
3. Nyufa (mbili)
4. Uzi (mmoja)
5. Fito (kadhaa)
6. Nyembe (chache)

### Zoezi la 16.5

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jazeni nafasi zilizo wazi katika sentensi zinazofuata kwa kutumia vivumishi vya idadi sahihi kutoka kwenye mabano.*

**Kwa mfano:** Nyaraka ______________ zimesomwa. (wanne, nne, zinne)

**Jibu:** Nyaraka ***nne*** zimesomwa.

1. Ulimi ______________ umeumia. (moja, mmoja, umoja)
2. Fito ______________ zitatumika kujengea. (nyingi, vingi, wingi)
3. Nyimbo ____________ zimetungwa na baba yake. (chache, uchache, wachache)
4. Nyuso ______________ zimepakwa mafuta. (tano, watano, vitano)
5. Ufagio ______________ uliuzwa jana. (moja, mmoja, umoja)

## Tathmini ya mada ya 4

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi kwa kutumia majina yafuatayo ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi mlivyopewa kwenye mabano.*

1. Wimbo (wao)
2. Kurasa (zake)
3. Nyufa (zetu)
4. Uzi (wangu)
5. Fito (zenu)
6. Nyembe (zako)

### Zoezi la 2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, kanusheni sentensi hizi.*

1. Utepe wangu ulipotea.
2. Kucha zenu zinapendeza.
3. Upanga wake ulivunjika.
4. Wimbo wa taifa unaimbwa sasa.
5. Wakati wa mapumziko umewadia.

### Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andikeni sentensi za zoezi la 2 lililo hapo juu katika umoja au wingi hali yakinishi.*

### Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tambueni vivumishi vya sifa katika sentensi zifuatazo.*

1. Udevu mfupi hautakatwa.
2. Ukuta mpana utapakwa rangi.
3. Funguo nyepesi zimeanguka.
4. Wembe mzee ulinikata.
5. Ubao mweusi utatumika.

### Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tungeni:*

1. Wasifu kuhusu shule yako.
2. Mazungumzo kati ya mzazi na mtoto wake.

### Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu madhara ya uvivu katika jamii hasa kwa mwanafunzi.*

**Faharasa**

somo: maarifa maalumu ambayo hufundishwa shuleni

insha: mtungo ulioandikwa kwa lugha ya mjazo kuhusu tukio au kitu fulani

utangulizi: mwanzo

mwili wa insha: sehemu ya mtungo (insha) inayobeba ujumbe kamili wa mtungo huo

hitimisho: mwisho

masimullizi: maelezo (usimuliaji) wa jambo au tukio

malezi: namna ya kumlea mtoto kwa taratibu zinazokubalika katika jamii

zizini: mahali wanapolala ng'ombe

aya: fungu la maneno lenye maana au ujumbe kamili

mada: anwani au kichwa cha insha

ubuni: utunge

kutiririka: kufuatana kwa mtiririko au mfuatano fulani

mwandiko: namna ya uandikaji wa mtu; hati

maendelezo: namna ya utaratibu wa kuandika maneno

kisukari: ugonjwa unaotokana na mwili kushindwa kudhibiti kiwango cha sukari kwenye damu

kidato cha tatu: darasa la tatu katika kiwango cha sekondari

karo: malipo yanayotolewa ili kupata mafunzo au maarifa fulani

mahitaji: jumla ya vitu muhimu kwa ajili ya kutimiza haja ya mtu

kijiji duni: sehemu yenye hali mbaya ya kimaisha kwa watu wanaoishi hapo

mpole: mwenye utulivu

ufadhili: usaidizi wa kifedha

# SURA YA TANO

## MADA KUU 5: LUGHA NA TEKNOLOJIA

**Mada Ndogo:** **Kiswahili katika teknolojia ya habari na mawasiliano**

## SOMO LA 17: Simu ya mkononi

### 17.1 Mazungumzo kuhusu matumizi ya simu ya mkononi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha zifuatazo kisha mwelezane vifaa mnavyoona pamoja na matumizi na umuhimu wake. Baadaye, msome kifungu cha mazungumzo kilicho hapo chini na mjibu maswali yanayofuata.*








**Baba:** (*Akiingia sebuleni*) Habari za mchana mke wangu?

**Mama:** Njema mume wangu. Karibu. Simu hii imenisumbua sana leo. Tangu nilipoipokea sijafahamu matumizi yake hadi sasa.

**Baba:** Simu imefanya nini? Tafadhali nieleze. Mambo ya teknolojia haya mke wangu!

**Mama:** Wajua simu hii bado ni mpya na sijajua jinsi ya kuitumia vyema! Simu hii ya kugusa badala ya kubofya vidude…

**Baba:** Enhee! Simu uliyonunuliwa na mwanao huko mjini Kigali? Usiwe na hofu, utajua matumizi yake polepole.

**Mama:** Asante sana. Jana nimemwandikia mwana wetu huyo arafa. Nikamweleza kuwa nimepokea simu…sikumweleza kuwa simu hii mpya inanitatiza kimatumizi (*akicheka*).

**Baba:** Ulifanya vyema sana. Hata hivyo, ingekuwa bora sana kama ungempigia simu badala ya arafa.

**Mama:** Mume wangu kwani unafikiri hata kuandika arafa hiyo ilikuwa kazi rahisi? Ilinitatiza sana. Unajua simu hii siyo ya kubofya ni ile ya kugusa tu halafu inakupa dunia nzima ya mambo!

**Baba:** (*Akicheka)* Yapi tena? Pole kwa kutatizika. Huku kijijini bado tuko nyuma sana kimaendeleo na kiteknolojia.

**Mama:** Sijui kamera, instagramu, fesibuku, Biblia, kamusi… mengi (*akicheka*).

**Baba:** Naona mawasiliano yatakuimarikia kwa hii simu mpya uliyonunuliwa.

**Mama:** Nashukuru. Binti yangu amenieleza kuwa bila intaneti mtu hawezi kusoma habari za fesibuku wala watisapu.

**Baba:** Hayo ni kweli kabisa. Kakwambia nini tena?

**Mama:** Simu hii inahitaji chaji nyingi ili isizime. Pia, nilielezwa kuwa kutumia watisapu, kusoma habari za mtandaoni pamoja na matumizi mengine yanahitaji hela nyingi.

**Baba:** (*Akiinamisha kichwa.*) Hayo uliyoambiwa ni kweli. Tatizo jingine ni kuwa huku kijijini pia hatuna mitambo ya kunasia mawimbi ya kutumika kwenye simu. Wakati mwingine inambidi mtu apande juu ya kilima ili kuwasiliana kwa simu. Tena aina hii ya simu ikianguka chini inaweza kupasuka kiwambo chake haraka sana hivyo kuharibika na isitumike tena.

**Mama:** Licha ya matatizo hayo mengi, nafurahia tu kupata simu hii kwa sababu ninaweza kufanya mambo mengi nayo. Naweza kupiga picha na hata kusoma taarifa za kiulimwengu.

**Baba:** Hali itakuwa shwari baada ya kuitumia kwa muda. Utaweza kuyafanya mambo mengi zaidi.

**Mama:** Kweli mume wangu. Tatizo jingine ni kwamba aina hii ya simu inafaa kutumika na wanaojua kusoma sana. Sisi wazee zinatutatiza.

**Baba:** Sharti twende na wakati. Hii ni dunia ya teknolojia.

**Mama:** Nakubaliana nawe. Sharti tujikakamue.

**Baba:** Kweli (*wanaingia ndani ya nyumba*).

## Maswali ya ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu cha mazungumzo yaliyo hapo juu kisha mjibu maswali yanayofuata.*

1. Taja wazungumzaji katika kifungu cha mazungumzo ulichosoma hapo juu.

2. Bila shaka mazungumzo yanahusiana na teknolojia. Kwa nini? Eleza.
3. Taja chombo cha mawasiliano kilichozungumziwa.
4. Orodhesha matumizi yoyote mawili ya simu ya mkononi waliyotaja wazungumzaji.
5. Mama ana matatizo gani kuhusiana na simu yake mpya?
6. Kulingana na baba, ni mambo gani ambayo huathiri matumizi ya simu ya mkononi kijijini kwao?
7. Teknolojia ni nini? Eleza kwa maneno yako mwenyewe.
8. Taja msamiati wa adabu ambao umetumika katika kifungu cha mazungumzo mliyoyasoma.

## 17.2 Msamiati kuhusu simu ya mkononi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu cha mazungumzo mlichosoma na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 17.1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.*

1. ***Simu ya mkononi*** ambayo mama alinunuliwa inamsaidia sana.
2. ***Teknolojia*** katika nchi yetu imekua kwa kiwango kikubwa.
3. Simu ya babu yangu ni ya ***kubofya vidude***.
4. Dada yangu aliye ng'ambo alinitumia ***arafa*** kwenye simu yangu.
5. Baba ***atampigia*** mwalimu wetu simu ili kuniombea ruhusa.
6. Simu mpya aliyonayo ni ya ***kugusa*** kwenye ***kiwambo*** chake.
7. Simu yangu ina ***kamera*** nzuri sana.
8. ***Intaneti*** ni muhimu sana katika matumizi ya simu.

## Zoezi la 17.2

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kamilisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:*

***arafa, watisapu, kunasia mawimbi, fesibuku, simu, chaji***

**Kwa mfano:** Baba alinunua ______________ mpya baada ya ile ya kwanza kuibwa.

**Jibu:** Baba alinunua ***simu*** mpya baada ya ile ya kwanza kuibwa.

1. Sharti simu iwe na ________________ ili iweze kutumika.
2. Watu wengi siku hizi wanatumia _______________ na ________________ kuwasiliana.
3. Mitambo ya ______________ katika kijiji chetu imeharibika.
4. Kaka alinitumia _____________________ kunijulisha kuhusu gari jipya alilonunua.

## 17.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni mchoro na picha zifuatazo kisha mwelezane kinachoendelea kwa kurejelea:*

i) Vifaa vya mawasiliano unavyoviona;
ii) Matumizi ya kila kifaa cha mawasiliano unachokiona;
iii) Umuhimu wa kila kifaa cha mawasiliano unachokiona;
iv) Kasoro au udhaifu wa kila kifaa cha mawasiliano unachokiona.









### Maelezo muhimu!

Kifaa cha kutuma taarifa kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia simu huitwa ***faksi***. Taarifa inayotumwa pia huitwa ***faksi***. Huhusisha matumizi ya umeme. Faksi ni aina ya barua au ujumbe unaotumwa kwa njia ya mashine inayoitwa faksi. Maelezo machache yanayofafanua ujumbe pekee hutumika.

## 17.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, igizeni mazungumzo mliyosoma hapo juu kati ya Baba na Mama.*

## 17.5 Sarufi

### Hali ya kuomba, tungo yakinishi

***A.*** *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zinazofuata kisha mwelezane ugunduzi wenu na baadaye mjibu zoezi l7.3 linalofuata.*

1. Tafadhali nipigie simu unapofika nyumbani.
2. Tafadhali imba wimbo wa taifa.
3. Tafadhali cheza mpira wa miguu.
4. Tafadhali pikeni mihogo kwa kuku.
5. Tafadhali zungumza lugha ya Kiswahili sanifu pekee.

**B.** *Badilisheni sentensi mlizosoma hapo juu kwa kutumia '**naomba**'.*

### Maelezo muhimu!

Msamiati wa adabu ambao hutumika kuomba mtu akutendee hisani fulani ni kama vile: ***tafadhali, naomba,*** n.k.

### Zoezi la 17.3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi tano sahihi katika hali ya kuomba, wakati uliopo.*

## SOMO LA 18: Matumizi ya tarakilishi

### 18.1 Kifungu kuhusu matumizi ya tarakilishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu mnachokiona katika mchoro na picha ifuatayo na mwelezane maana na matumizi yake. Baada ya hapo, msome kifungu cha habari kilicho hapo chini na mjibu maswali yanayofuata.*





Mapendekezo ya kuwa na mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto nchini Rwanda yana umuhimu mkubwa sana kwa elimu ya watoto wanaosoma. Mradi huu utawawezesha watoto kupata ujuzi wa kiteknolojia. Watoto wengi watafahamu maana ya tarakilishi, matumizi yake na faida zake katika elimu yao. Watoto wataweza kupata majibu ya maswali yao mengi kupitia kwa mtandao. Itakuwa rahisi kupata maana ya maneno, maelezo na taarifa muhimu kuhusu mada yoyote wanayofundishwa kwa kutumia tarakilishi. Tarakilishi huwa na kamusi ya msamiati mbalimbali, maelezo na istilahi ambazo ni rahisi kupata kwa haraka.

Mtandao umeufanya ulimwengu kuwa kama kijiji kidogo. Kupitia kwa tarakilishi, ni rahisi kuelewa utamaduni wa wanajamii wengine na pia kushirikiana na kutangamana nao. Hii ni kwa sababu watu wanaweza kutafuta habari muhimu kutoka kwenye mitandao kuhusu lugha, mavazi, vyakula na sherehe za watu na jamii nyingine.

Matumizi ya tarakilishi yamechangia katika kuyatunza mazingira yetu kwa kupunguza matumizi ya karatasi nyingi. Hili limechangia katika kupunguza ukataji ovyo wa miti ambao ndicho chanzo cha kuharibu misitu yetu. Rwanda ni miongoni mwa nchi safi sana duniani kutokana na matumizi haba ya karatasi na sandarusi.

Kupitia kwa tarakilishi, kiwango cha masomo kimeimarika sana. Watu wengi hasa wanafunzi wanaweza kujisomea kwa kufanya utafiti wao wenyewe na kufanya mazoezi mbalimbali kwenye mtandao.

Katika kuwezesha mawasiliano, kuna matumizi ya fesibuku na watisapu ambayo yanapendwa sana na watumizi vijana. Fesibuku ni huduma ya kutuma na kupokea arafa pamoja na picha ama video. Fesibuku ina faida kama vile: mtu anaweza kutuma na kupokea picha, video na hata nyimbo, majibu yake ni ya haraka, unaweza kutangaza bidhaa pale na kupata wanunuzi, taarifa husambazwa kwa haraka, ni njia rahisi ya kuhifadhi taarifa mbalimbali miongoni mwa nyingine. Fesibuku pia ina madhara yake kwani inaweza kuwafedhehesha wazazi na watoto ama wafanyakazi na waajiri wao. Mara nyingi watu husambaza taarifa chafu pamoja na picha chafu zikiwemo za watu walio uchi ama wanaofanya uhalifu.

Isitoshe, wahalifu na walanguzi wa dawa za kulevya huutumia mtandao wa fesibuku kuuza dawa za kulevya na kusambaza habari za ugaidi. Watu wengi wamelaghaiwa pesa na hata wengine hasa wanawake kuuawa na watu waliopatana nao tu kwenye fesibuku. Watisapu ni huduma iliyo ndani ya simu au tarakilishi kwa njia ya mtandao ambapo tu anaweza kupokea na kutuma taarifa kwa njia ya arafa, kupigia simu, kutuma na kupokea nyimbo, picha na video.

Upungufu mkubwa wa watisapu ni kwamba bila ya kuwa na simu au tarakilishi iliyowezeshwa, huwezi kupokea huduma hii. Isitoshe, ina gharama ya juu kwani lazima ununue bandali za intaneti.

Aidha, elimu, uchumi na jamii imeathirika kutokana na matumizi ya watisapu. Vijana wa shule na wafanyakazi wengine hupoteza muda mwingi wakiwasiliana na wenzao na kwa hivyo kupoteza muda mwingi wa masomo ama kazi.

Barua pepe ni ujumbe unaotumwa kwa njia ya kielektroni kupitia kwa tarakilishi au simu ya mkononi iliyounganishwa kwenye mtandao.

Barua pepe huwa ni njia ya haraka ya kupata ujumbe na kupokea majibu. Huhifadhi wakati na ni nafuu kuliko kuandika barua ya kawaida. Upungufu wake mkubwa ni kwamba, bila kuwa na mtandao ni njia isiyowezekana kutumika. Isitoshe inahitaji umeme. Pia, sharti mwenye kutuma na kupokea awe na anwani, kwa mfano: *kiswahili@gmail.com* ama *kiswahili@yahoo.com.*

## Maswali ya ufahamu

1. Taja faida zozote mbili za mradi wa tarakilishi kwa wanafunzi.
2. Taja faida zozote mbili za tarakilishi kwa watu kwa ujumla.
3. Jina jingine la tarakilishi ni lipi?
4. Mtandao hufanya ulimwengu kuwa kama kijiji kimoja. Kweli au la? Kivipi? Eleza.
5. Jadili upungufu mkubwa wa watisapu kulingana na kifungu ulichosoma.
6. Pendekeza anwani nyingine mwafaka kwa taarifa hii.
7. Je, teknolojia ina manufaa gani kwa nchi? Taja manufaa matano.
8. Eleza madhara yanayoweza kusababishwa na tarakilishi.
9. Matumizi ya tarakilishi yanawezesha vipi utangamano wa wanajamii mbalimbali?
10. Jadili matumizi, umuhimu na madhara ya:
    a) Fesibuku    b) Watisapu    ch) Barua pepe

## 18.2 Msamiati kuhusu matumizi ya tarakilishi

*Jipangeni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mtafute maana ya msamiati mpya katika kifungu mlichosoma hapo awali. Tafuteni maana ya msamiati huo kulingana na matumizi yake katika kifungu hicho. Tumieni kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 18.1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi hizi kisha mtunge sentensi zenu kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.*

1. ***Teknolojia*** imeufanya ulimwengu kuwa kama kijiji kidogo.
2. ***Tarakilishi*** ina manufaa mengi kwa binadamu.
3. ***Mtandao*** humwezesha mtafiti kupata taarifa nyingi.
4. ***Mradi*** wa tarakilishi kwa kila mwanafunzi utafaulu.
5. Mimi huisoma ***kamusi*** ya Kiswahili kwenye tarakilishi.
6. Tunaweza kuzifahamu ***tamaduni*** za jamii jirani kupitia kwa mtandao.
7. Wanajamii mbalimbali ***hutangamana*** kupitia kwa mtandao.
8. ***Akaunti*** yangu ya ***fesibuku*** imefungwa.
9. ***Watisapu*** yangu imejaa picha tele za harusi ya kaka yangu.
10. Nimeipata ***barua pepe*** aliyonitumia Kamana.


## 18.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni picha hizi kisha mzijadili na kuziambatanisha na sentensi zilizo hapo chini kwa usahihi.*

A





B




CH




D




1. Barua pepe ya rais wa Marekani ina jumbe nyingi sana.
2. Watisapu yangu ina jumbe nyingi sana.
3. Barua pepe niliyomtumia mwalimu mkuu haijajibiwa.
4. Ninataka kufungua akaunti yangu ya fesibuku.

### Zoezi la makundi

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu umuhimu wa tarakilishi kwa kuwaeleza wenzako:*

1. Maana ya tarakilishi.
2. Njia za mawasiliano kupitia tarakilishi unazozifahamu.
3. Faida za tarakilishi kwa watumizi.
4. Madhara ya tarakilishi kwa watumizi.

## 18.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu kuhusu matumizi ya tarakilishi kisha mjadili kuhusu:*

1. Faida za mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto nchini Rwanda.
2. Kasoro za mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto.
3. Mapendekezo yako kuhusiana na namna ya kuuboresha mradi huu.
4. Nchi nyingine ambazo zimewahi kutekeleza mradi huu wa tarakilishi kwa kila mtoto.
5. Madhara na umuhimu wa kutumia:
   a) Fesibuku
   b) Barua pepe
   ch) Watisapu

## 18.5 Sarufi

### Hali ya kuomba, tungo kanushi

**A.** *Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, chunguzeni sentensi zinazofuata kisha mwelezane ugunduzi wenu.*

1. Naomba uitoe simu hiyo kwenye chaji.
2. Tafadhali iwashe tarakilishi hiyo.
3. Tafadhali nunua mfuko wa kubebea tarakilishi yako.
4. Tafadhali naomba uniazime kitabu chako.
5. Naomba unileteе kalamu hiyo.

**B.** *Katika makundi yenu, chunguzeni sentensi zinazofuata kisha mwelezane ugunduzi wenu.*

1. Naomba usiitoe simu hiyo kwenye chaji.
2. Tafadhali usiiwashe tarakilishi hiyo.
3. Tafadhali usinunue mfuko wa kubebea tarakilishi yako.
4. Tafadhali usiniazime kitabu chako.
5. Naomba usiniletee kalamu hiyo.

*Je, mmegundua nini?*

### Maelezo muhimu!

***Tarakilishi*** ni chombo cha mawasiliano ambacho hufanana na runinga na hutumia intaneti. Tarakilishi huhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa pamoja na kuongoza mitambo mbalimbali.

## Zoezi la 18.2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa teknolojia ufuatao katika hali ya kuomba, tungo kanushi.*

**Kwa mfano:** Tafadhali usiharibu tarakilishi ya baba.

1. Mtandao
2. Simu ya mkono
3. Intaneti
4. Kompyuta
5. Televisheni
6. Fesibuku
7. Watisapu
8. Baruapepe

## Zoezi la 18.3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, badilisheni sentensi zifuatazo kutoka katika hali ya kuomba yakinishi hadi katika hali ya kuomba kanushi.*


**Kwa mfano:** Naomba unipigie simu usiku.
**Jibu:** Naomba usinipigie simu usiku.


1. Tafadhali nunua televisheni nyingine.
2. Naomba unitengenezee simu yangu.
3. Naomba uninunulie bandali za intaneti.
4. Tafadhali mtoto huyo atumie tarakilishi yangu.
5. Naomba uniandikie baruapepe kesho asubuhi.

## SOMO LA 19: Redio na runinga

### 19.1 Kifungu kuhusu matumizi ya redio na runinga

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni mchoro na picha zifuatazo kisha mjadili kuihusu. Baadaye, msome kifungu kilicho hapo chini kuhusu matumizi ya redio na runinga na mjibu maswali yanayofuata.*







Nchini Rwanda, redio na runinga ni vyombo ambavyo wananchi huvitegemea sana katika kupata habari mbalimbali kutoka maeneo mengi. Kupitia vyombo hivi wananchi huweza kusikia kuhusu kinachoendelea nchini mwao kuhusu masuala ya uongozi, kilimo, elimu, biashara, jamii, uchumi, michezo, siasa pamoja na habari za kimataifa. Vyombo hivi hutangaza taarifa mbalimbali kwa kuzirusha hewani. Anayerusha matangazo hewani kwa kutumia vyombo hivi anaitwa ***mtangazaji.*** Vyombo hivi husikika kupitia kwa ***mawimbi*** fulani.

Kupitia redio na runinga tunapata ***matangazo*** mbalimbali kama vile: matangazo ya kibiashara, taarifa za habari, matangazo ya mpira, matangazo ya kielimu, taarifa za kisiasa, habari kuhusu uchumi wa nchi, matangazo ya tanzia (vifo) na kadhalika. Vyombo hivi vina uwezo wa kucheza miziki mbalimbali kwa ajili ya kuwaburudisha wasikilizaji pamoja na watazamaji. Isitoshe, wasikilizaji na watazamaji hujifundisha lugha na fasihi kupitia vipindi vyenye nyimbo na ngoma mbalimbali, mashairi na vipindi vya kielimu kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo.

Utamaduni wetu pia huweza kusambazwa kupitia kwa vipindi hivyo pamoja na nyimbo zinazochezwa kupitia kwa redio pamoja na runinga.

Matangazo na vipindi huwezekana kwa sababu kuna wafanyakazi kadhaa wanaowezesha shughuli hiyo. Watu hao ni kama vile mkuu wa redio au runinga. Huyu huhakikisha kuwa kuna mpangilio, sera na utaratibu unaofaa wa kuandaa na kurusha matangazo hewani. Mfanyakazi wa pili ni mwandishi wa kipindi ama ***produsa***. Yeye hutayarisha habari zote muhimu ambazo zinafaa kupeperushwa hewani na namna zitakavyopeperushwa. Ubora wa vipindi unamtegemea yeye. Hatimaye kuna mtangazaji. Huyu ndiye wenzo unaopitisha ujumbe kwa sauti (kwenye redio) na kwa kuonekana (kwenye runinga) hadi umfikie msikilizaji pamoja na mtazamaji. Msikilizaji ni mtu yeyote anayetega sikio lake ili kusikiliza ujumbe kupitia kwa kituo cha redio. Mtazamaji na msikilizaji wa runinga husikiliza na pia kutazama picha kuhusiana na habari zinazotangazwa.

Madhara ya vyombo hivi vya habari ni kuwa habari zilizo potovu zinaweza kupeperushwa na kuwaathiri wananchi. Watoto huweza kutazama miziki na filamu chafu katika runinga na hivyo kuathiri maadili yao. Watu wengi huiga mavazi na mitindo ya wanamiziki, wanasiasa na waigizaji katika runinga. Hili huweza kuathiri maadili ya kijamii. Wanafunzi na watu wengi kwa ujumla hupoteza muda wao mwingi kukaa chini na kutazama runinga. Kitendo hiki kinaweza kuathiri ufanyaji wa kazi mbalimbali pamoja na kusoma shuleni.

## Maswali ya ufahamu

1. Eleza umuhimu wa redio na runinga kwa binadamu.
2. Redio na runinga hufundisha lugha na fasihi kwa njia gani?
3. Taja mifano mitatu ya msamiati wa redio na runinga.
4. Habari za kimataifa ni habari gani?
5. Taja mifano ya matangazo katika redio na runinga.
6. Ni kazi gani ya mtangazaji kulingana na kifungu ulichosoma?
7. Eleza maana ya '*msikilizaji*' na '*mtazamaji*' kwa kurejelea kifungu ulichosoma.
8. Taja vituo vya redio na runinga unavyovijua nchini mwako.
9. Eleza madhara ya redio na runinga kwa binadamu.
10. Eleza tofauti iliyopo kati ya redio na runinga.

## 19.2 Msamiati kuhusu matumizi ya redio na runinga

*Kutokana na kifungu cha habari mlichosoma hapo awali, katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu maana ya msamiati mpya uliojitokeza na unaohusiana na matumizi ya redio na runinga. Kamusi ya Kiswahili inaweza kutumika panapohitajika.*

**Kwa mfano:**

***redio:*** chombo kinachopokea mawimbi ya sauti kutoka hewani ili mtu asikie habari, ujumbe au muziki unaochezwa kupitia kituo cha redio

**Zoezi la 19.1**

A. *Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mchunguze maana ya msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi hizi. Tumieni kamusi inapohitajika.*

1. Watu wengi wanapenda kutazama ***runinga***.
2. Baba anasikiliza ***habari*** za kisiasa kwenye redio Rwanda.
3. Taarifa za habari zimepeperushwa ***hewani*** kwa wasikilizaji na watazamaji.
4. Kaka yangu ni ***mtangazaji*** katika kituo cha runinga cha Rwanda.
5. ***Mawimbi*** ya sauti katika redio yetu yanasikika vizuri.
6. ***Matangazo*** ya biashara yameshakamilika.
7. Hawa ni ***watazamaji*** wa filamu ya watoto kwenye runinga.
8. ***Mkuu wa redio*** katika kituo chao ametuzwa.
9. Mimi ninapenda kutazama ***vipindi*** mbalimbali kwenye runinga.

**B.** *Katika makundi yenu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi za Zoezi la kwanza A.*

## 19.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Jigaweni katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha mjadili kuhusu matumizi ya redio na runinga kwa kuwaeleza wenzako:*

1. Vipindi ambavyo unapenda kutazama kwenye runinga.
2. Vipindi ambavyo unapenda kusikiliza kwenye redio.
3. Mafunzo unayoyapata kutokana na vipindi unavyopenda kutazama na kusikiliza.
4. Watangazaji unaowapenda kwenye runinga na sababu za kuwapenda.

5. Watangazaji unaowapenda kwenye redio na sababu za kuwapenda.
6. Madhara ya redio na runinga kwa binadamu.

**Zoezi la 19.2**

*Jigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mjadili kuhusu tafsiri ya msamiati wa teknolojia mliopewa hapo chini.*

| **Kiingereza** | | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| a) *Mobile phone* | – | simu ya mkononi, rununu |
| b) *SMS (Short message)* | – | arafa |
| ch) *Email* | – | barua pepe |
| 1. *Website* | | |
| 2. *Internet* | | |
| 3. *Computer* | | |
| 4. *Whatsup* | | |
| 5. *Facebook* | | |
| 6. *Mouse* | | |
| 7. *Television* | | |

## 19.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, igizeni namna ya kutangaza habari au vipindi mbalimbali* kwenye *runinga na redio. Mzingatie lugha ya Kiswahili sanifu.*

## 19.5 Sarufi: Hali ya kuamrisha, tungo yakinishi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zinazofuata kwa kuzisoma kwa sauti kisha mwelezane ugunduzi wenu.*

1. ***Imba*** wimbo wa taifa.
2. ***Cheza*** mpira wa miguu.
3. ***Nenda*** usome kitabu hiki.
4. ***Pika*** muhogo kwa kuku.
5. ***Zungumza*** Kiswahili sanifu pekee.

*Je, mmegundua nini?*

### Maelezo muhimu!

Kitendo cha kutoa maagizo ya kufanyika kwa tendo fulani huitwa ***kuamrisha***.

**Kwa mfano:**

1. ***Nenda ukalale!***
   Katika sentensi hii, kuna agizo la mzungumziwa kwenda kulala.
2. ***Njoo hapa!***
   Katika sentensi hii, kuna agizo la mzungumziwa kwenda aliko mzungumzaji.

## Zoezi la 19.3

*Tungeni sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo kwa njia ya kuamrisha katika hali yakinishi.*

**Kwa mfano:** washa (televisheni)


**Jibu:** Nenda uiwashe televisheni ile.

1. Andika (baruapepe)
2. Tengeneza (tarakilishi)
3. Jibu (simu)
4. Tuma (arafa)
5. Fundisha (teknolojia)
6. Sikiliza (redio)
7. Tazama (runinga)
8. Soma (fesibuku)
9. Fungua (watisapu)
10. Nunua (gazeti)

# SOMO LA 20: Barua kwa mhariri

## 20.1 Kifungu kuhusu barua kwa mhariri

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni mchoro na picha zifuatazo kisha mwelezane mnachokiona. Baadaye, msome kifungu kilicho hapo chini na mjibu maswali yanayofuata.*





NEWTIMES

DROUGHT: KIGALI IN WATER SHORTAGE

Munyeshyaka, Bucyibaruta in French court this week

'Genocide lesson for all of us'

BELGIAN DEFENCE CHIEFS HERE

RWIGARA STILL ELUDING ARREST


IMVAHO NSHYA

Ibirimo

Umutekano wacu ntawawumeneramo-Kagame




Magazeti yana umuhimu mkubwa sana katika upashaji wa habari. Idadi kubwa ya watu ulimwenguni sasa ina uwezo wa kuandika na kusoma. Wengine hutegemea magazeti kupata habari mbalimbali. Hali siyo tofauti nchini Rwanda. Magazeti maarufu ni pamoja na *Rwanda Times, Muhabura, KT Press, The Rwanda Focus, Izuba Rirashe, Umuseke* miongoni mwa mengine.

***Barua kwa mhariri*** ni sehemu muhimu sana kwenye gazeti. Sehemu hii humpa msomaji fursa ya kutoa hisia zake kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Masuala yenyewe yaweza kuwa ya kutahadharisha, kupongeza, kuhimiza, kukosoa, kushtaki jambo ama kulalamika. Sehemu hii huwa jukwaa muhimu kwa wasomaji wa magazeti mbalimbali. Barua hizo zikishamfikia mhariri, yeye huamua ni masuala yapi yatachapishwa na ni yapi ambayo hayatachapishwa. Muhimu ni kwamba, barua hizo huwa zinalenga kusomwa na wasomaji wengine wa magazeti husika.

Barua kwa mhariri huwa na sifa nyingi. Miongoni mwa sifa hizo ni kwamba, barua huwa na mada na mada huhusu masuala yanayofahamika na yanayowaathiri watu pakubwa.

Mifano ya mada zinazoweza kushughulikiwa ni pamoja na: mafuriko, uongozi, siasa, uchumi, biashara, michezo, afya, athari za teknolojia, uhalif, n.k.
Aghalabu katika barua ya aina hii, jina la mwandishi hutajwa. Mtindo wa barua hii huwa mtindo wa barua rasmi lakini inapotokea kwenye gazeti, yanayochapishwa ni mtajo na ujumbe husika pamoja na jina la mwandishi. Kiini cha ujumbe wa mwandishi hubainika mara moja katika mwili wa barua yenyewe.
Soma mfano huu wa barua kwa mhariri ambayo Mutoni aliandika:

***Kwa mhariri,***
***Ninakupongeza kwa kuchapisha maoni ya wasomaji wa gazeti hili. Maoni yao ni muhimu kwa kutathmini hisia za wananchi kuhusu masuala ya kijamii na hasa kuhusu tabia za vijana siku hizi. Utumizi wa dawa za kulevya unazidi kuwa tatizo kubwa duniani na hasa katika nchi za barani Afrika.***
***Vijana wengi wanadhani kutumia dawa za kulevya ndio mtindo wa kisasa wa kuishi na kustarehe. Kutokana na fikra hizi mbaya na potovu, vijana wengi wameharibu mustakabali wao ikiwemo afya yao. Kuna visa vingi ambapo baadhi ya vijana wamevurugika kiakili na hata wengine kufa kwa sababu ya utumizi mwingi wa dawa za kulevya kwa kusukumwa na marika yao. Vijana wa kike aghalabu hujipata wamenajisiwa kwa sababu ya kutojielewa na kutofahamu lolote baada ya kutumia dawa za kulevya. Matokeo ya hali hii yanaweza kuwa: kupata mimba zisizotarajiwa, kupata magonjwa ya zinaa kama vile: UKIMWI, kisonono, kaswende na mengine.***
***Vijana wote wanafaa kufahamu kuwa matumizi ya dawa za kulevya yana athari mbaya kwao.***
***Mutoni K.***

## Maswali ya ufahamu

1. Taja sifa mbili za barua kwa mhariri.
2. Mwandishi wa barua kwa mhariri uliyosoma ni nani?
3. Pendekeza mada ya barua kwa mhariri uliyosoma.
4. Eleza hitimisho la barua kwa mhariri uliyosoma.
5. Kwa nini gazeti ni muhimu katika suala hili la barua kwa mhariri?
6. Taja magazeti yoyote muhimu nchini mwenu.
7. Eleza athari za dawa za kulevya kulingana na barua kwa mhariri uliyosoma.
8. Vijana wanaweza vipi kujizuia na matumizi ya dawa za kulevya.

## 20.2 Msamiati kuhusu barua kwa mhariri

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni msamiati mpya kutoka katika kifungu mlichosoma na kuueleza. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu hicho na mtumie kamusi pale inapohitajika.*

### Zoezi la 20.1

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi zifuatazo kisha mtunge sentensi zenu sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.*

1. Wananchi wengi hupenda kusoma ***magazeti*** kila siku.
2. Mutoni anaandika ***barua*** hii ili ichapishwe kwenye gazeti la *Rwanda Times*.
3. Hawa ni ***wasomaji*** wa gazeti la *Umuseke*.
4. Tutawapasha wananchi ***habari*** kuhusu mfumo mpya wa elimu.
5. ***Masuala*** yaliyopendekezwa na wasomaji ***yatachapishwa*** kwenye gazeti.
6. Sharti barua utakayoandika iwe na ***mada*** maalum.
7. Bw. Gasimba ndiye ***mhariri*** wa gazeti la *Muhabura*.
8. ***Barua kwa mhariri*** huandikwa kwa mtindo wa ***barua rasmi***.
9. Tujiepushe na matumizi ya ***dawa za kulevya***.
10. Matumizi ya dawa za kulevya huathiri ***mustakabali*** wa vijana wengi.

## 20.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilini kuhusu barua kwa mhariri ambayo umewahi kusoma kwa kuwaeleza wenzako:*

1. Barua hiyo ilikuwa imechapishwa katika gazeti gani?
2. Barua hiyo ilikuwa imehaririwa na nani?
3. Barua hiyo ilikuwa inahusu nini?
4. Ulijifunza nini kutokana na barua hiyo?

### Zoezi la kuandika

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni barua kwa mhariri itakayochapishwa katika gazeti la **KT Press**. Chagua mada yoyote.*

**Maelezo muhimu!**

Barua ambayo huandikwa na kutumwa kwa mhariri wa gazeti fulani kuhusu suala lolote linaloathiri jamii na baada ya utathmini kuchapishwa kwenye gazeti huitwa ***barua kwa mhariri***.

***Sifa za barua kwa mhariri***

- Huwa fupi na yenye ujumbe mahususi.
- Huangazia masuala muhimu sana katika jamii.
- Hutumia lugha sanifu na rahisi kueleweka kwa wasomaji wote.

## 20.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

*Katika makundi ya wanafunzi watano watano, kila mwanafunzi awasomee wenzake barua aliyoandika kwa mhariri hapo awali. Mjadili kuhusu:*

1. Barua inahusu nini?
2. Barua imeandikwa na nani na kwa lengo gani?
3. Barua imefuata mtindo wa kuandika barua kwa mhariri?

## 20.5 Sarufi: Hali ya kuamrisha, tungo kanushi

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, chunguzeni sentensi hizi kisha mwelezane ugunduzi wenu.*

1. a) Mwandikie mhariri barua kuhusu uchumi.
   b) Usimwandikie mhariri barua kuhusu uchumi.
2. a) Andika baruapepe hii na uitume haraka.
   b) Usiandike baruapepe hii na usiitume haraka.
3. a) Piga simu hiyo sasa hivi.
   b) Usipige simu hiyo sasa hivi.
4. a) Washa runinga tutazame na kusikiliza taarifa ya habari.
   b) Usiwashe runinga tutazame na kusikiliza taarifa ya habari.
5. a) Tumieni tarakilishi hizo vyema.
   b) Msitumie tarakilishi hizo vyema.

*Je, mmegundua nini?*

### Zoezi la 20.2

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, kanusheni sentensi zifuatazo katika hali ya kuamrisha.*

**Kwa mfano:** Funga mlango huo!

**Jibu:** Usifunge mlango huo!

1. Kimbia dukani ukanunue sukari!
2. Nipe redio hiyo ya Kamana!
3. Njoo hapa!
4. Kula chakula hicho haraka!
5. Fagia nyumba hii yote!
6. Mpeleke mgonjwa huyu hospitalini!
7. Endesha gari hilo polepole!
8. Tembea upesi!

### Zoezi la 20.3

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo katika hali ya kuamrisha, tungo kanushi.*

**Kwa mfano:** Rudi

**Jibu:** Usirudi mahali umetoka!

1. lia
2. chagua
3. andika
4. toroka
5. danganya

## Zoezi la kuandika: Insha

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni insha kuhusu:*
***Manufaa ya teknolojia shuleni.***

## Tathmini ya mada ya 5

### Zoezi la 1

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafsirini msamiati huu kutoka katika lugha ya Kiingereza hadi katika lugha ya Kiswahili.*

**Kwa mfano:** *Computer*

**Jibu:** Tarakilishi

1. *Radio*
2. *Laptop*
3. *Email*
4. *Internet*
5. *WhatsApp*
6. *Newspaper*
7. *Editor*
8. *News Anchor*

### Zoezi la 2

1. *Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni madhara ya vyombo hivi vya mawasiliano.*
   a) Redio
   b) Runinga
2. *Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, elezeni faida au umuhimu wa vyombo hivi vya mawasiliano.*
   a) Tarakilishi
   b) Simu ya mkononi
3. *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, husisheni maelezo haya na chombo cha mawasiliano kinachorejelewa.*

   **Kwa mfano:** Huonyesha picha na sauti ______________________

   **Jibu:** ***Runinga/ tarakilishi***

   i) Hutoa sauti pekee ______________________
   ii) Huhifadhi na kuchanganua habari zilizowekwa humo ___________
   iii) Hutangaza habari kwa njia ya kusomwa tu ______________________
   iv) Pia huitwa rununu ______________________

## Zoezi la 3

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kanusheni sentensi hizi:*

a) Tafadhali someni taarifa ya habari.
b) Tafadhali acheni siasa mbaya.
ch) Tafadhali tuombe Mungu wetu.
d) Tafadhali lindeni wanyamapori wetu.
e) Tafadhali tuishi vyema na majirani.

## Zoezi la 4

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadiliana na wenzako faida na upungufu wa arafa (ujumbe wa simu ya mkononi).*

## Zoezi la 5

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, yakinisheni sentensi zifuatazo.*

1. Tafadhali usizime televisheni.
2. Tafadhali usiwatumie baruapepe.
3. Tafadhali usiwashe redio kunaponyesha.
4. Tafadhali usihifadhi arafa niliyokutumia kwenye simu hiyo.

## Zoezi la 6

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, yakinisheni sentensi hizi.*

a) Tafadhali msikate miti ovyo.
b) Tafadhali msijizuie na ugonjwa wa UKIMWI.
ch) Tafadhali msipocheza mtakuwa wagonjwa.
d) Tafadhali msitupeleke tulikotoka.
e) Tafadhali asiniandikie barua akifika nyumbani.

## Faharasa

**faksi**: ujumbe unaotumwa kwa njia ya mashine inayoitwa faksi

**televisheni**: chombo kinachonasa picha, sauti na maandishi kutoka katika kituo cha kurushia matangazo

**tarakilishi**: pia ***kompyuta***. Hii ni mashine ya kielektroniki ambayo ina uwezo wa kuhifadhi na kuchanganua habari au taarifa zilizoingizwa na kuhifadhiwa huko ndani ya mtambo

**barua pepe:** ujumbe unaotumwa kwa njia ya kielektroniki kupitia kwa tarakilishi iliyounganishwa kwenye mfumo wa mtandao

**mtandao**: mfumo wa vitu kama vile wa simu ama umeme na wa kimawasiliano ya kielektroniki unaopitia kwenye tarakilishi unaotumiwa kutafuta habari kwa njia ya kupeana na kupokea taarifa

**redio**: chombo maalum ambacho hupokea mawimbi ya sauti na kutoa ujumbe hewani kwa njia ya taarifa; ujumbe, habari ama matangazo. Pia ni mfumo wa utangazaji wa kurusha sauti kwenye hewa

**fesibuku**: huduma ndani ya simu au tarakilishi inayotoa nafasi kwa njia ya mtandao kwa watu ili kuwasiliana kwa kutuma na kupokea ujumbe

**watisapu**: huduma ndani ya simu au tarakilishi kwa njia ya mtandao ambapo mtu anaweza kuweka picha yake, kutuma na kupokea ujumbe na hata kuhifadhi taarifa mbalimbali

**teknolojia**: maarifa ya sayansi yaliyowekwa katika matumizi ya vyombo kama mitambo ya ufundi wa mawasiliano

**simu ya mkononi**: simu inayofanya kazi kwa mfumo wa kielektroniki na inayopata mawimbi na mtu anaweza kuwasiliana na mwingine bila kuwa imeunganishwa na nyaya; pia huitwa ***simu tamba*** au ***rununu***.

**arafa**: ujumbe mfupi ambao hutumwa kwa kutumia simu ya mkononi

## MAREJELEO

BAKITA (2015); *Kamusi Kuu ya Kiswahili*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Mbaabu I. (1992); *Sarufi ya Kiswahili*; Longman; Nairobi, Kenya.

Mdee, J.S. , na wenzake (2011) *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Ntawiyanga, S. na wenzake (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 1*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Ntawiyanga, S. na wenzake (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

TUKI (2009); *Stadi za Lugha ya Kiswahili*; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili, kidato cha tatu*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili, kidato cha Pili*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Kagwa F. M. (2003); *Darubini ya Kiswahili*; Phoenix Publishers; Nairobi, Kenya.